# UCHANGANUZI WA KAULI KATIKA SENTENSI ELEKEZI YA KISWAHILI SANIFU: MTAZAMO WA NADHARIA YA UBANIFU

NA

MODGEN CHISIA

TASNIFU ILIYOWASILISHWA KUTIMIZA BAADHI YA MAHITAJI YA SHAHADA YA UZAMILI KATIKA MASOMO YA SANAA – SWAHILI STUDIES KATIKA CHUO KIKUU CHA NAIROBI

IDARA YA ISIMU NA LUGHA

OKTOBA, 2012

University of NAIROBI Library
0389222 1

## IKIRARI

Tasnifu hii ni kazi yangu binafsi na kadri ya uelewa wangu, haijawahi kuwasilishwa katika chuo kingine chochote kwa madhumuni ya kutimiza mahitaji ya kiusomi.

..............................

MODGEN CHISIA ..........1/11/2012..........

Tasnifu hii imewasilishwa kwa madhumuni ya kutahiniwa kwa idhini yetu kama wasimamizi wake katika Chuo Kikuu cha Nairobi.

..............................

Dkt. IRIBE MWANGI ..........07/11/2012..........

..............................

Dkt. PRISCA JERONO ..........6/11/2012..........

## YALIYOMO

YALIYOMO ............ iii
TABARUKU ............ iv
SHUKRANI ............ v
MUHTASARI ............ vii
ORODHA YA VIFUPISHO ............ viii

1.0. SURA YA KWANZA ............ 1
1.1. Utangulizi ............ 1
1.1.1 Dhana ya Kauli na Sentensi Elekezi ............ 1
1.2. Tatizo la Utafiti ............ 3
1.3. Madhumuni ya Utafiti ............ 4
1.4. Nadharia Tete ............ 4
1.5. Uhalalishaji ............ 4
1.6. Upeo na Mipaka ............ 5
1.7. Msingi wa Nadharia ............ 6
1.7.1. Utangulizi ............ 6
1.7.2. Dhana Muhimu katika Nadharia ya Ubanifu ............ 8
1.7.2.1. Mifanyiko ya Kimkokotoo ............ 8
1.7.2.2. Kanuni ya Ukaguzi Sifa ............ 10
1.7.2.3. Nafasi ya Mofolojia katika Nadharia ya Ubabifu ............ 14
1.8. Kudurusu yaliyoandikwa Kuhusu Mada ............ 17
1.8.1. Utangulizi ............ 17
1.8.2. Yaliyoandikwa Kuhusu Kauli ............ 17
1.8.3. Yaliyoandikwa Kuhusu Nadharia ............ 20
1.9. Mbinu za Utafiti ............ 22
1.10. Umuhimu wa Utafiti ............ 23

**2.0. SURA YA PILI: DHANA ZA UNYAMBUAJI NA UAMBISHAJI ............ 24**
2.1. Utangulizi ............ 24
2.1.1. Unyambuaji ............ 24
2.1.2. Uambishaji ............ 25

2.1.3. Tofauti kati ya Unyambuaji na Uambishaji ........................................ 25
2.1.3.1.Upambanuzi wa Kisintaksia ........................................ 26
2.1.3.2. Uzalishaji ........................................ 26
2.1.3.3. Taratibu za kimaana ........................................ 27
2.1.3.4. Mabadiliko ya kategoria ........................................ 27
2.1.3.5. Mazingira ya udhihirikaji ........................................ 28
2.2. Uambishaji wa Vitenzi ........................................ 28
2.2.1. Viambishi Awali ........................................ 29
2.2.1.1. Viambishi awali vya ukanushi ........................................ 29
2.2.1.2. Viambishi vya nafsi na ngeli ........................................ 30
2.2.1.3. Viambishi vya Njeo ........................................ 32
2.2.1.4. Viambishi vya hali ........................................ 34
2.2.1.5. Kiambishi cha masharti ........................................ 36
2.2.1.6. Kiambishi –ka- ........................................ 36
2.2.1.7. Viambishi vya uwezekano na masharti –nge-, -ngali- na –ngali- ........................................ 37
2.2.1.8. Kiambish Kirejeshi ........................................ 38
2.2.1.9. Viambishi vya yambwa/shamirisho ........................................ 39
2.2.1.10. Kiambishi cha Mrejeo sabaki ........................................ 40
2.2.1.11. Kiambishi cha Namna ........................................ 40
2.2.1.12. Kiambishi tupu cha mwala ........................................ 41
2.2.1.13.Viambishi vya mahali na wakati ........................................ 41
2.2.2. Viambishi Tamati ........................................ 42
2.2.2.1. Kiishio ........................................ 42
2.2.2.2. Kiambishi tamati cha ukanushi ........................................ 43
2.2.2.3. Viambishi vya amri, rai na himizo ........................................ 43
2.2.2.4. Kiambishi Tamati cha Urejeshi ........................................ 45
2.2.2.5. Viambishi vya mahali na wakati ........................................ 45
2.2.2.6. Kiambishi tamati cha namna ........................................ 46
2.3. Hitimisho ........................................ 46
2.4. Tanbihi ........................................ 47

**3.0. SURA YA TATU: VITENZI NA KAULI KATIKA KISWAHILI SANIFU .......... 48**
3.1. Utangulizi ........................................ 48
3.2. Vitenzi vya Kiswahili Sanifu ........................................ 48

3.2.1. Uainishaji wa Vitenzi (T) ......50
3.2.1.1. Vitenzi Vikuu ......51
3.2.1.2. Vitenzi Visaidizi (Ts) ......52
3.2.1.3. Vitenzi Vishirikishi (t) ......54
3.2.1.3.1. Vitenzi Vishirikishi Vikamilifu ......55
3.2.1.3.2. Vitenzi Vishirikishi Vipungufu ......55
3.2.1.4. Vitenzi Elekezi ......56
3.2.1.5. Vitenzi visoelekezi ......57
3.2.1.6. Vitenzi Visoukomo ......57
3.3.0. Kauli za Vitenzi ......59
3.3.1. Kauli Katika Vitenzi vya Asili ya Kibantu ......61
3.3.1.1 . Kauli ya kutendea ......61
3.3.1.2. Kauli ya kutendewa ......63
3.3.1.3. Kauli ya Kutendwa ......63
3.3.1.4. Kauli ya Kutendana ......64
3.3.1.5. Kauli ya kutendeana ......64
3.3.1.6. Kauli ya Kutendesha ......65
3.3.1.7. Kauli ya Kutendeshwa. ......68
3.3.1.8. Kauli ya Kutendeshana ......68
3.3.1.9. Kauli ya Kutendua ......69
3.3.1.10. Kauli ya Kutendata ......70
3.3.1.11. Kauli ya Kutendama ......70
3.3.0. Kauli katika Vitenzi vya Mkopo ......71
3.3.1. Kauli ya kutendea ......71
3.3.2. Kauli ya Kutendewa na Kutendwa ......72
3.3.3. Kauli ya Kutendana na Kutendeana ......73
3.3.4. Kauli ya Kutendesha ......74
3.3.5. Kauli ya Kutendeshwa ......74
3.3.6. Kauli kutendeshana ......75
3.3.7. Kauli ya Kutendesheana ......75
3.4.0. Hitimisho ......75
3.5.0. Tanbihi ......77

**4.0. SURA YA NNE: UCHANGANUZI WA KAULI ........ 78**
4.1. Utangulizi ........ 78
4.2. Kauli ya Kutendea ........ 81
4.3. Kauli ya Kutendwa ........ 83
4.4. Kauli ya Kutendewa ........ 85
4.5. Kauli ya Kutendeana ........ 87
4.6. Kauli ya Kutendana ........ 90
4.7. Kauli ya Kutendesha ........ 92
4.8. Kauli ya Kutendeshea ........ 95
4.9. Kauli ya Kutendeshana ........ 98
4.10. Kauli ya Kutendeshwa ........ 99
4.11. Hitimisho ........ 101

**5.0. SURA YA TANO: HITIMISHO NA MAPENDEKEZO ........ 102**
5.1. Hitimisho ........ 102
5.2. Mapendekezo ........ 105
MAREJELEO ........ 106

## TABARUKU

Ninaitabaruku tasnifu hii kwa marehemu nyanyangu Damara ambaye alikuwa mlezi, mshauri na mhimili wangu mkuu katika uchanga wangu.Matokeo ya kazi hii ni sehemu ya maelekezo yake kwamba 'aliyefanya jambo lisiishe ni kama asiyelianza'. Ufanisi huu mdogo ni jumla ya juhudi zake nyanya kuniongoza mimi mjukuu wake katika 'njia bora ya elimu na maisha ya kweli'.

## SHUKRANI

Katika kazi ya aina hii ni muhali kutoa shukrani kwa maandishi kwa jumla ya watu wote waliohusika kwa kuwataja majina. Hata hivyo, ninastahabu kutaja wachache kwa kuniauni nilipohitaji msaada wao.

Shukrani zangu za dhati ni kwa Maulana aliyeihifadhi siha yangu katika kipindi chote tangia mwanzo hadi mwisho wa kazi hii. Nilipopata senene, hasa nilipokuwa nikishughulikia sura ya pili, Mola alinirejeshea afya na nikawa buheri tena ili niendeleze shughuli hii. Asante kwa umbali ulionileta Jalali.

Wasimamizi wangu wawili, Dkt. Prisca Jerono na Dkt. Iribe Mwangi wamenifaa pakubwa katika ushauri na uvumilivu wao. Bila kuonekana kana kwamba ninatia chuku wema wao, ninashukuru kwamba nilibahatika kupata wasimamizi wanaotekeleza majukumu yao kwa utaalamu na udhati usiomithilishwa. Uvumilivu na uelewa wao nilipolimatia kwa senene ni mambo yaliyonipa ilhamu ya kuendelea 'kulisukuma gurudumu hili la usomi'. Sikumbuki hata wakati mmoja nilipohitaji ushauri wenu mkakosa kunipa. Dkt. Iribe na Dkt. Jerono kwenu ninasema 'shukrani kwa kazi mliyonifanyia kuniongoza katika ulimwengu wa Isimu'.

Idara ya Isimu na Lugha imebarikiwa wahadhiri wenye wema na vipaji anuwai. Nilibahatika kufundishwa na idadi kubwa ya wahadhiri hawa kuanzia miaka ya kwanza katika Chuo Kikuu cha Nairobi. Ninaomba kuwataja kwa mpito kwa fadhila waliyonitendea. Mwenyekiti wa Idara Profesa John Habwe, Dkt. Rayya Timmamy na Dkt. Ayub Mukwana asanteni sana kwani, japo hamlijui hili, sauti zenu katika kipindi cha makuzi ya Kiswahili miaka ya tisini katika redio ya KBC ndiyo yaliyopanda mbegu za mapenzi yangu kwa lugha hii adhimu. Isitoshe mafundisho mliyonipa katika viwango vyote viwili; kiwango cha shahada yangu ya kwanza na hiki cha shahada ya uzamili ni mambo nisiyoweza kuyasahau. Asanteni. Profesa Wamitila Dkt. Zaja, Dkt. Kineene Wa Mutiso, Dkt. Mbuthia, Dkt. Swaleh, Dkt. Mweri, Dkt. Mbatia na mwalimu Mungania ninatoa shukrani zangu za dhati kwenu kwa kunielekeza vyema katika taaluma hii.

Shukrani nyingi za dhati ni kwa mamangu Philia Khanaka ambaye alinitia moyo na kutaka kujua maendeleo yangu katika shughuli hii ingawaje hakujua bayana inahusu nini. Asante mama kwa kunihimiza nilipohitaji kusikia 'sauti ya mama kwa mwana'. Mchango wa mjomba David na Christopher Chisia hauwezi kusisitizwa. Mlijitolea mhanga kuniongoza, kunilea na kufadhili masomo yangu katika kipindi ambacho yalielekea kukatizwa. Shukrani

jazila kwenu na kwa familia zenu kwa ufadhili wa hali na mali mlionipa kabla na baada ya nyanyangu kutupa mkono.

Ndugu Kemoli, Kariuki, na dada Zipporah , ninyi ni marafiki wa dhati. Asanteni sana kwa urafiki wenu. Mliniauni pakubwa nilipomhitaji katika dhiki na faraja zangu. Maulana amjalie mema. Ninaomba pia kuwashukuru wanafunzi wenzangu tulioabiri na kusafiria chombo hiki kwa kipindi husika. Mawazo, mijadala na uchambuzi wenu wa masuala ya isimu ni mambo yaliyonikuza na kuniboresha. Bila kuwapuuza wengine, ninawatambua bwana Mstwenje, Kenguru na dada Mjomba kwa ukarimu na kauli zao za dhati za kuhimiza.

Kwa wote mliochangia katika shughuli hii, kutowataja hakufuti kwa vyovyote wema na uhusika wenu katika ufanisi wangu. Kwenu ninasema asanteni na Mola awajalie mema.

## MUHTASARI

Kazi hii inahusu uchanganuzi wa Kauli katika sentensi elekezi ya Kiswahili sanifu kwa kutumia nadharia ya Ubanifu. Kazi yenyewe ilikuwa na malengo ya kueleza dhana ya uambishaji na kuonyesha viambishi vya kauli katika kitenzi cha Kiswahili sanifu. Aidha, kazi hii imelenga kuonyesha uhusiano uliopo kati ya yambwa na viambishi vya kauli katika sentensi elekezi ya Kiswahili sanifu.

Kazi hii imefaulu katika kuonyesha kuwa dhana za uambishaji na unyambuaji ni taratibu mbili tofauti za kisarufi, na kwamba viambishi vya kauli ni tokeo la uambishaji wala sio la unyambuaji. Utafuti huu umebainisha kwamba viambishi vya kauli sio tu viambishi tamati, bali pia huongozwa na kanuni mbalimbali ikiwemo kanuni ya wiano wa irabu. Utafiti huu umeonyesha pia kwamba, Usogezi kama mojawapo ya mihimili mikuu ya nadahria ya Ubanifu, huongozwa na kanuni mbalimbali za iktisadi kwa lengo la kufanikisha ukuaguzi wa sifa muhimu.

Kazi yenyewe imepangwa katika sura tano; kila sura ikishughulikia vipengele mahususi. Sura ya kwanza imetoa utangulizi wa jumla kuhusu dhana za kauli na sentensi elekezi. Aidha sura hii imefafanua tatizo la utafiti, madhumuni ya utafiti, nadharia tete zilizoongoza utafiti pamoja na kueleza sababu za kuchagua mada ya utafiti. Sura hii pia imebainisha upeo na mipaka ya utafiti kabla ya kufafanua msingi wa nadharia iliyotumiwa ya Ubanifu na kudurusu yaliyoandikwa kuhusu kauli na nadharia ya Ubanifu. Hatimaye, sura hii imeeleza mbinu za utafiti na umuhimu wa utafiti huu. Sura ya pili imeshughulikia dhana za uambishaji na unyambuaji na kutoa vigezo vitano vya kuzitofautisha. Aidha, sura hii imeangazia viambishi awali na tamati vya vitenzi vya Kiswahili sanifu kwa kina.

Katika sura ya tatu, vitenzi vya Kiswahili vimefafanuliwa kwa kuonyesha aina zake kwa misingi mitatu. Sura hii imehitimishwa kwa kuangazia kauli mbalimbali za vitenzi vya Kiswahili katika muktadha wa sentensi elekezi. Sura ya nne imejishughulisha na uchanganuzi wa data yetu ambapo kauli tisa za vitenzi zimeelezwa kwa kutumia nadharia ya ubanifu. Dhana za uhusika na valensi pia zimeshughulikiwa hapa. Sura hii imetathmini kwa kina nafasi ya kanuni mbalimbali za nadharia ya Ubanifu zinazohakikisha kuwa tungo zinazozalika zinakuwa sahihi sio tu kifonetiki, bali pia kimantiki. Sura ya tano ya tasnifu hii imetoa mahitimisho ya utafiti wetu. Zaidi ya mahitimisho, sura hii imetoa mapendekezo ambayo watafiti wengine wanaweza kuzingatia katika tafiti zao za baadaye.

# ORODHA YA VIFUPISHO

a ........................................athari

ak ........................................athari ya kiima

at ........................................athari ya kitenzi

At ........................................ athari ya kitenzi kikuu

aTs ........................................athari ya kitenzi kisaidizi

ayew ....................................athari ya yambwa tendewa

ayw ........................................ athari ya yambwa tendwa

et al ...................................................na wengine

HAL .....................................hali

(K)KAN ................................. kauli ya kutendana

(K)KEAN ...............................kauli ya kutendeana

(K)KEW ................................kauli ya kutendewa

KH ........................................kirai kihusishi

KN.... .....................................kikundi nomino

KT .........................................kikundi tenzi

(K)KSH ...................................(kirai) kauli ya kutendesha

(K)KSHAN ............................. (kirai) kauli ya kutendeshana

(K)KSHEA ..............................(kirai) kauli ya kutendeshea

(K)KSHEAN ...........................(kirai) kauli ya kutendesheana

(K)KSHW ............................. kauli ya kutendeshwa

KUK ......................................kanuni ya ufasiri wa kina

(K)UPK ................................. (kirai) upatanisho wa kiima

(K)UPYEW ........................................ (kirai) upatanisho wa yambwa tendewa

(K)UPYW ........................................ (kirai) upatanisho wa yambwa tendwa

KW ........................................ kauli ya kutendwa

NJ ........................................Njeo

n.k. ........................................ na kadhalika

T ........................................kitenzi kikuu

t ........................................ kitenzi kishirikishi

Ts ........................................kitenzi kisaidizi

UF ........................................umbo fonetiki

UKAN ........................................ukanusho

UM ........................................ umbo mantiki

U&M ........................................ umilikifu na masharti

UP ........................................upatanisho

## 1.0. SURA YA KWANZA

### 1.1. UTANGULIZI

Sura hii itakusudia kufafanua dhana mbili za kauli katika vitenzi na sentensi elekezi ya Kiswahili sanifu. Aidha tutalenga kutoa tatizo la utafiti, malengo ya utafiti, nadharia tete, sababu za kuchagua mada ya utafiti na kufafanua mipaka na upeo wa utafiti wetu. Aidha, tutafafanua msingi wa nadharia, kazi tulizozidurusu, mbinu za utafiti, na hatimaye tueleze umuhimu wa utafiti wetu.

#### 1.1.1 DHANA YA KAULI NA SENTENSI ELEKEZI

Lugha ya Kiswahili inaainishwa katika jamii ya lugha ambishibainishi. Hili lina maana kwamba mizizi yake huweza kuambishwa viambishi mbalimbali na ikawa ni rahisi kuonyesha mizizi hiyo na viambishi ni vipi (Guthrie 1948:12).

Miongoni mwa maneno yanayoambishwa ni vitenzi. Viambishi vya vitenzi huwa vimepangika katika mpangilio maalum ambao unaweza kusemwa ni muundo wa kimofolojia wa kitenzi cha Kiswahili. Viambishi hivi vya vitenzi ni pamoja na vya nafsi, ngeli, ukanushi, njeo, hali, urejeshi, yambwa, kauli, dhamira, rai n.k. Kuna aina mbili kuu za viambishi katika lugha ya Kiswahili sanifu: viambishi awali na viambishi tamati. Viambishi awali hutiwa katika mzizi upande wa kushoto ilhali viambishi tamati huambishwa kwenye mzizi, upande wa kulia (Polome 1967:110).

Kauli ni mojawapo katika ufafanuzi wa sentensi au kishazi, ambayo hasa huhusu kitenzi, na hutumiwa kuonyesha jinsi sentensi zinavyoweza kubadili uhusiano uliopo baina ya kiima na yambwa bila kubadilisha maana ya sentensi (Massamba 2004:26).

Wataalamu wengi wa Kiswahili wamestahabu kutumia kifungu 'kauli za mnyambuliko' kuelezea hali hii. Mathalani, Kihore, et al (2003:122) wanasema kwamba, 'unyambuaji wa vitenzi ni utaratibu wa uundaji vitenzi katika lugha kwa kuongeza viambishi nyambulishi kwenye maumbo ya mzizi.' Kwa mfano:

1) a. Mwalimu alimsomesha mwanafunzi.

   b. Moris aliwapigia Wakenya ngoma.

Viambishi vinavyohusika hapo juu vina maana zifuatazo:

Kiambishi kilichokolezwa -esh- katika mfano wa kwanza ni kiambishi cha kauli ya kutendesha. Hili lina maana kwamba, mwalimu alimsababisha mwanafunzi asome; mwalimu hakusoma. Kuna uwezekano kwamba mwalimu huyo alikuwa na nguvu fulani zilizomfanya mwanafunzi kusoma. Katika mfano wa pili, kiambishi -i- ni kiambishi cha kauli ya kutendea. Kiambishi hicho kinaifanya sentensi husika kuwa na maana zaidi ya moja. Kwanza, sentensi ina maana kwamba Moris alipiga ngoma kwa manufaa ya Wakenya. Wakenya walifaidika na upigaji ngoma wa Moris. Pili, sentensi hiyo ina maana kwamba Moris alipiga ngoma kwa niaba ya Wakenya. Wakenya walistahili kupiga ngoma lakini Moris akaipiga badala yao. Maana ya tatu ya sentensi husika ni kwamba Moris aliwapiga Wakenya kwa kutumia ngoma. Hapa ngoma ni ala au nyenzo iliyotumiwa kuwapiga Wakenya. Katika utafiti huu tutadhamiria kuonyesha namna kauli za vitenzi zinavyobadili sio tu miundo ya sentensi, bali pia maana za sentensi hizo.

Katika utafiti huu tutatumia maneno haya 'kauli za mnyambuliko' kwa maana ile ile ya kupanua maana za kitenzi kwa kutia viambishi mbalimbali vya kauli katika mzizi. Kila umbo linalonyambuliwa huwa na maana tofauti ila maana hiyo inafungamana na maana msingi iliyosetiriwa katika mzizi wa kitenzi. Hata hivyo, tunatambua kwamba katika taaluma ya isimu, neno unyambuaji linatumiwa kuelezea utaratibu wa kuunda au kuzalisha kategoria tofauti za kisarufi kutokana na maneno yaliyopo. Kwa mfano, kutokana na kitenzi 'imba', tunaweza kuunda nomino 'wimbo' na 'uimbaji' (Katamba 1993, Massamba 2004, Radford 1997).

Sentensi elekezi ni sentensi iliyo na kitenzi kilicho na uwezo wa kuchukua yambwa katika muundo wa tungo fulani. Yambwa ni nomino inayotaja mtu, mnyama au kitu kinachopata athari au manufaa ya tendo fulani. Kuna aina mbili za yambwa; yambwa tendwa na yambwa tendewa. Yambwa tendwa hudokezwa kwa nomino inayoonyesha mtu, mnyama au kitu kinachopata athari ya kitendo. Yambwa tendewa kwa upande mwingine hudokezwa kwa nomino inayoonyesha mtu, kitu au mnyama anayepokea manufaa au hasara ya tendo. Katika lugha ya Kiswahili sanifu, yambwa tendwa hutanguliwa na yambwa tendewa ambayo hutokea katika mazingira punde baada ya kitenzi katika sentensi elekezi. Hata hivyo, sentensi inaweza kuwa na yambwa moja tu; ama yambwa tendwa au yambwa tendewa. Mathalani:

2) a. Alimpiga Simani.

b. Wangui alimwandikia mamake barua.

Katika mfano wa kwanza, Simani ni yambwa tendwa ihali katika ule wa pili, mama ni yambwa tendewa. Hii ni kwa kuwa 'mama' anapokea manufaa ya uandishi, ilhali barua ni yambwa tendwa; inapatwa na athari ya uandishi moja kwa moja. Yambwa hizi mbili aidha huitwa shamirisho kipozi na shamirisho kitondo mtawalia.

## 1.2.TATIZO LA UTAFITI

Dhana ya 'mnyambuliko wa vitenzi' imekuwa na utata kwa muda mrefu huku baadhi ya wataalam wakisema kuwa mnyambuliko ni neno linalotumiwa kuelezea utaratibu wa kuunda maneno kutokana na maneno mengine. Kwa mfano, nomino zinaweza kunyambuliwa kutokana na vitenzi na vivumishi (Massamba 2004 na Katamba 1993). Kwa wengine, mnyambuliko wa vitenzi ni utaratibu wa kupanua vitenzi kwa kuvitia viambishi tamati vya kauli kiasi kwamba maana za vitenzi hivyo zinabadilika tu kutegemea dhamira (Kapinga 1983, Kihore et al 2003, Mbaabu 1985). Kwa sababu hii wataalam mbalimbali wanatoa fasiri tofautitofauti kuhusu dhana hizi mbili za uambishaji na unyambuaji. Baadhi ya wataalam wanazitumia istilahi hizi mbili kama visawe na kwa hivyo kuzua utata kuzihusu katika Kiswahili sanifu. Utafiti wetu utalenga kufanya ufafanuzi wa dhana hizi mbili na kwa kutolea mifano halisi ya Kiswahili. Kwa hivyo, utafiti huu utachangia kuondoa utata huo.

Suala la kauli za 'mnyambuliko' limeandikiwa na wataalam mbalimbali wa Kiswahili kama vile Mgullu (1999), Habwe na Karanja (2004), Kapinga (1983) miongoni mwa wengine. Hata hivyo kazi hizo zilizoandikiwa kuhusu suala hili zimezingatia vitenzi katika upekee wake bila kuvitathmini katika muktadha wa sentensi. Tunatambua kwamba baadhi ya vitenzi vya Kiswahili, na hasa vitenzi halisi hujisimamia kama sentensi kamili. Hata hivyo, tafiti hizo hazikueleza mahusiano ya kauli za 'mnyambuliko' na mofu za yambwa katika sentensi elekezi. Utafiti huu unatarajia kuziba pengo hilo katika lugha ya Kiswahili kwani utachanganua kauli katika muktadha wa sentensi elekezi za Kiswahili sanifu.

Utafiti huu ulikusudia kuchanganua kauli za vitenzi katika sentensi elekezi ya Kiswahili sanifu kwa kutumia nadharia ya Ubanifu. Nadharia hii ya Ubanifu imetajwa kama iliyo mwafaka zaidi kuchanganua lugha ambishibainishi, kama Kiswahili (Kaviti, 2004), tulikusudia kubainisha hilo. Aidha utafiti huu ulidhamiria kuonyesha iwapo kanuni ya Ukaguzi Sifa ya nadharia hii inaweza kufafanua kauli za vitenzi katika sentensi elekezi ya Kiswahili sanifu.

## 1.3.MADHUMUNI YA UTAFITI

Utafiti huu unakusudia kutimiza malengo yafuatayo:

1. Kueleza dhana ya uambishaji katika kitenzi cha Kiswahili sanifu.
2. Kueleza kauli na nafasi ya viambishi vya kauli katika kitenzi cha Kiswahii sanifu.
3. Kufafanua uhusiano uliopo kati ya mofu za yambwa na kauli katika sentensi elekezi ya Kiswahili sanifu.
4. Kuhakiki ufaafu wa nadharia ya Ubanifu katika kuchunguza kauli katika vitenzi vya Kiswahili sanifu.

## 1.4.NADHARIA TETE

Utafiti huu utafanywa katika misingi ya nadharia tete zifuatazo:

1. Dhana ya uambishaji na unyambuaji ni taratibu mbili tofauti zinazohusu maneno katika lugha.
2. Viambishi vya kauli ni viambishi tamati katika kitenzi leksika cha Kiswahili sanifu.
3. Kauli za vitenzi huhusiana pakubwa na kuelekezwa na viambishi vya yambwa vinavyopatikana kabla ya mzizi wa kitenzi cha Kiswahili sanifu.
4. Nadharia ya Ubanifu, na hasa kanuni yake ya ukaguzi Sifa ni mwafaka zaidi katika kufafanua kauli mbalimbali katika kitenzi cha Kiswahili sanifu.

## 1.5.UHALALISHAJI

Wataalam na watafiti mbalimbali wa lugha wamefanyia utafiti na kuandika kuhusu viambishi tofautitofauti vya vitenzi vya Kiswahili. Wengi wao wamevitaja kwa mpito tu viambishi vya kauli bila kuvishughulikia kwa kina. Kwa mfano, Kapinga (1983:135) amefafanua kauli tatu za vitenzi; kauli ya kutenda, kutendwa na kutendeka. Utafiti huu ulikusudia kubainisha na kufafanua kauli zaidi ya kumi za vitenzi, na pia katika muktadha wa sentensi elekezi. Kwa kufanya hivi tulikusudia kuonyesha muswala ya kimofosintaksia yanayoathiri maumbo ya

vitenzi vinapofuatiwa na yambwa katika sentensi na vishazi. Hata hivyo, tulionyesha utendakazi wa usogezi na ukaguzi sifa katika kauli tisa za vitenzi.

Katika utafiti wake wa hali na njeo, Karimi (2008:112) anapendekeza haja ya kufanya utafiti kuhusu viambishi vya kiima, ukanusho, urejeshi, kauli na yambwa. Utafiti huu ulikusudia kushughulikia sehemu ya pendekezo hilo kwa kutafiti kuhusu viambishi vya kauli.

Watafiti wengine kama vile Kihore et al (2003), na Mbaabu (1985) wameshughulikia sarufi maumbo ya Kiswahili. Hawa wameangazia aina zote za maneno katika lugha ya Kiswahili. Kwa sababu hii, hawakuweza kuangazia viambishi vya kauli kwa uketo. Aidha kazi zao zinaelekea kulenga hadhira isiyo na ujuzi mkubwa wa kiisimu kwani hazielekei kutumia msingi maalum wa kinadharia. Utafiti huu ulikusudia kuziba pengo hili na kufafanua kauli za vitenzi sio tu katika muktadha wa sentensi elekezi, bali pia kwa kutumia nadharia ya Ubanifu.

Tulitumai kwamba utafiti huu ungechangia kukuza na kuboresha hazina ya tafiti za awali katika shughuli nzima ya kutoa uelewa wa kina wa kiisimu wa lugha ya Kiswahili; kwa kuwa tunaamini kuwa utafiti na uchunguzi wa lugha huchangia uelewa wake na kupanuka kwa matumizi ya lugha hiyo.

## 1.6.UPEO NA MIPAKA

Lugha ya Kiswahili ina lahaja nyingi; takribani kumi na nane (Bakari 1982). Hatungeweza kushughulikia utafiti wa kauli katika hizo lahaja zote. Sisi tulishughulikia viambishi vya kauli katika Kiswahili sanifu. Uamuzi huu ulitokana na hali kwamba lugha hii ndiyo inayotumiwa na watu wengi katika mazungumzo na maandishi. Aidha Kiswahili sanifu ni lugha ya taifa nchini Kenya na Tanzania na lugha rasmi nchini Kenya. Fauka ya hayo, Kiswahili kinafundishwa katika shule za msingi na za upili kama somo la lazima katika nchi hizo mbili. Aidha Kiswahili sanifu pamoja na fasihi ya Kiswahili hufundishwa katika vyuo vya walimu na pia katika vyuo vikuu vingi ulimwenguni.

Viambishi vya kauli ni aina moja tu ya viambishi vingi vya kitenzi cha Kiswahili. Viambishi vingine vya Kiswahili ni pamoja na vile vya nafsi, ngeli, ukanushi, njeo, hali, urejeshi, mahali, kiishio miongoni mwa vingine. Utafiti huu ulivifafanua viambishi hivyo ila kwa juujuu tu. Tulifanya hilo katika juhudi za kuvipambanua viambishi vya kauli na kuonyesha

uhusiano wake na viambishi vinginevyo vya vitenzi vya Kiswahili sanifu. Tulidhamiria kuonyesha kauli katika vitenzi vya asili ya Kibantu na vile vya mkopo.

Utafiti huu ulifanywa katika misingi ya nadharia ya Ubanifu aliyoiasisi mwanaisimu Noam Chomsky mwaka wa 1993. Tulitathmini pia nguzo muhimu za nadharia hii ambazo ni Kanuni za iktisadi. Tulifafanua namna ambavyo kanuni hizi hushirikiana kuunda tungo iliyo sahihi.

Kwa kuzingatia muundo, sentensi za lugha zinaweza kuainishwa katika makundi manne makuu; sentensi sahili, sentensi ambatano, sentensi changamano na sentensi ambatano changamano. Utafiti wetu ulijikita katika sentensi sahili ya Kiswahili sanifu tu. Uamuzi huu ulitokana na ubanifu wa kipindi cha utafiti huu kisichotukubalia kushughulikia aina nyinginezo za sentensi. Pale tulipogusia zile aina nyingine za sentensi ilikuwa ni kwa haja ya lazima ya kupambanua masuala fulani katika mipaka ya sentensi sahili.

Fauka ya hayo, utafiti wetu wa kauli ulifanywa katika muktadha wa sentensi elekezi ya Kiswahili sanifu. Sentensi tulizozingatia ni zile zenye vitenzi vinavyochukua yambwa moja na au mbili. Tunaelewa kuwa vitenzi elekezi vinaweza kuchukua yambwa moja au mbili. Sisi tulishughulikia aina hizi mbili bila ubaguzi lakini tulibainisha taratibu mbili kuu zinazohusisha kuongezeka na kupungua kwa valensi katika sentensi.

## 1.7.MSINGI WA NADHARIA

### 1.7.1. UTANGULIZI

Wanaisimu mbalimbali wamekuwa katika juhudi za kutafuta nadharia mwafaka ya kufafanua lugha asilia. Juhudi hizi zilifikia upeo miaka ya 1950, Nadharia ya Sarufi Zalishi ilipoasisiwa. Mwaka wa 1957, mwanaisimu Noam Chomsky alijitokeza na Kitabu, *Syntactic Structures.* Chomsky alileta mapinduzi makubwa mno katika taaluma ya isimu na suala la uchunguzi na uchanganuzi wa lugha asilia. Katika kitabu hiki, Chomsky alizua dhana mbili kuu: Umilisi na Utendaji.

Kulingana na Chomsky, umilisi ni ujuzi wa lugha anaoubwia msemaji mzawa wa lugha fulani. Ujuzi huu unamwezesha mzawa wa lugha fulani kuunda tungo sahihi, kufasiri tungo mbalimbali na kutofautisha tungo zilizo sahihi na zile zenye dosari katika lugha yake. Umilisi pia humwezesha msemaji mzawa wa lugha fulani kutunga sentensi nyingi na zisizo na ukomo; zikiwemo zile ambazo hajawahi kuzisikia katika aushi yake. Umilisi, kwa hivyo, ni

wa kijamii-lugha. Utendaji ni uhalisi kamili wa kutumia lugha kwa kusema na kufasiri kinachosemwa. Utendaji ni uhalisi wa mzawa lugha wa kutekeleza ujuzi (umilisi) kwa kuwasiliana katika jamii yake. Utendaji ni suala la kibinafsi na huweza kuathiriwa na mambo mbalimbali kama vile uchovu, ulevi, woga, furaha na kadhalika. Kulingana na Chomsky, utendaji sio kigezo mwafaka cha kukadiria umilisi wa mtu binafsi. Kwa sababu hii, mwanaisimu huyu alipendekeza kwamba uchunguzi wowote wa lugha unastahili kushughulikia umilisi kwa kuwa huwa haujaathiriwa na mambo kama tuliyoyataja hapo juu.

Mwaka wa 1965 nadharia hii ilifanyiwa marekebisho na Chomsky na akajitokeza na nadharia ya Sarufi Zalishi Geuza Maumbo. Mawazo haya mapya yalijumuishwa katika kitabu chake, *Aspects of the Theory of Syntax*. Mawazo haya yalichochewa na haja ya kuchunguza suala la umbo ndani na umbo nje katika lugha. Chomsky katika nadharia hii alipendekeza viwango vitatu vya uchunguzi vya sintaksia ya lugha;

a) Kitengo Msingi; hujumuisha miundo virai, uandikaji upya na msamiati. Kitengo hiki ndicho kizalishacho maumbo ndani.

b) Kitengo cha Ugeuza maumbo; hushughulika na kufanyia ugeuzaji maumbo yatokanayo na Kitengo Msimgi.

c) Kitengo Fonolojia; huwezesha uwasilishaji wa kifonetiki na ule wa kisemantiki.

Baadaye, 1970, nadharia hii ilifanyiwa mabadiliko na kuwa nadharia ya Wastani. Katika mwongo huo wa 1970 nadharia Wastani ilifanyiwa marekebisho na kuwa Nadharia ya Wastani Panuzi. Nadharia hizi zote zilijihusisha na Kanuni Miundo Virai.

Mwaka wa 1980, Chomsky aliaasisi nadharia ya Umilikifu na Masharti. Sifa kuu ya nadharia hii ni kuwepo kwa mifumo mingi ya kanuni ambazo ni bia na pia zenye vikwazo/ mipaka katika lugha mahususi. Nadharia ya Umilikifu na Masharti ina vijinadharia kama vile:

- Nadharia ya Eksba
- Nadharia ya Uhusika (Case Theory)
- Nadharia ya Umilikifu (Bounding Theory)
- Nadharia ya Unakili (Trace Theory)
- Nadharia Funge (Binding Theory)

- Nadharia ya Utawala (Government theory)
- Nadharia ya Thita (Theta Theory).

Ni kutokana kanuni nyingi zitumikazo katika nadharia hii ambapo ilikuja kujulikana kama Nadharia ya Masharti na Mipaka.

Nadharia ya Ubanifu ni mradi wa hivi karibuni kuzinduliwa na Noam Chomsky (1993) na 1995) katika juhudi za kuchunguza lugha asilia. Nadharia hii sio mkengeuko wa nadharia iliyoitangulia ya Umilikifu na Masharti, bali ni mwendelezo ulioboreshwa; nadharia hii ilibuniwa kufidia upungufu wa nadharia za awali. Kwa mujibu wa Cook na Newson (1996:312)

> 'Nadharia ya Ubanifu inaendeleza malengo ya nadharia ya Mipaka na Masharti kwa kutumia mkabala banifu. Masuala mapya katika nadharia hii hayakujitenga pakubwa na yale ya Mipaka na Masharti' (TY).

Nadharia ya Ubanifu inatilia maanani hali kwamba uchanganuzi mahususi wa sintaksia ya lugha yoyote ile unastahili kuzingatia sio tu sheria zinazotawala uundaji wa virai na sentensi, bali pia kanuni zinazotawala ufasiri wa kategoria za kileksika (Kaviti 2005).

Nadharia ya Ubanifu inasahilishwa ili kuoana na uwezo wa kiasilia alionao mtoto ambao humwezesha kutumia lugha kwa usahili. Usahili huu unatokana na uchache pamoja na usahili wa kanuni hizo. Hali hii inatokana na uhalisi wa nadharia za awali, hasa nadharia ya Umilikifu na Masharti ambayo ilihusu miundo na kanuni nyingi na changamano, hali iliyokwaza taratibu za watoto kujifundisha lugha (Radford, 1997:6). Katika kuibua nadharia hii ya Ubanifu, Chomsky alichochewa na maswali mawili makuu:

1. Je, uelewa wa lugha ya mtu binafsi (idiolect/ I-Language) huwasilishwa vipi akilini?
2. Je, watoto hupata vipi uelewa huu?


## 1.7.2. DHANA MUHIMU KATIKA NADHARIA YA UBANIFU

### 1.7.2.1.MIFANYIKO YA KIMKOKOTOO


Nadharia ya Ubanifu ina uchukulizi kuwa lugha ina vitengo viwili vikuu, yaani, Leksikoni mahususi, na Kitengo cha Mifanyiko ya Kimkokotoo (Chomsky 1995:168).

Msamiati (leksikoni) huhifadhi leksika na habari zote za kimofosintaksia kuhusu nomino na vitenzi. Kundi la vipashio vya kileksika na kimofosintaksia huchaguliwa kutoka kwa leksikoni katika utaratibu uitwao niumerali katika mfanyiko wa kimkokotoo. Uchaguzi huu huongozwa na Kanuni ya Fasiri ya Kina ambayo ni hitaji la iktisadi ambapo ni vipashio muhimu na mwafaka zaidi katika uundaji wa virai na sentensi vinavyochaguliwa tu. Katika nadharia hii vipashio vyote vinavyochaguliwa katika leksikoni ni sharti vitumike katika uundaji. Hii ni kwa sababu nafasi tupu pamoja na miundo isiyo sahihi hunyimwa nafasi ya kudhihirika. Mifanyiko ya kimkokotoo huwa na mchakato mwingine ujulikanao kama 'muungano'. Muungano ni mchakato unaosafirisha habari kuhusu sifa za vitenzi na nomino kutoka katika leksikoni hadi katika hatua ya Mjumuiko (Interface). Hatua hii ndiyo iliyojulikana kama hatua ya umbo nje katika nadharia ya Umilikifu na Masharti (Chomsky 1993:3).Nadharia hii inatambua viwango viwili vya uwakilishaji; umbo Fonetiki na Umbo Mantiki, tofauti na nadharia ya Umilikifu na Masharti mbayo ilihusisha viwango vinne: umbo ndani, umbo nje, Umbo Fonetiki na Umbo Mantiki (Munyao 2006).


Nadharia ya Ubanifu imesalisha kipengele cha uhusiano wa spesifaya-kichwa na kichwa-kichwa cha nadharia ya awali ya X-ba. Vipashio vya kileksika kutoka katika leksikoni hugeuzwa katika uhusiano wa spesifaya-kichwa au ule wa kichwa-kijalizo (Schroeder 2002). Kielelezo kifuatacho kinafafanua hili;




Kwa mujibu wa Radford (1997:174), michakato ya uundaji tungo hufanyika kutegemea kuwepo kwa haja. Tungo ziundwazo katika mfanyiko wa kimkokotoo ni sharti ziidhinishwe na habari za kimofosintaksia au za kileksika katika leksikoni. Endapo hapana haja ya kupima uhusika, kielelezo cha kichwa bila kijalizo huwa hivi:




Tunafafanua hili kwa kutumia mfano katika kielelezo kifuatacho ambacho kinadhihirisha kuwepo kwa kichwa bila spesifaya hasa endapo upimaji wa uhusika haukusudiwi:




Wanacheza

1.7.2.2.KANUNI YA UKAGUZI SIFA

Kanuni ya Ukaguzi Sifa ni utaratibu katika Ubanifu ambao hukusudia kuhakikisha kuwa vipengele vyote vya kileksika vina sifa zihitajikazo kabla ya kutumiwa katika nafasi yoyote katika muundo wa sentensi. Kulingana na Kaviti (2004:66),

> Jukumu kuu la ukaguzi sifa ni kutathmini maneno yaliyozalishwa katika leksikoni na kulinganisha viambishi vyake na masharti ya lugha husika kuhusu nafasi za viambishi hivyo katika maneno hayo (TY).

Ukaguzi sifa hufanikishwa na kuwepo kwa usogezi; usogezi ambao ni utaratibu ambapo sifa dhahania za uambishaji hukaguliwa ili kukadiria usahihi wake mintaarafu nafasi zake katika tungo (Haegeman 1994:591). Sifa hizo dhahania za uambishaji ni kama vile njeo na upatanisho.

Katika nadharia hii ya Ubanifu, njeo na upatanisho huwa na majukumu mawili. Kwa mujibu wa nadharia tete ya Kuvunjika Virai, uambishaji hugawanywa katika njeo, upatanisho kiima na upatanisho yambwa. Kategoria hizi amilifu za njeo na upatanisho huwa hazitawali mofolojia ambishi bali huthaminiwa kama vitita vya sifa dhahania. Usogezi katika upatanisho kiima, njeo na upatanisho yambwa ni taratibu za ukaguzi sifa zinazokusudia kuondoa sifa dhahania ili zisidhihirike katika hatua ya Umbo Fonetiki. Mivurumisho (projections) ya njeo

na upatanisho huhakikisha kwamba sifa za vikundi tenzi zimekaguliwa ilhali sifa za uhusika hukagua vikundi nomino. Katika mchakato huo, ukaguzi sifa huhakikisha kwamba kundi tenzi linakubaliana na kundi nomino ili kuunda sentensi sahihi. Ukaguzi huu huweza kutokea katika awamu yoyote ya uundaji tungo kabla ya hatua za umbo fonetiki na umbo mantiki (Schroeder 2002).

Mofolojia ya nomino hukaguliwa sifa za uhusika katika nafasi ya spesifaya inayofaa kama upatanisho kiima na upatanisho yambwa. Mofolojia ya vitenzi kwa upande mwingine hutoa sifa zipimwazo katika kitenzi kama vile hali, njeo, upatanisho, kauli na kadhalika. Sifa hizi za kitenzi hukaguliwa katika nafasi ya kichwa-kichwa ili kuhakikisha usahihi wa kimuundo wa virai.

Kwa mujibu wa nadharia Tete ya Kuvunjika Virai (Split Inflectional Hypothesis) kila kiambishi katika kitenzi huwa kirai ambacho hujisimamia. Kwa hivyo, viambishi vyote katika vitenzi ni virai vyenye vichwa mbalimbali (Jerono, 2003). Kwa misingi hii, viambishi kama vile vya njeo, upatanisho, hali na kauli ni virai kamili.

Nadharia hii ya Ubanifu huziainisha lugha asilia katika makundi mawili makuu kutegemea kigezo cha upatanisho. Kuna lugha za upatanisho imara na zile za upatanisho dhaifu. Lugha za upatanisho imara hudhihirika katika UF ilhali zile za upatanisho dhaifu hazidhihiriki. Lugha za upatanisho imara kama Kiswahili hulazimisha vitenzi kusogezwa ili kukagua kitita cha sifa dhahania. Sifa hizo huondolewa kabla ya utaratibu wa mdhihiriko wazi haujafikia UF. Maadamu lugha za upatanisho dhaifu hazina sifa ya kukaguliwa, usogezi hufanywa kidhahania.Usogezi hutawaliwa na ushirikiano wa Kanuni za iktisadi; mmojawapo wa mihimili mikuu ya nadharia ya Ubanifu. Kanuni hii inadokeza kuwa 'ni vipashio vichache tu ambavyo huweza kusogezwa ili kutimiza mahitaji ya kisarufi katika tungo fulani' (Radford 1997:230). Kanuni hizo ni pamoja na;

a) Kanuni ya Usogezi mfupi zaidi (Principle of Relativized Minimality)

Kanuni hii inapendekeza kuwa viambajengo huweza kusogezwa katika mahali karibu mno panapotokea ulazima wa kisarufi.

b) Kanuni ya kuchelewesha (Principle of Procrastinate)

Kanuni hii huwezesha usogezi endapo ni wa lazima, na sharti usogezi huo uongozwe na sheria za kimofosintaksia au za kileksika katika lugha husika.

c) Kanuni ya Ubinafsi (Principle of Greed)

Kanuni hii huongoza kwamba usogezi wa viambajengo hutokea kwa haja ya kutimiza mahitaji ya viambajengo hivyo na wala sio viambajengo vingine; sharti manufaa yawe ya kipashio husika (Murantz 1995, anavyonukuliwa na Swaleh 2005:12).

d) Kanuni ya Usogezi wa lazima ( Last Resort Principle)

Kanuni hii ina maana kwamba usogezi hufanywa tu kama hiyo ndiyo njia ya pekee na mwafaka katika kuhakikisha usahihi wa tungo.

Baada ya miundo mbalimbali kujengwa, mfanyiko wa kimkokotoo hudhihirisha wazi habari za leksikoni katika Umbo Fonetiki (UF) na Umbo Mantiki (UM) katika mfanyiko ujulikanao kama Mdhihiriko Wazi na hatimaye kuishia katika hatua iitwayo Mjumuisho. Mdhihiriko wazi ni hatua muhimu kwa kuwa inawezesha kutenga habari za kifonolojia na zile za kisemantiki katika tungo zinazoundwa. Utengaji huu wa habari za UF na zile za UM hukusudia kuhakikisha kuwa habari za UF hazidhihiriki katika hatua ya uwasilishaji wa UM, na vilevile kwamba habari zinasohusiana na maana za tungo hazidhihiriki katika hatua ya uwasilishaji wa UF. Kipengele hiki ndicho tulichokibainisha hapo juu kama Kanuni ya Ufasiri wa kina. Kanuni hii huhitaji kwamba seti yote ya vipashio vinavyoshirikishwa katika mfanyiko wa kimkokotoo kutoka kwa leksikoni ni sharti zitumike. Sharti hilo linapotimizwa mchakato mzima hutajwa kama 'uliojumuika'. Kwa upande mwingine, sharti hilo likikosa kutimizwa na hivyo basi habari za UF zikachanganywa na zile za UM, basi husemekana kuwa kuna 'mpomoko'. Hili lina maana kwamba tungo zitakazozalika katika mfanyiko mzima wa kimkokotoo huwa si sahihi kisarufi (Radford 1997:171).

Nadharia ya Ubanifu ina chukulizi kwamba kategoria za maneno huwa na sifa tatu kuu:

a) Sifa za kichwa au neno kuu ambazo hufafanua sifa zote za kisarufi za neno hilo.

b) Sifa za kijalizo ambazo huamua vijalizo vinavyoweza kuchukuliwa na neno kuu.

c) Sifa za spesifaya ambazo huamua spesifaya inayoweza kuchukuliwa na neno kuu.


Chukulizi hizi ni muhimu kwa sababu husaidia kusuluhisha tatizo la jinsi ya kuondoa sifa zinazoweza kufafanuliwa katika wakilisho la UM pamoja na mipaka ya kisarufi inayowekewa vichwa katika uchaguzi wao wa spesifaya na vijalizo. Sifa zisizoweza

kufafanuliwa hubidi zikaguliwe katika umbo lifaalo la ukaguzi na hatimaye kuondolewa mbali. Hali hii inafafanuliwa na Bobaljik (1995) kama anavyonukuliwa na Kaviti (2004),

> 'Kichwa hukagua sifa za spesifaya na kijalizo chake. Sifa za spesifaya na kijalizo huchukuliwa kuwa haziwezi kufafanuliwa.'

Kielelezo kifuatacho kinafafanua utaratibu unaoishia katika vitengo viwili vya UF na UM;

Asili: Schroeder (2005). *Hand-out on Minimalist Program* presented in a seminar at the University of Nairobi.



## 1.7.2.3.NAFASI YA MOFOLOJIA KATIKA NADHARIA YA UBANIFU

Mapema katika karne ya ishirini, kabla ya 1950, taaluma ya Mofolojia ilipuuzwa kama mojawapo wa viwango vikuu vya uchunguzi wa lugha. Baadhi ya Wanasarufi walidai kwamba taaluma ya uundaji maneno ingeshughulikiwa chini ya taaluma za sintaksia na fonolojia. Hata hivyo, kufikia mapema miaka ya 1970, wanaisimu kama vile Mathews (1972 na 1974) na (Robins 1959) walijadili sana umuhimu wa mofolojia katika taaluma ya uchunguzi wa lugha (Katamba 1993:10).

Kwa mujibu wa Ouhalla (1991:48) '... kiunzi cha mofolojia ni daraja ya $X^0$ ilhali ile ya sintaksia ni awamu $X^{'}$ na $X^{'}$ ya uwakilishaji wa viambajengo.' (TY)


Fasili hii ina maana kwamba kiunzi cha mofolojia kinapojishughulisha na taratibu za uundaji maneno, sintaksia kwa upande wa pili hujishughulisha na uundaji virai na sentensi. Katika uchanganuzi wa lugha ambishibainishi kama Kiswahili, kwa hivyo, ni sharti taaluma hizi mbili za isimu zizingatiwe kwa pamoja.

Mifanyiko yote ya kimkokotoo katika nadharia hii ya Ubanifu huongozwa na mahitaji ya kimofolojia. Aidha usogezi ufanywao ili kutimiza masharti ya ukaguzi sifa hutegemea mofolojia ya lugha husika (Chomsky 1993:32).

Kama tulivyodokeza hapo juu, lugha huainishwa kama zilizo na upatanisho thabiti au zilizo na upatanisho dhaifu. Upatanisho thabiti hudhihirika katika UF ili usogezi wa vitenzi uweze kuondoa kitita cha sifa dhahania kabla ya mchakato wa mdhihiriko wazi haujafikia UF.

Katika nadharia hii ya kimofosintaksia, sifa za uambishaji na unyambuaji hupewa vitenzi na nomino katika leksikoni. Ni katika leksikoni ambapo utaratibu mzima wa uundaji tungo huanzia. Vipashio vya kileksika vilivyoambishwa huzalishwa kimsingi katika kundi tenzi chini ya vichwa vyao mwafaka. Hatimaye usogezi wa vitenzi hufanywa ili ukaguzi sifa utekelezwe.

Katika nadharia hii Kanuni ya Ukaguzi Sifa huelekeza kwamba kitenzi kinasogezwa katika vifindo vya uzalishaji tungo na virai nomino husogezwa kwenye spesifaya za Kirai cha upatanisho kiima (KUPK) na Kirai upatanisho yambwa (KUPY) kwa ukaguzi wa sifa za kiima na zile za yambwa zinazoonekana na kujisimamia. Mathalani;




Katika kielelezo hiki usogezi na ukaguzi sifa za nomino na kitenzi unafanyika kama ifuatavyo ; yambwa tendwa picha inasogezwa kutoka kwa KN la T' hadi kwa spesifaya ya KUPY ili uhusika wake wa yambwa tendwa ukaguliwe. Kiima 'mtoto' ambacho kinawakilisha mtenda katika nadharia ya Uhusika ya Charles Filmore (1968) kinasogezwa kutoka kwa spesifaya ya KT hadi katika ile ya KUPK ili sifa yake ya upatanisho kiima utekelezwe.Kwa upande mwingine, kitenzi kinasogezwa kutoka kwa UPY ya UPY' hadi kwa

NJ ya NJ' kwa ukaguzi wa sifa ya njeo. Kisha kinasogezwa kwa UPK ya UPK' kwa ukaguzi wa sifa ya upatanisho wa ngeli. Usogezi huu unakusudia kuhakikisha kwamba tungo zalika ni sahihi kwa mujibu wa Kanuni ya Ufasiri wa Kina.

Ufuatao ni muhtsari wa tofauti kati ya nadharia ya U & M na nadharia ya Ubanifu na unaelekea kuonyesha kuwa tofauti kati ya nadharia hii na zile tangulizi si kubwa mno, na kwa hivyo kushinikiza mawazo ya baadhi ya wataalam kwamba nadharia ya ubanifu sio mkengeuko wa nadharia za awali bali imeboreshwa kutoka kwazo (Kaviti 2004).

TOFAUTI KATI YA NADHARIA YA UMILIKIFU NA MASHARTI NA NADHARIA YA UBANIFU

| **Nadharia ya Umilikifu na Masharti** | **Nadharia ya Ubanifu** |
|---|---|
| Umuhimu kuwekwa kwa sintaksia | Umuhimu kuwekwa kwa Leksikoni |
| Huhusisha mwingiliano changamno wa sheria na vijinadharia vingi | Sheria zimebanwa na zimesahilishwa kwa Kujumlisha. |
| Viwango vinne vya uwalilishaji: umbo ndani Umbo nje, UF na UM. | Viwango viwili vya uwasilishaji: UF na UM. |
| Muundo wa nje. | Kitengo kimoja cha mjumuisho. |
| Kuwepo kwa nadharia ya Eksiba | Uhusiano wa Spesifaya-kichwa na kichwa-kichwa. |
| Kanuni ya sogeza thita | Muungano na usogezi. |
| Usogezi kuhusu umbo ndani hadi umbo nje. | Usogezi hukusudia kukagua sifa. |
| Nadharia ya Uhusika. | Nadharia ya Ukaguzi. |

## 1.8.KUDURUSU YALIYOANDIKWA KUHUSU MADA

### 1.8.1. UTANGULIZI

Katika sehemu hii tutashughulikia yaliyoandikwa kuhusiana na mada yetu ya utafiti. Sehemu hii imegawanywa katika awamu mbili kuu. Awamu ya kwanza itaangazia kazi ambazo zinahusiana na kauli za mnyambuliko katika sentensi elekezi ya Kiswahili Sanifu. Katika awamu ya pili tutashughulikia kazi zilizoandikwa kuhusu nadharia za sarufi, na hasa nadharia ya Ubanifu.

### 1.8.2. YALIYOANDIKWA KUHUSIANA NA KAULI

Mbaabu (1985) ameshughulikia aina mbalimbali za maneno katika lugha ya Kiswahili. Miongoni mwa maneno hayo ni vitenzi. Kazi hiyo ilitufaa sana hasa kipengele cha mnyambuliko wa vitenzi. Hii ni miongoni mwa kazi za mwanzo kabisa kushughulikia vitenzi katika lugha ya Kiswahili kuchapishwa.

Kazi ya Kapinga (1983) ilikuwa muhimu katika utafiti huu.Kazi hii inatoa ufafanuzi muhimu kuhusu aina za maneno katika Kiswahili sanifu. Kapinga ameshughulikia viambishi mbalimbali katika kitenzi cha Kiswahili. Miongoni mwa viambishi hivyo ni vile vya kauli. Japo maelezo yake kuhusu kauli yana upungufu, na hali kwamba anabainisha kauli tatu tu: kutenda, kutendwa na kutendeka, kama kauli za pekee katika Kiswahili sanifu, kazi hiyo ilituelekeza katika kuchanganua kauli katika sentensi elekezi ya Kiswahili sanifu.

Kihore et al (2003) wameshughulikia masuala mbalimbali katika Kiswahili. Katika kurasa kati ya 114 na 136, wataalam hawa wamechanganua vitenzi. Sehemu hiyo ilikuwa muhimu katika utafiti wetu, hasa kipengele cha mnyambuliko wa vitenzi. Aidha wataalam hawa wameshughulikia 'kanuni elekezi'. Kipengele hicho kilitufaa katika kuelewa dhana ya sentensi elekezi. Ingawa kazi yenyewe inalenga hadhira isiyo na ujuzi wa kiisimu ilitufaidi pakubwa kuelewa aina mbalimbali za kauli za mnyambuliko katika vitenzi vya Kiswahili.

Mgullu (1990) amechanganua sentensi za aina tatu kimuundo; Sentensi sahili, sentensi ambatano na sentensi changamano. Katika kueleza miundo yake, mtaalam huyo ameangazia aina tofautitofauti za virai. Maelezo hayo yatatusaidia kuelewa kundi tenzi la Kiswahili na vipashio vinavyolifuatia, hasa yambwa; kipashio ambacho tulikishughulikia katika utafiti huu. Nadharia anayotumia ya Sarufi Geuza Maumbo Zalishi ilitusaidia kuelewa misingi ya nadharia fuatilizi na sababu za kuchipuka kwa nadharia hizo ikiwemo nadharia ya Ubanifu.

Mgullu (1999) ni muhimu katika utafiti wetu hasa katika kurasa 182-212 ambapo mofolojia ya vitenzi vya Kiswahili imechanganuliwa. Japo kwa muhtasari, kazi hii pia imefafanua dhana ya 'unyambuaji' wa vitenzi na kufafanua aina kadhaa za kauli katika Kiswahili sanifu. Kwa hivyo, kazi hiyo ilitupa msingi mzuri kuhusu viambishi vya kauli, na hasa katika vitenzi ambavyo vina mizizi ya silabi moja.

Jerono (2003) amebainisha kwamba Kishazi huru arifu cha Kiswahili hutawaliwa na kitenzi. Aidha kazi hiyo imeonyesha muundo wa kishazi huru arifu, hali inayohusiana pakubwa na sentensi elekezi ya Kiswahili. Umuhimu wa kazi hii ulikuwa katika hali kwamba kazi yetu inahusu kauli za vitenzi ambazo kimsingi zinahusisha viambishi katika kitenzi. Aidha, kazi hii ilitufaa mno katika kuelewa nadharia tete ya Kuvunjika Virai ambayo inaeleza kuwa kategoria amilifu katika Umilikifu na Masharti hujisimamia kama virai, kila kimoja kikiwa na mvurumisho wake.

Munyao (2006) ametafiti kuhusu kauli za 'mnyambuliko' katika lugha ya Kikamba. Umuhimu wa utafiti huu haumo tu katika uhalisi kwamba Kikamba ni lugha ya Kibantu kama Kiswahili, bali pia ametumia nadharia ambayo tutaitumia katika utafiti wetu. Kwa hivyo, kazi hii ilikuwa tunu katika kurahisisha uelewa wetu wa nadharia hii ya Ubanifu na utendakazi wake katika Kiswahili, lugha ambishi bainishi kama kilivyo Kikamba.

Loogman (1995) ameangazia kategoria mbalimbali za maneno katika lugha ya Kiswahili. Maelezo yake kuhusu vitenzi na nomino ni yenye manufaa kwetu kwa kuwa kategoria hizi ndizo tulizozitumia katika utafiti wetu. Aidha ameangazia sentensi za Kiswahili. Kazi hiyo ilikuwa muhimu kwa utafiti wetu hasa kipengele cha mahusiano na maingiliano ya maneno katika sentensi ya Kiswahili sentensi.

Kamau (2002) ameshughulikia Sintaksia ya Virai vya Kiswahili sanifu na Kikuyu cha Kabete kiulinganishi. Kazi hii ilitusaidia kwani virai ni viambajengo vya sentensi ambayo tulilishughulikia katika utafiti wetu. Utafiti wetu ulinufaika zaidi hasa na kipengele cha Kirai nomino hasa katika mkabala wa yambwa katika sentensi elekezi.

Iribehmwangi (2008) ilikuwa mhimili mkuu katika utafiti huu. Msomi huyu ametafiti na kuandikia kwa kina mofofonolojia katika Kiswahili sanifu kwa kutumia nadharia ya Fonolojia Zalishi Asilia (NGP). Msomi huyu amefafanua vitenzi, aina zake na viambishi vya vitenzi japo kwa mpito. Tulinufaika na hili kwani utafiti wetu ulieleza viambishi vya kauli kwa kina zaidi. Katika sura ya tatu na ya nne ameangazia pakubwa mifanyiko inayohusu

konsonanti na irabu mtawalia. Sura hiyo ya nne ilitufaa sana kwani inahusisha mifanyiko ya irabu, ukiwemo mfanyiko uitwao tangamano la irabu. Mfanyiko huo ulitusaidia kuelewa suala la uwezekano wa kubashiri aina za viambishi vya kauli kwa kuzingatia irabu zinazopatikana katika mizizi ya vitenzi.

Katamba (1993) amefanya uchanganuzi wa kina kuhusu miundo ya maneno katika lugha. Aidha amejadili kwa kina mahusiano ya mofolojia na taaluma nyingine za isimu. Utafiti wetu ulifaidika pakubwa kutokana na ufafanuzi wake wa 'mofimu za unyambuaji na uambishaji.' Maadamu utafiti wetu ulihusu vitenzi, tulipata uelewa mwafaka wa aina mbalimbali za viambishi vya vitenzi; vikiwemo viambishi vya kauli za vitenzi. Zaidi ya hayo, kazi hii ilitusaidia katika kueleza kwa kina dhana za unyambuaji naa uambishaji katika Kiswahili sanifu.

Swaleh (2005) amefafanua kishazi kama tungo yenye kiima na kiarifu iliyomo katika tungo kuu. Utafiti huo ulikuwa na manufaa kwa huu wetu kwa kuwa ulitusaidia kuelewa aina mbalimbali za vishazi; vipengele vya kimsingi katika sentensi maadamu utafiti wetu unlishughulikia sentensi elekezi ya Kiswahili sanifu. Fauka ya hayo, Kitikuu ni lahaja mojawapo wa lahaja za Kiswahili, kwa hivyo kutupa mwanga kuhusu mwelekeo wa uchanganuzi wetu.

Maringah (1987) amefanya ufafanuzi wa viambishi vya vitenzi kiulinganishi katika Kiswahili na Kimbeere. Amebainisha kauli sita za 'mnyambuliko' zikiwemo kauli za kutendesha, kutendea, kutendeka, kutenduka, kutendewa na kutendwa. Kazi hiyo ilikuwa na umuhimu kwetu kwani inaeleza bayana kwamba viambishi vya kauli ni viambishi tamati. Japo Maringah ametumia nadharia ya Sarufi Zalishi Geuza Maumbo, tasnifu hiyo ilitupa mwelekeo kuhusu kauli nyinginezo katika vitenzi.

Kulikov et al (2006) ilitufaa katika kuelewa dhana ya sentensi elekezi. Wataalam hawa wanaeleza kuwa sentensi elekezi huweza kuchukua yambwa moja au mbili. Isitoshe, wanapendekeza njia tano za kutofautisha kiima na yambwa katika sentensi: kutumia uhusika (case), upatanisho (agreement), uchaguzi (selection) msambao (precedence) na mkazo (prominence) (uk. 272).Kazi hiyo hata hivyo haijishughulishi na kipengele cha kauli. Utafiti wetu ulitumia maarifa ya kazi hii kuchanganua suala la yambwa katika sentensi elekezi ya Kiswahili sanifu pamoja na uhusiano wa yambwa hizo na kauli.

Habwe na Karanja (2004) wameshughulikia vipengele mbalimbali vya taaluma ya isimu. Mojawapo wa hivyo ni vitenzi vya Kiswahili. Chini ya mada 'Muundo wa Kitenzi cha Kiswahili', wataalam hawa wameeleza kwa uketo viambishi mbalimbali vikiwemo vile vya kauli. Kazi hii imeainisha kauli nane za viambishi vya vitenzi vya Kiswahili na kwa sababu hiyo ilituongoza katika utafiti wetu wa viambishi hivi vya kauli. Aidha kazi yao imeeleza kauli nje ya mipaka ya sentensi elekezi. Utafiti wetu uliendа zaidi ya hatua hiyo na kushughulikia kauli katika sentensi elekezi ya Kiswahili sanifu.

### 1.8.3. YALIYOANDIKWA KUHUSU NADHARIA

Katika juhudi za kuelewa Nadharia ya banifu, tulidurusu kazi za wataalam tofauti tofauti, zikiwemo zile zilizochapishwa, makala na tasnifu za kiusomi.

Miongoni mwa kazi zilizotupa uelewa wa kimsingi wa nadharia ya Ubanifu ni zile za Chomsky (1993 na 1995). Katika kazi hizi, Chomsky anafafanua dhana ya umilisi na kubainisha kwamba umilisi ni wa aina mbili. Unahusu Ufasiri wa Matamshi (Articulatory-Perceptual) na Utambuzi wa Fikra (Conceptual-Intentional). Kwa kupitia kwa maelezo haya tuliweza kuelewa awamu mbili za uwasilishaji; UF na UM, awamu ambazo ni matokeo ya Mjumuiko.

Katika kazi ya 1995, Chomsky anaeleza kwa kina nafasi ya leksikoni katika kubeba habari za kimofosintaksia za vitenzi na nomino. Anafafanua pia mfanyiko wa kimkokotoo na taratibu zake za muungano na mdhihiriko wazi, kama michakato inayoishia katika uzalishaji wa tungo sahihi kisemantiki na kimatamshi katika lugha asilia. Aidha kazi hii (1995:200) inatoa maelezo muhimu kuhusu Kanuni ya Iktisadi, mhimili muhimu wa nadharia ya Uminimalisti. Kanuni hii hutagusana na kanuni nyinginezo zinzohusisha usogezi kwa manufaa ya ukaguzi Sifa katika kuhakikisha kwamba ni sifa zihitajikazo za tungo tu ndizo zitumiwazo katika mkokotoo ili kuunda tungo sahihi.

Radford (1997) ametoa ufafanuzi wa kina kuhusu chimbuko la nadharia ya Ubanifu na uhusiano wake na nadharia ya awali ya U na M. Radford anaeleza sifa ya Mipaka na Masharti kama ilivyotumiwa katika U na M, na namna inavyotumika katika nadharia ya Ubanifu. Mipaka na masharti ni nadharia inayoziona sarufi za lugha asilia kama zilizo na ubia. Inatoa maelezo ya kijumla kuhusu sarufi za ulimwengu lakini pia inatambua tofauti za lugha kwa namna zinavyofinyanga kanuni fulani kukidhi mahitaji ya lugha mahususi. Ni

kupitia ufafanuzi huu ambapo Radford alituelekeza kuelewa nafasi ya nadharia ya Ubanifu katika kubana na kusahilisha shughuli ya kujifundisha lugha miongoni mwa watoto kwani nadharia hii ina kanuni chache sana na za jumla kuhusu lugha, tofauti na nadharia iliyoitangulia ya U na M. Kazi hii pia ilitusaidia kuelewa Kanuni ya Ufasiri wa Kina, sharti la nadharia ya Ubanifu lihakikishalo kuwa tungo zalika ni sahihi (1997:171).

Singleton (2000:23) anafafanua umuhimu ambao kitengo Leksikoni kimepewa tangu miaka ya 1980, wakati nadharia ya U na M ilipoasisiwa. Mtaalam huyu anaeleza kwamba muundo wa vipashio vya lugha kama vile virai hutegemea mofolojia na sintaksia ya lugha husika mbali na sifa za kileksika za kila kichwa cha kirai. Kazi hii ilichangia pakubwa uelewa wetu kwamba leksikoni ni kipengele muhimu katika kuzalisha tungo za lugha kwani ndiyo inayobeba leksika na sifa za kimofosintaksia za nomino na vitenzi.

Kaviti (2004) ilikuwa kazi tunu katika utafiti wetu. Msomi huyu ameshughulikia mofosintaksia ya Kikamba kwa kutumia nadharia ya Ubanifu. Kaviti anaeleza kwamba nadharia hii haijakengeuka sana kutoka kwa ile ya U na M. Anaendelea kufafanua sababu mbili zilizomchochea Chomsky kuasisi nadharia hii. Fauka ya kutoa maelezo kuhusu leksikoni na mfanyiko wa kimkokotoo, kazi hii inafafanua kategoria amilifu na kategoria leksika. Kategoria amilifu kama vile njeo, hali, upatanifu, kauli n.k. Kwa upande mwingine kategora za kisarufi ni kama vile nomino, vivumishi, vitenzi n.k. Sifa kuu ya kategoria hizi ni kwamba huwa na maana na antonimu katika lugha. Uelewa wa kategoria hizi ulikuwa muhimu kwetu hasa ikizingatiwa kuwa sentensi ya Kiswahili huwa nazo katika usanjari fulani. Kikamba ni lugha ambishibainishi kama Kiswahili. Kazi hii kwa hivyo kazi hii ilitupa mwanga kuhusu uambishaji katika lugha hii, hali ambayo inawiana sana na uambishaji katika vitenzi vya Kiswahili sanifu.

Haegeman (1994) amefanya ufafanuzi wa kina kuhusu nadharia ya U na M. Kazi hii pia inatoa habari muhimu kuhusu nadharia za awali; ubora na upungufu wake. Inafafanua vijinadharia mbalimbali vya nadharia hii 'jumuishi' kama vile Thita, Ufunge, X-ba, Utawala, Umilikifu na Masharti. Kupitia kwa maelezo yake tulifahamu kipengele cha X-ba cha Spesifaya-Kichwa na Kichwa-Kichwa. Kipengele hiki kilikuwa muhimu kwa utafiti wetu kwani kilituongoza kuelewa miundo mbalimbali ya tungo kama vile virai na sentensi katika Kiswahili sanifu.

Schroeder (2005) ilikuwa muhimu kwa utafiti tulioufanya. Makala haya yanatoa muhtasari wa uundaji wa tungo kutokea katika kitengo leksikoni, mfanyiko wa kimkokotoo, Muungano

na Mdhihiriko Wazi hadi katika Mjumuiko. Tulitumia uelewa huu kufafanua kauli za vitenzi katika sentensi elekezi ya Kiswahili sanifu.

## 1.9. MBINU ZA UTAFITI

Utafiti huu kwa jumla ulikuwa wa maktaba. Ili kupata habari zilizotusaidia kutosheleza mahitaji ya mada yetu ya utafiti, tulisoma vitabu, majarida ya kiusomi na makala ya kitaalamu. Aidha tulisoma tasnifu mbalimbali za watafiti wa awali katika viwango vya shahada ya uzamili na kile cha uzamifu, hasa zile zinazohusiana na mada yetu ya utafiti. Tulistahabu kutumia mbinu hii kwa kuwa Kiswahili sanifu kinapatikana zaidi katika maandishi. Kiswahili sanifu hutumiwa kwa nadra sana na wazungumzaji, tena katika mawanda finyu sana.

Fauka ya mbinu hii utafiti wetu ulizingatia makala muhimu katika tovuti za kiusomi. Zaidi ya mbinu hizi, utafiti huu ulijikita katika mijadala na ushauri wa kiusomi kutoka kwa wahadhiri, wasomi mbalimbali pamoja na wanafunzi wenzetu. Muhimu zaidi ulikuwa mchango wa Wahadhiri waelekezi wa mtafiti kwani ushauri wao ulitegemewa zaidi kutimiza mahitaji ya mada yetu.

Mtafiti pia alitumia ujuzi wake wa lugha ya Kiswahili kutunga sentensi elekezi. Katika utafiti huu tulitumia vitenzi arobaini na tano. Kati ya vitenzi hivi, ishirini na tano vilikuwa vya asili ya Kibantu, kumi na tano vilikuwa vya asili ya kigeni na vitano vilikuwa vya silabi moja. Baada ya kuchagua vitenzi hivi, tulitumia kamusi mbalimbali kukadiria usanifu wake. Baadhi ya kamusi tulizotumia ni:

TUKI (1980) *Kamusi ya Kiswahili Sanifu*

TUKI (2003) *English- Swahili Dictionary.*

Kwa kuwa kazi hii ilihusu kauli, tulivitia vitenzi hivyo viambishi mbalimbali vya kauli ili kufafanua aina tofauti za kauli katika Kiswahili katika jitihada za kutimiza malengo yetu ya utafiti.

## 1.10. UMUHIMU WA UTAFITI

Kadiri ya uelewa wa mtafiti wa kazi hii, kuna maandishi kadhaa kuhusu kauli za uambishaji. Maandishi hayo hata hivyo, yana upungufu wa kimaelezo na hata mengine yanapotasha. Tunatarajia kwamba utafiti huu utakuwa ni mchango mkubwa sana katika taaluma ya isimu. Nadharia ya Ubanifu ni nadharia ya hivi karibuni katika uchunguzi wa lugha asilia. Watafiti kadhaa wameitumia nadharia hii katika kuchanganua vipengele tofautitofauti katika lugha ya Kiswahili sanifu. Utafiti huu unatarajiwa kusaidia kueleza dhana ya kauli katika msingi wa nadharia hii ya Ubanifu.

Aidha yalikuwa matumaini yetu kwamba matokeo ya utafiti huu yangechangia kuwachochea watafiti wengne kutafiti kuhusu viambishi vingine vya vitenzi kama vile kiima, dhamira, mahali na kadhalika. Pamoja na hilo yalikuwa matarajio yetu kwamba watafiti wengine watachochewa kufanya utafiti sio tu katika viambishi vya Kiswahili sanifu lakini pia katika lugha nyinginezo asilia, ama kwa nadharia ya Ubanifu au nadharia nyingine ile.

Tulitumai pia, kwamba utafiti huu ungechangia pakubwa kuleta uelewa mzuri wa sentensi elekezi ya Kiswahili Sanifu miongoni mwa watumizi wa lugha hii. Hatimaye, tulitarajia kwamba utafiti wetu ungeondoa utata tulioutaja hapo awali wa uambishaji na unyambuaji kama taratibu mbili tofauti katika lugha asilia.

## 2.0.SURA YA PILI: DHANA ZA UNYAMBUAJI NA UAMBISHAJI

### 2.1.UTANGULIZI

Katika sura hii tutashughulikia dhana za unyambulishaji na uambishaji. Tutaonyesha namna taratibu hizi zinavyojitokeza katika Kiswahili sanifu. Aidha, tutapania kuonyesha tofauti kati ya taratibu hizi mbili za sarufi. Tutaonyesha kwa kina taratibu za uambishaji wa vitenzi vya Kiswahili sanifu huku tukitoa mifano halisi ya vitenzi na sentensi elekezi za Kiswahili.

### 2.1.1. UNYAMBUAJI

Unyambulishaji ni utaratibu wa kupachika viambishi kwenye mizizi ili kuunda maneno mapya (Massamba 2004:105). Fasili hii ina maana kwamba maneno mapya yanaweza kuundwa kutokana na yaliyopo kwa kutia mofimu mbalimbali katika mizizi ya maneno hayo chanzi.

Kulingana na Bussman (1996), unyambuaji ni utaratibu wa uundaji maneno kutokana na mengine ambapo maneno zalika huwa ya kategoria tofauti za kisarufi na yale chanzi. Mathalani, nomino zaweza kuundwa kutokana na vitenzi, ilhali kutokana na nomino vivumishi vywaweza kunyambuliwa kama inavyodhirika katika mifano:

3. Vitenzi — Nomino
   a) Soma — somo, usomi, msomi
   b) Jenga — jengo, ujenzi, mjenzi

4. Nomino — Vivumishi
   a) Ujanja — mjanja
   b) Uhodari — hodari

5. Vivumishi — Vielezi
   a) -zuri — vizuri
   b) -baya — vibaya

6. Vivumishi — Vitenzi
   a) Duni — dunisha

b) Harabu haribu

Katika lugha ya Kiswahili sanifu, mofimu za unyambuaji huwa viambishi awali na vile tamati.

2.1.2. UAMBISHAJI

Kulingana na Massamba (2004:89), uambishaji ni utaratibu wa taaluma ya mofolojia unaohusisha kuweka kiambishi kabla, katikati na baada ya mzizi. Fasili hii, hata hivyo, haituwezeshi kubainisha tofauti kati ya taratibu hizi mbili za uambishaji na unyambuaji. Tungependa kuongeza na kubainisha kwamba, uambishaji huhusisha kulipanua au kulirefusha neno kimlalo na kuliweka katika hali tofautitofauti za kategoria iyo hiyo husika ya kisarufi (Habwe na Karanja 2004:91).

Crystal (2003:233) anaifafanua dhana hii vyema anapodokeza kuwa mofimu za uambishaji huwa na uamilifu wa kuonyesha mahusiano ya kisarufi kama vile njeo, nafsi, hali, umoja na wingi n.k na utaratibu huu hausababishi kuzalika kwa maneno ya kategoria tofauti. Kwa mfano, kutokana na mzizi wa nomino -tu, tunaweza kuunda nomino mbalimbali kwa kuongeza mofimu awali:

7. -tu **m**tu (hali wastani)

**Kiji**tu (hali ya udogo)

**Ji**tu (hali ya ukubwa)

Utu (nomino dhahania)

2.1.3. TOFAUTI KATI YA UNYAMBUAJI NA UAMBISHAJI

Dhana hizi mbili zimezua hali ya kutofautiana kwa maoni kati ya wanaisimu wa taaluma ya mofolojia (Katamba 1993:47). Kutoafikiana huku kunatokana na hali kwamba taratibu hizi zinahusiana pakubwa na hata kuingiliana. Wanasarufi wanaoshughulikia lugha moja huenda wasikubaliane endapo utaratibu fulani ni uambishaji au unyambulishaji. Aidha katika lugha tofautitofauti, huenda utaratibu fulani uwe unyambulishaji na katika nyingine uwe uambishaji. Hali hii ndiyo inayotuchochea kuweka mipaka ya tofauti kati ya taratibu hizi mbili. Tunakusudia kuonyesha tofauti kuu kati ya taratibu hizi mbili zinazohusu maneno katika lugha kwa kuzingatia vipengele kadhaa.

2.1.3.1.Upambanuzi wa Kisintaksia

Uambishaji ndio utaratibu kuhusu maneno unaohusiana pakubwa na sintaksia. Uambishaji, kwa mfano, katika vitenzi huzua hali tofautitofauti za kisarufi kama vile njeo, ukanushi, nafsi, umoja na wingi, kauli miongoni mwa nyinginezo. Tataeleza hali hii kwa kuzingatia kitenzi 'cheza' ambapo viambishi mbalimbali vina uamilifu tofautitofauti wa kisarufi;

8. a) A-li-m-chez-e-a

b) Wa-nge-chez-e-an-a

c) Ni-si-ngali-ku-chez-esh-e-a.

Tutafafanua viambishi hivi kwa kina katika aya za hapo mbele.

2.1.3.2.Uzalishaji

Utaratibu wa uambishaji huweza kuchangia kuzalishwa kwa maumbo mengi yenye maana tofautitofauti kutokana na leksimu moja kuliko unyambuaji. Hili linatokana na uhalisi kwamba, kuna viambishi vingi ambavyo huwa na uamilifu mwingi wa kisarufi katika lugha kama inavyojitokeza katika mifano;

9. a) Unyambuaji:

Lim.a Kilimo

Ukulima

Mkulima

Ulimaji

9. b) Uambishaji:

Lima limia

Usilime

Limeni

Watalima

Limianeni

Wasingelima

Hatamlimia

Wangelimishiana

Nilivyolima

Kulimiana n.k

Kama inavyodhihirika katika mfano tulioutoa hapo juu, unyambuaji huzua ufungizi hivi kwamba hauzalishi msamiati mwingi kama vile uambishaji. Tungependa kuongeza kuwa utaratibu wa kuambisha katika mfano tulioutoa hapo juu unaweza kuzalisha maneno mengi zaidi ya mifano michache tuliyoitaja. Katika lugha ya Kiswahili, ni muhali kwa unyambuaji kwenda zaidi ya hatua sita. Uambishaji huzua mofu nyingi zenye majukumu mbalimbali ya kisarufi.

2.1.3.3.Taratibu za Kimaana

Katika kipengele hiki tunatathmini utaratibu unaozua tofauti za kimaana ambapo maneno zalika huweza kuingizwa katika makamusi kama vidahizo. Kila neno litokanalo na utaratibu wa unyambuaji huweza kuingizwa na likajisimamia katika kamusi kama kidahizo chenye maana. Kwa upande mwingine, maneno yaliyoambishwa huwa hayajisimamii katika kamusi. Isitoshe, viambishi kama vile vya kauli huonyeshwa baada ya kutolea kidahizo ufafanuzi. Kwa mfano, maneno yanayonyambuliwa kutoka kwa kitenzi 'la' kama vile chakula, mlo, ulaji, lishe na mlafi yanajitokeza kama vidahizo katika TUKI (1990).

2.1.3.4.Mabadiliko ya Kategoria

Unyambuaji ni utaratibu wa kimofolojia wa kuunda maneno mapya na huhusu hali ambapo maneno zalika huwa ya kategoria mpya (Bussman 1996). Kwa mfano, kutokana na kitenzi 'piga' tunapata nomino 'pigo'. Katika uambishaji, kwa upande mwingine, neno hutiwa viambishi vya upanuzi na likasalia katika kategoria iyo hiyo. Mathalani, kitenzi 'shona' chaweza kuambishwa na kusalia kitenzi kinachodhihirika kama 'shonea', 'atamshonea' hawakushoneana' n.k.

2.1.3.5.Mazingira ya Udhihirikaji

Mofimu za unyambuaji hutokea karibu sana na mzizi kuliko zile za uambishaji. Hali hii inabainika vyema sana katika lugha ya Kiingereza ambapo, kwa mfano, katika neno 'governments' mofimu ya unyambuaji '–ment' iko karibu na mzizi na inatangulia ile ya uambishaji –s (idhihirishayo wingi wa nomino). Aidha, katika lugha kama vile Kiingereza, mofimu za uambishaji hutokea tu baada ya mzizi. Katika Kiswahili sanifu hata hivyo, mofimu, zote; za uambishaji na unyambuaji hutokea kabla na baada ya mzizi. Mathalani'

Unyambuaji:

**10. a) Uchezaji**

**b) Mchezo**

Uambishaji:

**11. a) Alimchezea**

**b) Watachekeana.**

Baada ya kuonyesha tofauti kati ya unyambuaji na uambishaji, hebu sasa tufafanue Uambishaji wa Vitenzi vya Kiswahili sanifu.

2.2.UAMBISHAJI WA VITENZI

Kama tulivyotaja awali, uambishaji ni utaratibu wa kupachika viambishi kabla, katikati na baada ya mzizi. Kila kiambishi katika neno hutekeleza jukumu mahususi la kisarufi. Kila lugha ina utaratibu wake wa kuambisha. Kiswahili sanifu ni lugha ambishi bainishi. Hili lina maana kwamba mizizi yake huweza kuchukua viambishi na viambishi hivyo vikaweza kupambanuliwa kwa kuwa havichangamani na mzizi. Miongonii mwa maneno yanayoambishwa katika Kiswahili sanifu ni vitenzi.

Vitenzi vya Kiswahili, kama tulivyodokeza hapo awali, huchukua viambishi awali na viambishi tamati ambavyo hutokea kabla na baada ya mzizi mtawalia[1]. Vitenzi huchukua viambishi hivyo tofauti katika mpangilio fulani, hali ambayo wataalam kama vile Iribemwangi (2008) na Polome (1967) wanaitaja kama muundo wa kitenzi cha Kiswahili. Tutaanza kwa kufafanua viambishi awali.

### 2.2.1. Viambishi Awali

Kama tulivyotaja awali, viambishi hivi hutokea kabla ya mzizi. Wataalam mbalimbali wanajitokeza na idadi tofauti ya viambishi hivi. Mathalani, Schadeberg (1984) anatambua viambishi awali saba ilhali Polome (1967) anabainisha jumla ya viambishi awali vitano. Mgullu (1999) na Habwe na Karanja (2004) wanabainisha nafasi kumi, na sita mtawalia za viambishi hivi. Japo uainishaji huu unatofautiana kwa kiasi fulani, kuna nafasi maalum za viambishi hivi zinazobainika katika fafanuzi za wataalam hawa. Aidha sio lazima viambishi hivi vitokee kwa pamoja katika kitenzi. Kutokea kwa viambishi fulani kunaoana na kanuni ya Ufasiri wa Kina wa nadharia ya Ubanifu ambayo hukubalia vipashio vinavyohitajika tu kudhihirika katika utaratibu mzima wa kimkokotoo. Tutaonyesha nafasi hizi hapa chini:

#### 2.2.1.1. Viambishi awali vya ukanushi

Kwa mujibu wa Polome (1967), nafasi hii huchukuliwa na kiambishi {ha} na {hu} vya nafsi ya pili na tatu mtawalia. Tunaongeza kwamba kiambishi kikanushi cha nafsi ya kwanza {si} pia kinaangukia katika nafasi hii. Viambishi hivi hudhihirika kwa maumbo tofautitofauti kutegemea idadi (umoja na wingi). Mathalani:

Kiambishi {hu} hudokeza ukanushi wa nafsi ya pili umoja. Mathalan:

Unaimba **hu**imbi.

Kiambishi {ha} huwakilisha ukanushi nafsi ya pili, wingi. Kwa mfano:

Mliimba **ha**mkuimba.

Aidha, kiambishi hiki huwa na uamilifu wa ukanusho wa nafsi ya tatu katika hali ya umoja na wingi –hachezi, hawachezi. Kiambishi hiki {ha} pia huwakilisha ukanusho wa vitu visivyo na nafsi. Kwa mfano,

12. a) Jino **ha**liumi.

b) Njia hii **ha**ipitiki.

1. Viambishi vya nafsi na ngeli

Viambishi hivi hutekeleza jukumu la upatanisho wa kiima katika vitenzi yakinishi. Maadamu Kiswahili ni lugha inayoweza kuwa na kiima kisicho dhahiri viambishi hivi hutiwa katika vitenzi ili kufanikisha upatanisho wa kiima[2].

a) Viambishi vya nafsi

Viambishi vya nafsi huwakilisha viumbe vyote vyenye nafsi kama vile binadamu, wanyama, ndege na wadudu.Vambishi hivi huwakilisha m(wa)tendaji katika umoja na wingi. Kuna nafsi tatu zinazodhihirika katika umoja na wingi:

i) Nafsi ya kwanza.

Nafsi hii huwakilisha m(wa)semaji. Vimbishi vya nafsi ya kwanza ni {ni} katika umoja na {tu} katika wingi. Mathalani

| 13. Umoja | Wingi |
|---|---|
| a) **Ni**nasoma | **tu**nasoma |
| b) **Ni**liandika | **tu**liandika |

ii) Nafsi ya pili

Viambishi vya nafsi ya pili huwakilisha m(wa)tu wa pili ambaye hushiriki katika mawasiliano kama mrejelewa; ni yule anayeambiwa au anayesikiliza. Mofu za nafsi hii ni {u} na {m} katika umoja na wingi mtawalia. Kwa mfano,

| 14. Umoja | Wingi |
|---|---|
| a) **U**tasafiri | **m**tasafiri |
| b) **U**nanisikiliza | **m**natusikiliza |

iii) Nafsi ya tatu

Nafsi hii huwakilisha m(wa)tu katika nafsi ya tatu ambao wanazungumziwa ila hawajitokezi moja kwa moja katika mazungumzo. Mofu za nafsi ya tatu ni {a} na {wa} katika umoja na wingi mtawalia kama idhihirikavyo katika mifano hapa chini:

15. Umoja Wingi

a) Anaamini **W**anaamini.

b) Alimpikia. **Wa**liwapikia.

b). Viambishi vya ngeli

Viambishi hivi huwakilisha kiima ambacho hakina nafsi. Kiambishi hiki hutokea katika mzizi kama kipatanisho cha kiima. Umbo la kiambishi cha ngeli hutegemea ngeli ya nomino husika. Kwa mfano;

Ngeli ya U-YA

16. Umoja Wingi

a) Uasi **u**lizuka. Maasi **ya**lizuka.

b) Ugonjwa utamponza. **Ma**gonjwa yatawaponza.

Ngeli ya LI-YA

Viambishi vya ngeli hii katika umoja na wingi ni li- na ya- katika umoja na wingi mtawalia. Mathalani,

17. Umoja Wingi

a) Gari lake **li**libingiria. Magari yao **ya**libingiria.

b) Hili tunda **li**naliwa. Haya matunda **ya**naliwa.

Ngeli ya I-ZI

Mofu za ngeli ya I-ZI ni {i-} katika hali ya umoja na {zi-} katika wingi. Kwa mfano,

18. Umoja Wingi

a). Meza **i**liundwa juzi. Meza **zi**liundwa juzi.

b). Saa **i**liyopotea **i**mepatikana. Saa **zi**lizopotea **zi**mepatikana.

Kwa jumla viambishi vya ngeli ni vingi kadri ya ngeli za nomino katika lugha ya Kiswahili sanifu. Aidha baadhi ya ngeli hudhihirika kwa mofu moja kwa kuwa hazina dhana ya umoja na wingi. Mifano ya ngeli hizo ni ngeli ya I-I, KI-KI, LI-LI na YA-YA.

2.2.1.3. Viambishi vya Njeo

Njeo huelezwa kwa virejelezi vya 'sasa' na hapa, na hivyo matukio hutokea au hukosa kutokea wakati uliopita, uliopo na ujao (Karimi (2008:64). Njeo ni kategoria inayotumiwa katika ufafanuzi wa kisarufi kueleza namna lugha zinavyoakisi wakati tendo lilipotokea au halikutokea. Kulingana na Crystal (1980:348), njeo huhusu wakati wa kuzungumza ambao huchukuliwa kama kiini usonde cha 'sasa'.

Kuna aina tatu za njeo: njeo iliyopita, njeo ya sasa na ijayo (Comrie 1985:36).

i). Njeo iliyopita

Njeo iliyopita huonyesha kuwa jambo fulani lilifanyika au halikufanyika wakati fulani uliopita; wakati kabla ya kuzungumza. Njeo iliyopita huwakilishwa kwa mofu {li} na {ku} katika hali yakinishi na hali kanushi mtawalia. Kwa mfano,

| 19. Hali yakinishi | Hali kanushi |
|---|---|
| a) A**li**mkaribisha. | Ha**ku**mkaribisha. |
| b) Wa**li**zua zogo. | Hawa**ku**zua zogo. |

Mohammed (2001:128), akimrejele Ashton (1982) anaongeza kuwa njeo iliyopita hudokezwa pia na kiambishi –ali-.Kwa mfano;

| | | |
|---|---|---|
| 20. a) N-ali-penda | Nalipenda. | (nafsi ya kwanza, umoja) |
| b) Tw-ali-penda. | Twalipenda. | (nafsi ya kwanza wingi) |
| c) Mw-ali-penda. | Mwalipenda. | (nafsi ya pili wingi) |
| d) W-ali-penda. | Walipenda. | (nafsi ya tatu wingi). |

Utafiti huu haukubaliani katu na maelezo haya. Hii ni kwa kuwa matumizi haya hayajitokezi katika Kiswahili sanifu. Kwa hivyo, tunasema kuwa huenda hali hiyo ikawa ni bayana katika baadhi ya lahaja tu wala sio katika Kiswahili sanifu.

ii) Njeo iliyopo

Njeo iliyopo huonyesha kwamba tendo linatokea sasa; sambamba na uzungumzaji. Mofu za njeo hii ni {na}, {a} na {Θ} katika vitenzi yakini na kanushi.

21. a) Ki**na**somwa. Vi**na**somwa.

b) Yu**a**lima. Wa+Ølima.

c) A+Ølima. Wa+Ølima.

Kulingana na Mohammed (2001:126) kiambishi -a- ni kibadala cha kiambishi {na} kwani hudhihirika kama mofimu ya kuonyesha njeo iliyopo katika lahaja tofautitofauti. Sisi tunatofautiana na ufafanuzi huo na kwa hivyo kuafikiana na Mbaabu (1985) kwamba kiambishi {a} hudhihirisha wakati usio bayana. Mathalani, katika sentensi;

22. a) Bush **a**rushiwa kiatu

Wakati unaotajwa katika sentensi hii hapa juu haudhihiriki kuwa maalum. Hali hii hujitokeza sana katika vichwa vya habari kwa nia ya kuibua hisia za taharuki na ari ya kusoma au kufuatilia habari hizo miongoni mwa hadhira lengwa. Sentensi hiyo inatofautiana na:

22. b) Bush a**na**rushiwa kiatu.

Hali inayodokezwa inabainisha wazi kwamba tendo la kurusha kiatu linafanyika sambamba na usemaji.

Licha ya kuonyesha njeo iliyopo, mofu {na} huwakilisha hali ya kuendelea. Tathmini sentensi:

23. Mimi ninasoma katika Chuo kikuu cha Nairobi.

Katika sentensi hii, ni bayana kuwa kusoma huku sio suala la wakati au muda mfupi tu bali ni tendo ambalo linachukua kipindi kirefu, yamkini miaka miwili.

iii) Njeo ijayo

Njeo ijayo huwakilishwa kwa mofu {ta}. Hii huonyesha kuwa kitendo kitafanyika wakati baada ya sasa. Kwa mfano;

24. a) Tu**ta**safiri vyema.

b) Wakenya wa**ta**sifia amani.

Mbali na kiambishi –ta-, mofu {takapo} pia hutumiwa kuonyesha vitendo vinavyotarajiwa. Mofu hiyo, hata hivyo, hutumiwa pamoja na –ta- katika sentensi ili kuifanya sentensi husika kuwa sahihi. Zingatia sentensi:

25. a) Wa**takapo**potea watatafutwa.

b) Binadamu atapata amani a**takapo**jifundisha kuwa mwenye subira.

Kama inavyodhihirika katika mifano hii, inajitokeza pia kwamba mbali na kuonyesha wakati ujao, kiambishi –takapo- pia huakisi hali ya masharti. Hili lina maana, kwa mfano kwamba katika mfano wa kwanza, kutafutwa kwa walengwa kunategemea kupotea kwao. Lau hawatapotea hawatatafutwa.

Kiambishi hiki –takapo- hukanushwa kwa kiambishi –sipo-. Mathalani:

25. c) Wa**sipo**soma hawatajua.

2.2.1.4. Viambishi vya hali

Kulingana na Massamba (2004:15), hali

'... ni kipengele cha kisarufi ambacho hutumika kwa kuandamana na kitenzi, kisingi kikiwa na uamilifu wa kuonyesha ama kukamilika au kutokamilika kwa tendo linalotajwa.'

Hali, tofauti na njeo ambayo ni kipengele cha kiusonde kinachoakisi urejelezi wa kitendo mintaarafu wakati wa kukizungumzia, huonyesha taswira ya ndani ya vitendo kwa misingi ya kukamilika kwake au kutokamilika katika kipindi fulani cha wakati (Comrie 1976:3).

Viambishi hivi huonyesha kama vitendo vimekamilika, vinaendelea kutendeka, hutendeka kila mara au hujirudiarudia. Viambishi vya hali havitokei kwa pamoja katika kitenzi na vile vya njeo; huwa na uhusiano wa mgawanyo wa kiutoano katika kitenzi cha Kiswahili hivi kwamba endapo kitenzi kina kiambishi cha hali, hakiwezi kuambishwa mofu ya njeo. Hata hivyo, kuna kiambishi cha njeo –na- ambacho hutekeleza jukumu la hali kama tulivyotaja awali. Kuna viambishi mbalimbali vya hali kama tutakavyojadili hapa chini;

i). Viambishi vya Hali Timilifu

Viambishi hivi ni –me- na –ja- katika hali yakinishi na hali kanushi mtawalia. Hali timilifu huonyesha kwamba tendo lilifanyika wakati uliopita lakini kutokea kwake kuna athari kwa wakati wa sasa. Mathalani:

26. a) Juma a**me**safiri Mwanza.

b) Juma ha**ja**safiri Mwanza.

Hali timilifu huweza kuonyesha wakati uliopita na wakati ujao pia. Tutafafanua hili kwa kutumia sentensi:

26. c) Mataifa mengi ya Afrika yalikuwa ya**me**jinyakulia uhuru kufikia 1970.

d) Mama akija nitakuwa ni**me**pika.

Katika mfano wa kwanza, kufikia mwa wa 1970 uhuru ulikuwa umepatikana katika mataifa mengi. Katika mfano wa pili, msemaji atakuwa amepika kisha muda mfupi baadaye mamake afike. Katika kufanikisha hali hii timilifu katika wakati uliopita na ujao, viambishi –li- na –ta- vinafungamanishwa na kitenzi 'kuwa' mtawalia.

ii) Viambishi vya hali ya Mazoea

Hali ya mazoea huonyesha kuwa vitendo hutokea au havitokei mara kwa mara, kwa kujirudiarudia au kwa kawaida. Kiambishi cha hali ya mazoea hali yakinishi ni –hu- ilhali kile cha ukanusho ni –ha-katika ngeli zote na katika nafsi zote isipokuwa katika nafsi ya kwanza umoja ambapo kiambishi cha ukanushi ni –si-. Tathmini sentensi:

| 27. Hali yakinishi | Hali kanushi |
|---|---|
| a) Kalamu hii **hu**andika vyema. | Kalamu hii **ha**iandiki vyema. (ngeli I-ZI) |

b) Mimi **hu**penda sinema. Mimi (huwa) **si**pendi sinema. (nafsi ya kwanza umoja)

Kama inavyodhihirika katika mifano hii, sentensi kanushi ya hali ya mazoea huwa na maana mbili hivi kwamba uelewa wake hutegemea muktadha wa mazungumzo. Maana ya kwanza ni kwamba kitendo kinachoakisiwa katika kitenzi hakitokei sasa, na maana ya pili ni ile ya mazoea, kwamba kitendo husika huwa hakitokei mara kwa mara.Hali hii huwafanya wazungumzaji kutia kitenzi kisaidizi 'huwa' kabla ya kitenzi kikuu kinachokanushwa ili kubainisha hali hiyo ya mazoea.

2.2.1.5. Kiambishi cha masharti

Viambishi vya masharti katika vitenzi vya Kiswahili ni –ki- na –sipo- katika hali yakinishi na kanushi mtawalia. Kiambishi –ki- cha masharti hutumiwa katika sentensi yenye vitenzi viwili kuonyesha kwamba kutokea kwa kitenzi cha pili hutegemea kutokea kwa kile kilichoambishwa mofu {ki}. Kwa mfano, katika sentensi;

28. a) Mvua i**ki**nyesha nitapanda mbegu.

Inabainika kwamba upanzi wa mbegu utafanyika tu endapo mvua itanyesha. Ikiwa mvua haitanyesha, kwa hivyo, mhusika hatapanda mbegu. Katika kukanusha sentensi hiyo inakuwa;

28. b) Mvua **isipo**nyesha sitapanda mbegu.

Katika mfano huu, upanzi hautafanyika endapo mvua haitanyesha; ni sharti mvua inyeshe ndipo upannzi wa mbegu utekelezwe.

2.2.1.6. Kiambishi –ka-

Kiambishi –ka- hutumiwa kuonyesha vitendo vilivyo katika hali ya mfululizo wa kufuatana. Kiambishi hiki kinapotumiwa katika sentensi kama hiyo, kitenzi cha kwanza huwa na kiambishi cha njeo iliyopita –li-. Mathalani,

29. a) Mgeni alifika, a**ka**pokelewa kwa takrima, a**ka**hutubia umati, a**ka**pongezwa, a**ka**tuzwa na a**ka**ondoka kwa hiari.

Kama inavyodhihirika katika mfano huu, kitenzi cha mwanzoni mwa sentensi hakiambishwi mofu {ka} bali ni vile vitenzi vifuatilizi vinavyoambishwa.

Mbali na matumizi hayo tuliyoyaeleza hapo juu, kiambishi –ka- huonyesha pia kwamba tendo fulani ni tokeo la jingine, hasa lile linalotangulia. Kwa mfano,

29. b) Mwanasiasa huyo aliifisidi nchi **aka**pigwa kalamu.

Sentensi hii ina maana kwamba mwanasiasa alipigwa kalamu kwa sababu aliiba. lau asingeiba asingepigwa kalamu.

Huku *akiafikiana na Wilson (1970)*, Mohammed *(2001:160)* anaongeza kuwa mofu hii hutumiwa katika vichwa vya habari, hasa magazetini na katika runinga kwa nia ya kuibua hisia ya ari ya kusoma kisa husika miongoni mwa hadhira lengwa. Hali hii inachochewa na uhalisi kwamba vyombo vya habari hukusudia kuonyesha kuwa habari fulani bado ni geni kwani havitaki kuifungamanisha na wakati uliopita. Hali hii ndiyo inayobainika katika sentensi:

30. Waziri **ka**pigwa kalamu.

Kikitumiwa kwa maana hii, kiambishi hiki hutokea mwanzoni mwa sentensi na huhusisha nafsi ya tatu umoja.

2.2.1.7. Viambishi vya uwezekano na masharti –nge-, -ngali- na –ngali-

Mohammed (2001) anaeleza kuwa kiambishi –nge- kilielezwa na wanasarufi mapokeo kuwa ni kiambishi kinachotumiwa kuakisi matendo ambayo ni ya kutamanika tu lakini yasiyoweza kutokea. Anatoa mfano wa sentensi;

'Ni**nge**kuwa tajiri ni**nge**wasaidia maskini.' Huku tukikubaliana na maelezo hayo, tunaongeza kwamba, mofu {nge} hutumiwa pia kuonyesha uwezekano ambao haukutekelezwa/ haukutimizwa wakati uliopita. Katika mfano huo hapo juu, mhusika hakuwasaidia maskini kwa kuwa hakuwa tajiri.

Kuhusu –ngali-, Mohammed (2001:167) anasema kuwa wanasarufi hao mapokeo walieleza kuwa mofu hii inaonyesha uwezekano ambao ungetekelezwa wakati uliopita ila haukufanyika, na kwa hivyo hakuna nafasi ya kutokea tena. Anaongeza kuwa mofu hiyo

inatofautiana tu na mofu {ngeli} kwa misingi kuwa {ngeli} inarejelea wakati wa kitambo sana. Mwanaisimu huyu haelekei kutoa hitimisho lake kuhusu viambishi hivi ila anatoa kauli kwamba;

> '...hali hii haiwiani kabisa na matumizi ya ya wasemaji wazawa wa Kiswahili.'

Katika kazi hii, sisi tunakubaliana na Zawawi (1971), Waihiga (1999:124-5 na Iribeh (2008) wanapoeleza kuwa viambishi hivi vina uamilifu sawa na kwamba huvijikiti katika wakati mahususi; vinaweza kuwa na maana ya wakati uliopita, uliopo au hata kuonyesha matamanio ya msemaji kuhusu baadaye kama inavyodhihirika katika sentensi zifuatazo.

32. a) Ni**nge**kuwa na mabawa ningeruka.

    b) Ni**ngali**kuwa na mabawa ningaliruka.

    c) Ni**ngeli**kuwa na mabawa ningeliruka.

Tunasadiki kuwa maelezo potoshi kuwa mofu {ngali} na {ngeli} yanachochewa na hali ya kuzingatia 'li' katika mofu hizo mbili. Wanaoyatoa maelezo hayo wanaelekea kudhani kuwa 'li' ni kiambishi cha njeo iliyopita. Ukweli wa mambo ni kuwa mofu hizo hazistahili kuvunjwa kama wanavyoelekea kufanya. Jambo muhimu katika matumizi ya mojawapo ya viambishi hivi vitatu ni kuwa hutokea kila kimoja katika upekee wake katika sentensi, wala havitumiwi viwili tofauti.

2.2.1.8. Kiambishi Kirejeshi

Kiambishi kirejeshi ni kiambishi cha pekee pamoja na kiambishi cha mahali katika kitenzi cha Kiswahili kinachotokea ama kabla au baada ya mzizi. Kiambishi hiki huwa na uamilifu wa kurejelea nomino au kiwakilishi kilichodokezwa awali. Kiambishi kirejeshi huchukua maumbo tofautitofauti kutegemea ngeli ya nomino husika. Zingatia mifano:

33. i) Ngeli ya A-WA

    a) Umoja: Mtoto ali**ye**sifiwa ni mwema.

    b) Wingi: Watoto waliosifiwa ni wema.

ii) Ngeli ya U-I

a) Umoja: Mlango ulioundwa utavunjwa.

b) Wingi: Milango iliyoundwa itavunjwa.

iii) Ngeli ya LI-YA

a) Umoja: Jino linalouma litang'olewa.

b) Wingi: Meno yanayouma yatang'olewa.

Ni bayana kutokana na mifano hii kwamba, mofu ya urejeshi huundwa kwa kipatanishi ngeli cha nomino husika na mofu {o} ya urejeshi. Yaani kila ngeli huchochea maumbo tofautitofauti ya kiambishi cha urejeshi.

2.2.1.9. Viambishi vya yambwa/shamirisho

Kama tulivyoeleza awali, mofu za yambwa huwakilisha mtu au kitu kinachopata athari ya kitendo. Kwa mfano,

34. Niliiramba asali.

Katika sentensi hii, asali ni yambwa kwa kuwa ndiyo inaathiriwa moja kwa moja na kitendo cha kurambwa. Katika kitenzi 'niliiramba' kiambishi kilichokolezwa wimo ni cha yambwa. Hii ni yambwa tendwa/ shamirisho kipozi.

Kitenzi elekezi cha Kiswahili sanifu pia huweza kuchukua mofu ya yambwa tendewa. Hii ni yambwa inayopokea manufaa au madhara ya kitendo kinachoakisiwa katika kitenzi. Yambwa tendwa aghalabu huwa mtu au mnyama aliye na uwezo wa kutendewa jambo. Mathalani, katika sentensi:

35. a) Alimnunulia zawadi.

Kiambishi -m- kinaakisi mtu anayepokea manufaa ya kitendo. Hii ni yambwa tendewa/shamirisho kitondo.

Utafiti huu unabainisha kuwa mofu ya yambwa tendwa na tendewa idhihirikayo kabla ya mzizi wa kitenzi huwa na mofimu mbalimbali ambazo zinaelekezwa na viambishi vya kauli. Tathmini mifano:

35. b) Nili**m**somesha Kifaransa.

c) Nili**m**someshea mwanawe Kifaransa.

Katika mfano wa 35 b), ni dhahiri kuwa mofu iliyokolezwa {m} inamrejelea mtu ambaye ametendeshwa kitendo cha kusoma. Mtu huyo, kwa hivyo, amepokea manufaa ya kitendo sio kwa kutendwa, bali kwa kutendeshwa, yaani amesomeshwa.

Mofu {m} katika mfano wa 34 c) nayo kwa upande mwingine inadokeza mtu anayepokea manufaa kwa kutendeshewa. Kwa sababu hiyo mofu hii inasetiri maana ya mtendeshewa.

2.2.1.10. Kiambishi cha Mrejeo sabaki

Kiambishi cha mrejeo sabaki huwakilisha mofimu –ji- ya anayepokea athari ya kitendo ambaye pia ndiye mtendaji. Kiambishi hiki kwa hivyo huonyesha kuwa kitendo kimempata *mtu binafsi aliyekitenda; ama kwa hiari, lazima au kwa ajali.* Kwa mfano,

36. a) Mwashigadi ali**ji**salia kadamnasi.

b) Wenyeji wa hapa hu**ji**pikia kila siku.

2.2.1.11. Kiambishi cha Namna

Utafiti wetu unabainisha kiambishi cha namna ambacho huonyesha kitendo kilitokea kwa jinsi gani. Watafiti wa awali hawajakibainisha bali wanaangazia kiambishi cha urejeshi 'o' tu. Kiambishi hiki ni –vyo- na ni tofauti na kiambishi cha urejeshi katika ngeli ya KI-VI , vyo- kwa kuwa hiki hakionyeshi urejeshi. Zingatia sentensi:

37. Wakenya walifurahia ali**vyo**cheza.

Mofu iliyokolezwa wino inaonyesha jinsi mhusika alivyoufanya mchezo wake.

2.2.1.12. Kiambishi tupu cha muala

Utafiti huu unaainisha kiambishi tupu cha muala. Kiambishi hiki hutokea katika vitenzi vya silabi moja katika kauli ya kutenda, njeo iliyopita, iliyopo na ijayo[3]. Kiambishi hiki ni –ku- na huweza kuleta mwala katika kitenzi cha silabi moja kiasi kwamba kitenzi hicho kinakuwa na maana. Kiambishi hiki hutokea punde kabla ya mzizi wa kitenzi. Tunalinganisha vitenzi vya silabi moja vyenye mofu tupu ya muala na vitenzi vinginevyo ili kuthibitisha umuhimu wa kiambishi hiki:

38. i) Vitenzi vya silabi moja.

a) Ali**ku**la wali.

*Alila wali.

b) Mvua ina**ku**nya sasa.

* Mvua inanya sasa.

c) Viumbe vyote vyenye uhai vita**ku**fa.

*Viumbe vyote vyenye uhai vitafa.

38. ii) Vitenzi vinginevyo

a) Yeye alienda chuoni.

b) Mwajuma anaandika tamthilia nzuri.

c) Wakenya watapenda amani.

Katika mifano hii inabainika kwamba kiambishi tupu cha muala kina umuhimu mkubwa sana katika kitenzi cha silabi moja kwa kuwa hukifanya kitenzi husika kuwa na mantiki. Kiambishi hicho, hata hivyo, hakitokei katika vitenzi vinginevyo.

2.2.2.13. Viambishi vya mahali na wakati

Viambishi vya mahali ni –po-, -ko- na –mo- na vina alomofu {pa}, {ku} na {mu}, na huwakilisha mahali dhahiri, mahali kusiko dhahiri na mahali ndani mtawalia. Viambishi vya

mahali huwezesha kujua mahali ambapo kitendo kilitokea, kinatokea au kitakamotokea. Zingatia sentensi;

39. a) Wanapopitia panavutia. (mahali dhahiri).

b) Alikoenda kuna miti mingi. (mahali kusiko dhahiri).

c) Nilimotayarisha mlikuwa na siafu. (mahali ndani).

Viambishi hivi vya mahali vinapotumiwa katika sentensi, huweza kuchukuana na viambishi vya ngeli ili kutimiza upatanifu wa kisarufi.

Mofimu ya wakati hudokezwa kwa kiambishi –po-. Kiambishi hiki hutangulia mzizi na huonyesha wakati ambapo tendo lilitokea, linapotokea au litakapotokea. Kiambishi hiki huonyesha wakati maalum wa kitendo husika. Mathalani,

39. c) Lilipobingiria halingewza kuokolewa.

d) Alipompenda Rosa alimchumbia.

## 2.6. VIAMBISHI TAMATI

Viambishi hivi huambishwa katika mzizi, upande wa kulia. Viambishi hivi pia huitwa viambishi vifuatilizi na ni vichache vikilinganshwa na viambishi awali. Tutajadili aina tofautitofauti za viambishi tamati hapa chini. Mzizi unapofungamanishwa na viambishi tamati huwa tunapata shina (Katamba 1993:145 na Mgullu 1999:199).

Viambishi tamati huwa tofauti katika vitenzi vya Kiswahili sanifu kutegemea asili ya vitenzi hivyo (kama ni vya asili ya Kibantu au vya mkopo) au dhamira ya sentensi. Fauka ya hayo, hali ya kitenzi; yakinishi au kanushi huathiri viambishi vyake tamati. Tutajadili viambishi hivyo hapa chini.

### 2.2.2.1. Kiishio

Vitenzi vya asili ya Kibantu huchukua mofu {a} ya kiishio katika hali yakinishi katika kauli ya kutenda kama inavyodhihirika katika mifano ifuatayo:

40. Umoja | Wingi
--- | ---

| | |
|---|---|
| 40. Umoja | Wingi |
| a) Nilirukа. | Tuliruka. |
| b) Unapika. | Mnapika. |

2.2.2.2. Kiambishi tamati cha ukanushi

Kiambishi cha ukanushi katika vitenzi vya asili ya Kibantu ni –i- katika njeo iliyopo, umoja na wingi. Hata hivyo, katika njeo iliyopita na ijayo, ukanushi hudokezwa kwa mofu {a} lakini mofu za ukanushi {si}, {hu} na {ha} za awali zikasaidia kuelekeza kwamba sentensi husika zimo katika hali za ukanushi nafsi ya kwanza, ya pili na ya tatu mtawalia kama tulivyoonyesha hapo awali. Mifano yetu hapa chini itahusu njeo iliyopo;

i) Njeo iliyopo

| | |
|---|---|
| 41. Umoja | Wingi |
| a) Sichezi. | Hatuchezi. |
| b) Siandiki. | Hatuandiki |

2.2.2.3. Viambishi vya amri, rai na himizo

Amri hutolewa kwa mtu (au watu) aliye katika nafsi ya pili (msikilizaji). Sentensi ya amri aghalabu haina upole na kiimbo chake hupanda. Amri hutolewa kwa wakati uliopo ikikusudiwa kutekelezwa mara moja au muda mfupi kutoka wakati wa kutolewa. Katika vitenzi vya dhamira ombi/rai au himizo kiimbo hushuka kwa kuwa sentensi hizi, tofauti na zile za amri huwa na upole. Tofauti katika dhamira hizi tatu huonyeshwa kwa alama hisi (!) katika maandishi inayodokeza amri na alama ya kikomo (.) inayoonyesha rai au himizo. Katika vitenzi vya asili ya Kibantu, amri, rai na himizo huwakilishwa kwa mofu tamati {a} katika umoja, hali yakinishi na mofu {eni} katika wingi, hali yakinishi kama inavyodhihirika katika mifano ifuatayo:

| | |
|---|---|
| 42. Umoja | Wingi |
| a) Imba! | Imb**eni**! |

b) Cheza! Chez**eni**!

Katika hali kanushi, mofu ya amri huwa {e} katika umoja na wingi. Zingatia mifano:

43. Umoja Wingi

a) Usiende! Msiend**e**!

b) Usiruke! Msiruk**e**!

Katika vitenzi vya silabi moja, mofu ya amri katika umoja na wingi husalia {a} na {eni} katika hali yakinishi lakini mofu tupu ya mwala {ku} hutangulia mzizi kama inavyodhihirika katika mifano:

44. Umoja Wingi

a) Kunywa! Kuny**eni**!

b) Kuja! Kuj**eni**!

Hata hivyo mofu hii tupu ya mUala hudodoshwa katika ukanushi na badala yake kiambishi cha ukanushi –si- kikatiwa kabla ya mzizi, na mzizi ukafuatiwa na mofu ya amri kanushi {e} katika umoja na wingi. Tathmini:

45. Umoja Wingi

a) Usinywe! Msinyw**e**!

b) Usije! Msij**e**!

Katika vitenzi vya mkopo kiambishi cha amri katika wingi huwa –ni-. Tunapenda kukumbusha hapa kwamba vitenzi vya mkopo huwa na irabu 'e', 'u' au 'i' mwishoni ambazo ni sehemu ya mizizi wa vitenzi kama inavyojitokeza katika vitenzi: samehe, thubutu na sali. Katika umoja, maumbo ya vitenzi hivi husalia katika kauli ya kutenda isipokuwa kiimbo cha sauti hupanda. Zingatia mifano:

46. Umoja Wingi

a) Shiriki! Shiriki**ni**!

b) Thubutu! Thubutu**ni**!

c) Samehe! Sameheni!

2.2.2.3. Kiambishi Tamati cha Urejeshi

Kiambishi tamati cha urejeshi hurejelea kiima katika kitenzi cha Kiswahili. Kiambishi hiki hutokana na 'o' rejeshi na huchukua maumbo mbalimbali kutegemea ngeli ya nomino husika katika umoja na wingi. Kiambishi tamati cha urejeshi, tofauti na kile cha awali kinachoonyesha wakati maalum, huonyesha wakati usio maalum. Tathmini sentensi:

| 47. Umoja | Wingi | |
|---|---|---|
| a) Shamba anyakualo. | Mashambayo wanyakuayo. | (Ngeli ya LI-YA) |
| b) Mkono uumao | Mikono iumayo. | (Ngeli ya U-I) |
| c) Maktaba ipendezayo. | Maktaba zipendezazo. | (Ngeli ya I-ZI) |

2.2.2.5. Viambishi vya mahali na wakati

Mbali na kutokea kama viambishi awali, viambishi vya mahali na kile cha wakati hudhihirika pia kama viambishi tamati. Viambishi vya mahali huwakilishwa kwa mofu {po}, {ko} na {mo} zenye alomofu {pa}, {ku} na {mo} za mahali dhahiri, kusiko dhahiri na mahali ndani kama tulivyoeleza katika viambishi awali hapo awali. Mathalani:

48. (i) a) Aendapo pana amani.

b) Wapoteleako hakujulikani.

c) Waingiamo mna giza.

Mofu ya wakati huwakilishwa kwa {po} ambayo pia huonyesha wakati usio maalum. Zingatia mfano:

48. (ii). a) Yeye aingiapo humliza kila mtu nyumbani.

b) Watoto wachezapo hujipaka tope.

### 2.2.2.6. Kiambishi tamati cha namna

Kiambishi tamati cha namna ni –vyo- na huonyesha jinsi kitendo kinavyotokea, kitakavyotokea au kilivyotokea. Kama viambishi tamati vya mahali, urejeshi na wakati, kiambishi –vyo- tamati hudhihirisha wakati usio maalum. Zingatia:

49. a) Kwa namna achezavyo, atafunga bao.

b) Sipendi amwaminivyo mwanawe.

Katika mifano hii miwili, haijulikani kwa bayana endapo vitendo viwili husika hufanyika kila mara au vinafanyika tu wakati wa sasa kuendelea. Kwa sababu hiyo, kiambishi hiki kinadhihirisha njeo iliyopo na hali endelezi.

## 2.3. HITIMISHO

Katika sura hii, tumefafanua dhana za unyambuaji na uambishaji. Tumeonyesha kuwa unyambuaji ni utaratibu unaohusisha uundaji wa leksimu mpya ilhali uambishaji ni utaratibu wa kupachika mofu katika mzizi ili kupanua maana za neno fulani. Katika kufanya hili tumefafanua viambishi mbalimbali vya awali na tamati katika vitenzi na kuonyesha, kama wataalamu wa awali kwamba, Kiswahili ni lugha ambishi bainishi. Inabainika kwamba, viambishi awali ni vingi kuliko viambishi tamati.

Tofauti na tafiti za awali ambazo zimeainisha na kueleza kwa wingi viambishi tisa vya awali, utafiti wetu umeainisha na kufafanua viambishi kumi na tatu vya awali. Tumeonyesha kiambishi tupu cha muala na namna kinavyodhihirika. Utafiti wetu umeweka mipaka bayana kati ya viambishi virejeshi na vile vya namna, jambo ambalo, kadiri ya uelewa wa mtafiti huyu, halikuwa limeshughulikiwa kwa uketo tulioufanya.

Miongoni mwa kundi la viambishi hivi tamati ni viambishi vya kauli. Tunastahabu kuvifafanua kwa kina viambishi hivyo katika sura zifuatazo maadamu utafiti huu hasa unahusu kauli katika sentensi elekezi.

## 2.4. TANBIHI

1. Baadhi ya vitenzi vya mkopo, hasa vya asili ya Kiarabu vinaelekea kuwa na uwezo wa kuchukua viambishi ndani. Hali hii inatokana na uhalisi kuwa mizizi ya nomino ndiyo pia mizizi ya vitenzi. Tathmini; sujudu na sijida, hutubu na hatibu kisha thamini na thamani.

2. Kiswahili ni miongoni mwa lugha zinazoainishwa kuwa zilizo na uwezo wa sentensi kuwa bila kiima kinachodhihirika bayana na kwa hivyo kiima hicho huwakilishwa kama mofu funge za upatanisho katika vitenzi (Null subject languages) (Radford 1997).

3. Kiambishi tupu cha muala kama tafsiri ya 'metrically motivated empty affix' husaidia vitenzi vya silabi moja kudhihiri maana katika njeo iliyopo, iliyopita na ijayo, hali yakinishi.

# 3.0. SURA YA TATU: VITENZI NA KAULI KATIKA KISWAHILI SANIFU

## 3.1. UTANGULIZI

Katika sura hii, tutafafanua dhana ya vitenzi. Aidha tutaeleza kwa kina aina za vitenzi kwa misingi ya uamilifu, miundo na asili yake. Tutakusudia kuonyesha pia kwamba, kitenzi ndicho neno kuu katika sentensi kiasi kwamba sentensi ya Kiswahili kama lugha ambishi bainishi, yaweza kuwa ya neno moja tu ambalo ni kitenzi. Hatimaye tutafafanua aina mbalimbali za kauli katika muktadha wa sentensi elekezi ya Kiswahili sanifu. Katika kufanya hilo, tutaanza kwa kushughulia vitenzi vya asili ya Kibantu kabla ya kushughulika vile vya mkopo.

## 3.2. VITENZI VYA KISWAHILI SANIFU

Kitenzi ni kipashio kinachotoa taarifa kuhusu tendo linalofanyika, lililofanyika au litakalofanyika (Massamba 2004:38). Nao Richards et al (1985) wanaeleza kwamba,

> 'Kitenzi ni neno ambalo hutokea kama sehemu kuu ya kiarifu na ambalo huambishwa mofu za njeo, nafsi, idadi na dhamira. Fauka ya hayo, vitenzi hutoa habari kuhusu tendo na hali' (TY).

Fasili hii inakaribiana sana na ya Cystal (2003:490-1) ambaye anasema kuwa 'kitenzi ni kipashio kinachodhihirisha uwezo wa kimofolojia wa kuambishwa mofu za upatanisho, njeo, hali, idadi, na nafsi.'

Kiuamilifu, kitenzi ni kipashio ambacho, kwa upekee wake au kwa pamoja na vitenzi vingine, hutumiwa kama kiarifu cha sentensi na huweza kuandamana na kiima.

Kulingana na fasili hizo hapo juu, inabainika kwamba vitenzi ni maneno yanayotoa habari kuhusu matendo ya watu, wanyama au vitu. Mathalani:

50. a) Juma **anaandika** barua.
    b) Gari **lilibingiria.**

Katika mifano miwili ya sentensi hapo juu, maneno 'andika'na'bingiria' ndiyo vitenzi. Huku tukikubaliana kwa kiasi fulani na maelezo haya, tunatambua kwamba yana upungufu kwa kuwa, mbali na kuarifu kuhusu matendo, vitenzi kwa jumla hutoa taarifa kuhusu kiima cha sentensi. Baadhi ya habari zinazoweza kusetiriwa katika kitenzi ni pamoja na:

i. Hali ya kuwa au kutokuwa na kitu. Katika mkabala huu, kitenzi huonyesha nomino ni au si ya nani. Kwa mfano;

| | |
|---|---|
| 51. Hali yakinishi | Hali kanushi |
| a) Kenya **ina** mafuta. | Kenya **haina** mafuta. |
| b) Mimi **nina** subira. | Mimi **sina** subira. |

i) Hali ya kuwa au kutokuwa mahali fulani. Katika matumizi haya, kitenzi huarifu kuhusu kuwepo au kutokuwepo kwa nomino mahali fulani katika kipindi fulani cha wakati. Tathmini sentensi;

| | |
|---|---|
| 52. Hali yakinishi. | Hali kanushi |
| a) Maua **yamo** sebuleni. | Maua **hayamo** sebuleni. |
| b) Mkulima **yu** shambani. | Mkulima **hayumo** shambani. |

ii) Wakati wa tukio. Kitenzi pia huarifu kuhusu wakati ambapo jambo fulani lilitukia au lilikosa kutukia. Kama tulivyoonyesha katika sura ya pili, wakati hudhihirika katika njeo tatu: iliyopita, iliyopo na ijayo. Kupitia kwa mofu za njeo katika kitenzi, habari kuhusu wakati hubainika kama inavyojitokeza katika mifano:

| | |
|---|---|
| 53. Hali yakinishi. | Hali kanushi |
| a) Wakenya wa**ta**piga kura. | Wakenya hawa**ta**piga kura. |
| b) Mandela a**li**pigania uhuru. | Mandela ha**ku**pigania uhuru. |

iii) Cheo/kazi/taaluma/hadhi ya mtu au kitu. Kitenzi hutoa taarifa kuhusu kazi anayoifanya au asiyoifanya mtu, cheo chake au taaluma yake au taaluma isiyo yake. Tathmini mifano:

| | | |
|---|---|---|
| 54. Hali yakinishi | Hali kanushi | |
| a) Oukot **ni** wakili. | Oukot **si** wakili. | (taaluma). |
| b) Elizabeth **ni** malkia. | Elizabeth **si** malkia. | (hadhi). |
| c) Kaurenje **ni** meneja wa mauzo. | Kaurenje **si** meneja wa mauzo. | (cheo). |

iv) Sifa za mtu/kitu au zisizo za mtu/kitu. Kupitia kwa vitenzi habari kuhusu wasifu wa mtu au kitu fulani hujitokeza. Habari hizo hujitokeza vyema kupitia kwa vitenzi vishirikishi. Mathalani;

55. Hali yakinishi. Hali kanushi

a) Yeye **ni** mvumilivu. Yeye **si** mvumilivu.

b) Kikosi hicho **kilikuwa** hodari. Kikosi hicho **hakikuwa** hodari.

Kwa jumla, sentensi ya Kiswahili sanifu huwa na viambajengo viwili vikuu. Viambajengo hivyo ni kiima na kiarifu. Kiima hutawaliwa na nomino au kiwakilishi ambacho habari zake hutolewa na kitenzi katika kiarifu. Kwa upande mwingine, kiarifu hubeba kitenzi ambacho huwasilisha wazo la sentensi. Hata hivyo, sentensi yaweza kuwa na kiarifu pekee kinachodhihirika. Kiarifu hicho, kulingana na Crystal (2003), kinaweza kuwa ni kitenzi peke yake kwa kuwa katika nadharia nyingi za sarufi, kitenzi ndicho kipashio muhimu zaidi katika sentensi. Hali hii hutokana na uhalisi kwamba kitenzi cha Kiswahili huweza kuambishwa mofu za ngeli na nafsi ambazo huwakilisha kiima. Kwa mfano:

56. a) Mhadhiri **anamsomesha** mwanafunzi.

b) **A**namsomesha mwanafunzi.

Ukweli wa mambo, hata hivyo, ni kwamba, fasili hii inajikita katika aina chache za vitenzi, na kwa hivyo kutozingatia aina nyingine, hasa vitenzi vishirikishi ambavyo huonyesha hali na havina uwezo wa kuambishwa mofu fulani kama vile za njeo, hali n.k. Kulingana nasi, kwa hivyo, fasili ya kitenzi inastahili kuzingatia hizo sifa sita tulizozibainisha hapo juu.

### 3.2.1. UAINISHAJI WA VITENZI (T)

Kama tulivyotanguliza hapo juu, kuna aina tofauti za vitenzi kwa kuzingatia miundo na uamilifu wake katika tungo. Kihore et al (2001:114) na Iribemwangi (2008) wanabainisha aina tatu za vitenzi; vitenzi vikuu, vitenzi visaidizi na vitenzi vishirikishi. Hat hivyo, wanakuwa wepesi wa kutaja kuwa uainishaji huo ni wa kisintaksia. Sisi katika tasnifu hii, tutaangazia kwa juujuu aina hizi za vitenzi. Hata hivyo, tutashughulikia pia vitenzi kwa misingi ya asili yake na miundo yake. Kwa jumla, hakuna mwafaka kuhusu uainishaji wa vitenzi hivi kwani idadi inatofautiana kutegemea mtafiti. Watafiti wengine kama vile Oichoe (2005) na Swaleh (2005) wanabainisha aina nne za vitenzi lakini kuna tofauti katika aina hizo. Sisi tutazingatia makundi hayo kisha tuongeze aina nyingine zaidi kwa misingi ya miundo, uamilifu na sifa zake za kisintaksia. Kwa hivyo tunaainisha vitenzi ifuatavyo:

1. Vitenzi Vikuu
2. Vitenzi Visaidizi

3. Vitenzi Vishirikishi
4. Vitenzi Visoukomo
5. Vitenzi Elekezi
6. Vitenzi Visoelekezi.

3.2.1.1. Vitenzi Vikuu

Kulingana na Mohammed (2001:80) Vitenzi vikuu ni vitenzi vinavyobeba maana leksika ya sentensi.Vitenzi hivi humsaidia msomaji au msikilizaji kuelewa mambo kadhaa kuhusu sentensi:

i) Mambo yanayotokea, yaliyotokea na yatakayotokea. Mathalan: Alikuja jana.
ii) Kauli ya sentensi; kama ni ya kutendwa, tendewa n.k. Mathalani; Kiti kimevunjwa.
iii) Kiimbo cha sentensi; ya taarifa, swali, mshangao, amri au rai. Kwa mfano: Niongezee tafadhali.

Vitenzi vikuu hutusaidia kuelewa mambo, ama yanayofanywa na kiima, au yanayofanyiwa kiima.Vitenzi vikuu huweza kutokea pekee katika sentensi au vikatanguliwa na kitenzi au vitenzi kisaidizi (visaidizi). Tathmini:

57. a) Shabesh **atausomea** umma hotuba yake.
    b) Kemboi alikuwa **anakimbia** uwanjani.
    c) Tunapaswa kwenda **kuunda** vinyago.

Katika mifano hii hapa juu, maneno yaliyokolezwa wino ni vitenzi vikuu. Katika mfano wa kwanza, kitenzi kikuu kinajitokeza pekee lakini katika mfano wa pili na wa tatu, vitenzi vikuu vinatanguliwa na kitenzi kisaidizi kimoja na viwili mtawalia.

Kama tulivyoonyesha katika sura ya pili, vitenzi vikuu vina uwezo mkubwa wa kuambishwa mofu mbalimbali zenye uamilifu mbalimbali wa kisarufi, zikiwemo mofu za kauli. Ni kutokana na uwezo huu wa kuchukua viambishi tofautitofauti ambapo wataalam kama vile Ireri (1985) na Iribemwangi (2008:119) wanahitimisha kuwa kitenzi cha Kiswahili huwa na muundo changamano.

Utafiti huu unatoa sifa nyingine ya vitenzi vikuu mbali na sifa tulizofafanua hapo juu: vitenzi vikuu huweza huambishwa mofu za kauli. Sifa hii ni bainifu kwa kuwa vitenzi visaidizi na

vitenzi vishirikishi havina uwezo huu wa kuchukua viambishi vya kauli. Tutatoa mifano hapa wa vitenzi vikuu na kuonyesha sifa hii;

58. a) Mulama **alicheza** mpira. (kauli ya kutenda)
    b) Mulama **alituchezea** mpira. (kauli ya kutendea)
    c) Mulama na Wingu **walichezeana** mpira. (kauli ya kutendeana).

Yamkini mbali na kusetiri wazo kuu katika sentensi, sifa hii ni muhimu katika kutofautisha vitenzi vikuu na vile vingine katika lugha ya Kiswahili.

3.2.1.2. Vitenzi Visaidizi (Ts)

Vitenzi visaidizi ni vitenzi ambavyo uamilifu wake ni kusaidia kitenzi kikuu kukamilisha uarifu wake (Massamba (2004:38). Ufasiri huu una maana kwamba vitenzi visaidizi hutokea katika muktadha wa vitenzi sambamba katika sentensi ambapo vitenzi hivi visaidizi hutangulia vitenzi vikuu. Kwa mfano;

59. a) Mtoto **alitaka** kuchezea puto.
    b) Wao **wangali** wanajiandaa kwa mashindano.

Tofauti na vitenzi vikuu, vitenzi visaidizi havina uwezo wa kuchukua viambishi vya kauli, na havitokei pweke katika sentensi. Vitenzi visaidizi vina uamilifu wa aina tofautitofauti kulingana na (Mohammed 2001):

i). Huonyesha njeo.

Vitenzi visaidizi husaidia kuelewa kama tendo la sentensi linahusu njeo ya sasa, iliyopita au ijayo, kwa mfano:

60. a) Teresia **alikuwa** akipalilia maua.
    b) Wavinya **atapata** kuwakilisha eneo bunge hilo.
    c) Wakenya **wanapaswa** kuheshimu uamuzi wa mahakama.

ii). Huonyesha hali ya sentensi.

Vitenzi hivi husaidia kuonyesha kama sentensi imo katika hali yakinishi au kanushi. Mathalani:

61. a) Mimi **ninaweza** kuimba wimbo wa taifa la Tanzania. (hali yakinishi)

b) Viongozi wa Afrika **hawastahili** kutawala nchi zao kwa mabavu. (hali kanushi)

iii. Husaidia kutunga sentensi sahihi.

Hali hii hutokea wakati vitenzi visaidizi hutumiwa katika mazingira kabla ya vitenzi visoukomo. Endapo kitenzi kisaidizi hakikutangulia kitenzi kisoukomo, basi sentensi husika haiwi sahihi. Tathmini mifano:

57. a) Seremala **hakuweza** kuzipiga mbao zake msasa.

*Seremala kuzipiga mbao zake msasa.

b) Mkulima huyu **amewahi** kutuzwa na rais.

*Mkulima huyu kutuzwa na rais.

Vitenzi Visaidizi vya Kiswahili sanifu ni vichache. Tutaorodhesha mifano ifuatayo ambayo pia tutaitungia sentensi kudhihirisha matumizi yake:

i) Kwisha: Nimekwisha amua kwamba Misri sirudi tena.
ii) Pasa: Watu wanapasa kuishi kwa amani.
iii) Stahili: Mwaibale alistahili kujua kwamba ushirikina hauna nafasi katika karne ya ishirini na moja.
iv) Faa: Afaaye kubezwa ni mtu asiyetambua busara ya wazee.
v) Weza: Nchi hii inaweza kuwasaidia walemavu kikamilifu.
vi) Enda: Huenda kukanyesha alasiri.
vii) Taka: Baba alitaka wasome kwa bidii.
viii) Penda: Mrisho anapenda kutalii janibu za Afrika Mashariki.
ix) Ngali: Kiptoo angali anasomea Makerere.
x) Kuja: Tundor atakuja kunyakua tuzo ya mwanaspoti bora nchini.
xi) Wahi: Kila binadamu amewahi kuvunja sheria alizopewa Musa na Maulana.
xii) Pata: Nitapata kumshukuru kwa wema alionitendea juzi.
xiii) Kuwa: Wananchi wa Budalangi wamekuwa wakilalamikia mafuriko pindi kunyeshapo.

Kwa mujibu wa Baya (1993:32), kitenzi kisaidizi 'kuwa' ni aina maalum ya kitenzi kwa kuwa huweza kuchukua maumbo mbalimbali kutegemea njeo na hali. Wazo hili linabainika bayana tunapozingatia mifano ifuatayo;

62. a) Yeye **ni** mwerevu. (njeo iliyopo)

b) Yeye **alikuwa** mwerevu. (njeo iliyopita)

c) Yeye **si** mwerevu. (hali kanushi, njeo iliyopo)

d) Yeye **hakuwa** mwerevu. (hali kanushi, njeo ijayo)

e) Mmojs wetu **atakuwa** mkurugenzi mkuu. (njeo ijayo)

Hata hivyo, sisi hatukubaliani na maelezo haya kwani mtafiti huyu haweki mipaka dhahiri kati ya vitenzi vishirikishi na vile visaidizi. Kama tutakavyoonyesha hapa chini, mifano hii inastahili kuwa ya vitenzi vishirikishi wala sio ya vitenzi visaidizi. Hali hii inatilia mkazo wazo letu kuwa uainishaji wa vitenzi haustahili kuzingatia miundo yake pekee bali pia sifa zake za kisintaksia na etimolojia yake.

Katika sentensi kanushi, Ts ndivyo hukanushwa na wala sio vile T ambavyo husalia katika hali yakinishi. Zingatia mifano;

63. a) Mwanariadha **hakuweza** kunyakua dhahabu.

b) Amani **haistahili** kuvurugwa.

3.2.1.3. Vitenzi Vishirikishi (t)

Vitenzi vishirikishi hushirikisha vitu kihali, kitabia na kimazingira katika sentensi (Waihiga 1999). Vitenzi hivi havionyeshi matendo bali mahusiano ya nomino na hali, tabia au mazingira fulani. Vitenzi vishirikishi huwa havina uarifishaji mkamilifu. Tofauti na vitenzi vikuu, hivi haviwezi kutokea katika sentensi katika upekee wake. Kwa sababu hiyo, vitenzi hivi hufuatiwa na vijalizo ili kufanikisha uarifishaji huo. Vijalizo hivyo ni kama nomino, vivumishi na vielezi. Tathmini mifano ifuatayo:

64. a) Mwanasiasa huyu **ni** mwongo.

b) Jembe **lilikuwa** kitaluni.

c) Philemon **si** mwalimu.

Katika mifano hii mitatu, maneno mwongo, kitaluni na mwalimu ni vijalizo: kivumishi, kielezi na nomino mtawalia na yanatanguliwa na vitenzi vishirikishi.

Kutokana na mifano hiyo mitatu, inabainika pia kwamba kuna aina mbili kuu za vitenzi vishirikishi: vitenzi vishirikishi vikamilifu na vipungufu.

3.2.2.3.1. Vitenzi Vishirikishi Vikamilifu

Vitenzi vishirikishi vikamilifu huweza kuambishwa mofu za nafsi, njeo na hali (Waihiga 1999). Huku tukikubaliana na maelezo haya, tunaongeza kuwa vitenzi vishirikishi vikamilifu huambishwa mofu za ngeli na za ukanusho. Aidha vitenzi hivi ndivyo hudhihirika kama vitenzi visaidizi vinapotokea katika usambamba na vitenzi vikuu. Hali hii, kama tulivyodokeza hapo juu, inatokana na uhalisi kuwa **t** hufuatiwa na kijalizo. Zingatia mifano:

65. a) Mgonjwa **angali** hali mahututi.
    b) Mkulima **alikuwa** shambani kutwa nzima.
    c) Wanaofuzu **wanastahili** shukrani za dhati.

Kama inavyobainika katika mfano (b) hapo juu, baadhi ya vitenzi vishirikishi vikamilifu hutokana na vitenzi t vipungufu (tutavifafanua hapa chini). Muundo wa ndani wa kitenzi 'kuwa' ni 'ni' na kwa hivyo hubadilika umbo kutegemea njeo.Kulingana na Baya (1993:32-3), kitenzi cha 'kuwa' ni aina maalum ya kitenzi ambacho kinaweza kujitokeza kwa sura tofautitofauti. Sura hizi ni; 'kuwa' 'ni', 'si' na 'ndio'. Huku tukikubaliana na maelezo haya kuhusu sura tofautitofauti za kitenzi hicho, tunatofautiana naye kwamba hizo sura ni vitenzi visaidizi. Kulingana nasi, hivyo ni vitenzi vishirikishi vipungufu kama tulivyotaja awali.

Isitoshe vitenzi **t** vikamilifu hudhihirika katika mazingira ambamo havitangulii vitenzi vikuu bali vinatangulia nomino, vivumishi au vielezi.

3.2.1.2. Vitenzi Vishirikishi Vipungufu

Hivi ni vitenzi ambavyo huweza kuambishwa mofu za nafsi na ngeli na idadi. Vitenzi hivi pia huonyesha dhana yakinishi na kanushi. Hata hivyo, kama t vikamilifu, haviwezi kutokea pekee katika sentensi; sharti vifuatiwe na vijalizo. Kama tulivyodokeza hapo juu, baadhi ya t

vipungufu hutokana na vitenzi vishirikishi vikamilifu. Mifano ya vitenzi vishirikishi vipungufu ni pamoja na:

66. a) Kitabu **ki** mezani.
    b) Mimi **ndimi** mla mamba.
    c) Mvuvi **yu** ufuoni.

Mifano zaidi ya vitenzi hivi ni; ni, tu, wa, u, -mo, -ko, si n.k. Waihiga (1999) anahitimisha kuwa t vipungufu vina uamilifu wa kisintaksia na kisemantiki katika kufanikisha mawasiliano katika lugha ya Kiswahili.

3.2.1.4. Vitenzi Elekezi

Kitenzi elekezi ni kitenzi ambacho (kimantiki) kila mara kinaendana na yambwa, k.m, vitenzi piga, nunua, safisha, kata, n.k. (Massamba 2004:38).

Kulingana na fasili hii, kitenzi elekezi sharti kifuatiwe na yambwa, ama tendwa au tendewa au hata yambwa zote mbili kwa pamoja.Tutafafanua hili kwa kutathmini mifano;

67. a) Poghisio **alisikia** ukwenzi.
    b) Waumini **walisomewa** Kuran tukufu.
    c) Kenya **ilijinyakulia** uhuru.

Katika mifano hii, vitenzi vyote ni elekezi kwa kuwa vinafuatiwa na yambwa.

Habwe na Karanja (2004:175) wanaongeza kuwa:

> '... aina hizi za vitenzi huashiria kitendo na hali ambayo huruka mipaka na kuathiri maneno mengine ya sentensi'.

Hata hivyo, wataalam hawa wanasema pia kwamba, kuna mjadala kuhusu kuwepo au kutokuwepo kwa vitenzi elekezi katika lugha Kiswahili. Kuhusu madai haya, sisi tunaunga mkono mawazo ya Mohamed (1996) kuwa baadhi ya vitenzi vya Kiswahili sharti vifuatiwe na yambwa. Endapo hilo halikutokea, vitenzi hivyo huchochea maswali miongoni mwa wasikilizaji. Kwa mfano katika mifano hiyo hapo juu, bila maneno 'ukwenzi', Kuran' na 'uhuru', msikilizaji atajiuliza, alisikia nini? Walisomewa nini? Na ilijinyakulia nini?

3.2.1.5. Vitenzi Visoelekezi

Vitenzi visoelekezi havihitaji yambwa; hukamilika kimatumizi. Hata hivyo, vitenzi hivi hufuatiwa na vielezi au virai vielezi (Oichoe 2005:75). Inaeleweka kwamba, baadhi ya vitenzi katika lugha hueleweka bila kuongeza yambwa kwani kuongeza huko hufanya sentensi kukosa mantiki. Zingatia

68. a) Waliopata ajali walikufa.

*Waliopata ajali walikufa kifo.

b) Mtoto analia .

*Mtoto analia kilio.

c) Bakari alioa.

*Bakari alioa mke.

Katika mifano hii, ni wazi kuwa maneno kifo, kilio na mke hayana umuhimu katika sentensi husika[1]. Yaelekea kwamba vitenzi visoelekezi huathiri yambwa ambayo ni bayana katika lugha na kwa hivyo kuirudia katika sentensi ni kuifanya iwe na makosa kwani ni kuongeza urudiaji usiofaa.

3.2.1.6. Vitenzi Visoukomo

Vitenzi visoukomo hudokezwa kwa kiambishi awali 'ku-'. Vitenzi hivi huwa na muundo wa nomino za vitenzi-jina. Hata hivyo, vinakuwa vitenzi pale vinapokuwa na uamilifu wa kuarifu. Vitenzi hivi huchukua viambishi vya kauli na huweza kutanguliwa na vitenzi visaidizi (Swaleh 2005:80). Mathalani;

69. a) Yeli anataka **kutuchezea** kinubi.

b) Majirani hawa hupata **kulimishiana** mashamba.

Huku tukikubaliana na Swaleh kwa kiasi fulani, tunatofautiana naye kwa kauli kuwa vitenzi visoukomo huchukua yambwa. Tunasadiki kuwa vitenzi hivi sio lazima vichukue yambwa, kwa hivyo vinaweza au vikakosa kuwa elekezi kutegemea muktadha wa matumizi. Zingatia mifano:

70. a) Makeba alipenda **kuimba** wimbo wa Kizulu. (elekezi)

b) Yatima huyu aliwahi **kustarehe**. (soelekezi)

Baada ya kuangazia aina hizo za vitenzi, tunastahabu kutaja kwamba vitenzi vya Kiswahili huainishwa katika makundi mawili kutegemea asili:

1. Vitenzi vya asili ya Kibantu, na
2. Vitenzi vya asili ya kigeni.

Vitenzi vya asili ya Kibantu huwa ni msamiati asilia wa Kibantu. Sifa kuu ya vitenzi hivi ni kuwa huwa na kiishio 'a'. Mathalan;

Imba, cheza, ruka, ogopa, piga n.k

Vitenzi vya asili ya kigeni kwa kawaida hukopwa kutoka kwa lugha za kigeni kama vile Kiajemi, Kihindi, Kiingereza, na hasa Kiarabu miongoni mwa lugha nyinginezo zinazopata kutagusana na Kiswahili[1]. Sifa bainifu ya vitenzi vya mkopo ni kuwa huisha kwa viishio 'i', 'e' au 'u'. Zingatia mifano'

| 71. | Kiishio 'i' | Kiishio 'e' | Kiishio 'u' |
|---|---|---|---|
| | i) Shiriki | samehe | thubutu |
| | ii) Safari | starehe | haribu |
| | iii) Sali | balehe | dhulumu |

Ijapokuwa utaratibu wa viishio hutumiwa kama kigezo cha kuainisha vitenzi, tunakubaliana na kauli ya Ireri (1985) kwamba kigezo hicho sio jumuishi kwa kuwa kuna vitenzi vingine vya mkopo ambavyo huwa na kiishio 'a' kama vitenzi vya asili ya kibantu. Mifano ya vitenzi hivyo ni nuia, shiba, duwaa, rejea n.k.

Mbali na uainishaji huu, tunatambua kwamba lugha ya Kiswahili ina vitenzi vingine vinavyoainishwa kama vya silabi moja. Vitenzi hivi ni maalum katika Kiswahili hasa tunapozingatia uambishaji wa mofu za kauli. Mgullu (1999:207) anatambua vitenzi hivi ila mifano anayoitoa inapotosha kwani ni ya vitenzi vya silbi mbili. Anaorodhesha vitenzi zaa, kaa, vaa, tia na zoa.

Vitenzi vya silabi moja ni kumi kwa idadi na ni vifuatavyo;

fa, wa, cha, chwa, ja, la, pa, pwa, nya na nywa. Sifa nyingine inayovibainisha vitenzi hivi ni matumizi ya kiambishi tupu cha muala hasa vitenzi hivyo vinapotumiwa katika njeo iliyopita, iliyopo na ijayo katika hali yakinishi. Mathalani;

72. a) Maji ya bahari yataku**pw**a saa mbili asubuhi.

b) Mtoto aliku**l**a chakula kibovu.

c) Mzee Savalanga aliku**f**a kwa ugonjwa usiojulikana.

d) Mvua inaku**ny**a sasa.

Katika mifano hii michache, sehemu iliyokolezwa wino ndiyo mzizi wa kitenzi husika na ikiambatanishwa na irabu fuatilizi inakuwa ni silabi moja.

## 3.3.0. KAULI ZA VITENZI

Massamba (2004:26) anaeleza kauli kama 'kategoria mojawapo katika ufafanuzi wa sentensi au kishazi, ambayo hasa huhusu kitenzi, na hutumiwa kuonyesha jinsi sentensi zinavyoweza kubadili uhusiano uliopo baina ya kiima na yambwa pasi na kubadili maana ya sentensi.'

Kama inavyobainika katika maelezo haya, kitenzi cha Kiswahili sanifu kinaweza kuambishwa mofimu ambalimbali za kauli ambazo huibua maana tofautitofauti ila zilizoegemezwa katika maana ya kimsingi inayosetiriwa katika mzizi wa kitenzi husika. Aidha, mofu za kauli ni viambishi tamati; hutokea baada ya mzizi kama tulivyoeleza katika sura ya pili.

Tunapenda kukumbusha kama tulivyoeleza awali katika 2.1.3.4 kuwa mofu za kauli hazibadilishi neno kutoka katika aina moja hadi nyingine kama vile zile za unyambuaji. Uambishaji wa mofu za kauli pia huhusisha vitenzi tu wala sio aina nyinginezo za maneno ya Kiswahili. Uambishaji wa mofu za kauli katika mizizi ya vitenzi katika lugha ambishi bainishi, kama Kiswahili, huwa na uamilifu wa kisemantiki wa kuongeza au kupanua maana msingi ya mzizi (Oichoe 2005:112 na Abdulaziz 1996:47).

Kulingana na Katamba (1993:45) na Ilongo (1983), kabla ya kutia viambishi vya kauli, kitenzi husemekana kuwa katika hali yake ya msingi. Hali hii huwa katika kauli ya kutenda na ndiyo hali ambapo vitenzi hudhihirika kama leksimu. Vitenzi vya asili ya Kibantu huisha kwa irabu 'a' ilhali vile vya asili ya mkopo, kwa jumla, huisha kwa viishio: 'i', 'e' au 'u' katika hali hii ya msingi. Mathalani;

73. a) Soma

b) Starehe

c) Shiriki

d) Tubu

Utaratibu wa kuambisha mofimu za kauli huweza kuenda zaidi ya hatua mbili, huku kila kiambishi cha kauli kikizua maana panuzi ya kitenzi. Zingatia mfano;

74. a) Mkulima anamlim-**i**-a mwenzake shamba.

b) Wakulima wanalim-**i-an**-a mashamba.

c) Somo hawa hulim-**ish-i-an**-a mashamba yao.

d) Mkupa alilim-**ish-i-w**-a shamba.

Uambishaji wa mofu za kauli hufanyika kwa kuzingatia kanuni ya utangamano wa irabu. Katika kanuni hii, irabu inayopatikana katika mzizi huweza kuelekeza irabu ya kauli itakayotumiwa. Kwa mfano, endapo mzizi wa kitenzi una mojawapo wa irabu kaze /i/, /a/ au /u/, mofu ya kauli huwa 'i'. Wakati uo huo, endapo mzizi wa kitenzi una mojawapo ya irabu za kati /e/ au /o/, mofu ya kauli huwa 'e'. Zingatia mifano ifuatayo:

75. a) Kiplagat aliir**u**ki**a** Kenya viunzi katika mashidano ya Olimpiki.

b) Salome na Kibwana walif**a**nyi**a**na utani.

c) Mzazi mwema hums**o**m**e**a mwanawe hadithi kabla ya kulala.

d) Wapenzi hawa huch**e**k**e**ana kadamnasi.

Katika mifano sentensi (a) na (b) hapo juu, ni bayana kwamba irabu 'u' na 'a' zipatikanazo katika mzizi huchochea kudhihirika mofu {i} ya kauli. Vivyo hivyo, katika sentensi (c) na (d) irabu za mizizi ya vitenzi 'o' na 'e' inaelekeza kudhihirika kwa kiambishi cha kauli ambacho huwa ni irabu ya kati /e/ (Iribemwangi 2008, Ireri 1985, Maringah 1987 na Mohamed 2001).

Huku tukikubaliana na mahitimisho ya hawa wataalam, tunapenda kutaja kwamba, mofu hizo za kauli huwa na alomofu hadi kufikia nne kutegemea mazingira mbalimbali ya kifonolojia ya irabu zinazohusika. Tutafafanua hali hii hapo mbele.

Kama tulivyodokeza hapo awali, kuna aina nyingi za kauli zinazodhihirika katika vitenzi na sentensi za Kiswahili sanifu. Sisi tutazingatia kauli zifuatazo kama zinavyodhihirika katika sentensi elekezi za Kiswahili:

1) Kauli ya kutendea

2) Kauli ya kutendewa

3) Kauli ya kutendwa

4) Kauli ya kutendana

5) Kauili ya kutendeana

6) Kauli ya kutendesha

7) Kauli ya kutendeshwa

8) Kuli ya kutendeshana

9) Kauli ya kutendesheana

10) Kauli ya kutendata

11) Kauli ya kutendua

### 3.3.1. KAULI KATIKA VITENZI VYA ASILI YA KIBANTU

#### 3.3.1.1. Kauli ya kutendea

Mofimu ya kauli ya kutendea huonyesha kuwa tendo linafanywa kwa manufaa ya mtu mwingine ambaye hudhihirika kama yambwa (Maringah 1987). Huku tukitambua maelezo haya, tunayaona kama yaliyo finyu. Hii ni kwa kuwa mofu hii huwa na maana zaidi ya nne (Mgullu 1999:207 na Habwe na Karanja 2004:109). Mbali na maana tuliyoitaja hapo juu, mofu hiyo yaweza kuwa na maana ya kutenda kwa niaba ya mtu, kutenda kwa kutumia kifaa au ala fulani na kutenda kuelekea sehemu au mtu fulani, kutenda mtendaji akiwa mahali fulani au hata kutenda kwa 'sababu ya'. Tutaonyesha hili kwa kuzingatia mifano ifuatayo:

76. a) Sussy alimwandikia Kadam barua.

Katika sentensi hii, mofu ya kauli {i} ina maana mbili. Maana ya kwanza ni kuwa Sussy aliiandika barua kwa manufaa ya Kadam; ujumbe uliokuwa katika barua ulinuia kumfaidi Kadam. Maana ya pili ya sentensi ni kuwa Sussy aliiandika barua kwa niaba ya Kadam.

Hapa, Kadam alistahili kuiandika barua lakini Sussy akatekeleza tendo hilo kwa niaba yake Kadam.Mofu hiyo ya kutendea inafafanuliwa zaidi katika mfano huu wa sentensi;

77. b) Kawira alimpigia Khavutsa mpira.

Kama sentensi 4. a) hapo juu, sentensi hii ina maana zaidi ya moja. Kwanza sentensi hii ina maana maana mbili zinazosetiriwa katika hiyo ya kwanza lakini pia ina maana kuwa mpira ulitumiwa kama ala au kifaa cha kumpiga Khavutsa. Nne, sentensi ina maana kwamba sababu ya Kawira kumpiga Khavutsa ilikuwa mpira. Yamkini Khavutsa aliupoteza au aliuharibu na Kawira akampiga kwa kuudhika naye. Hatimaye, sentensi hii ina maana kuwa Kawira aliupiga mpira kumwelekezea Khavutsa walipokuwa wanaucheza.

Mofu ya kauli ya kutendea ina alomofu ambazo huwa katika mgawanyo wa kiutoano. Mosi, mofu /i/ katika mazingira ambamo mzizi wa kitenzi huwa na mojawapo ya irabu kaze /i/, /a/ au/u/. Kwa mfano;

78. a) Alimlimia shamba.

b) Nitamrambia asali.

c) Walivukia mpaka sehemu ya chini.

Pili mofu {i} huwa na alomofu {e} katika mazingira ya mzizi wa kitenzi ulio na ama irabu 'e' au ''o' na kuisha kwa konsonanti. Mathalani,

78. d) Maimuna aliuchezea umma nataki.

e) Mzazi mwema humsomea mwanawe hadithi kila jioni.

Tatu, kauli ya kutendea hudhihirika kwa alomofu {li} au {le} katika mazingira mizizi ya vitenzi ambavyo huisha kwa irabu na kwa hivyo kuwa na shadda la irabu mwishoni. Kiambishi –li- hudhihirika katika hali ambapo mzizi wa kitenzi huwa na mojawapo ya irabu kaze 'i' 'a' na 'u, kisha mzizi huo umalizike kwa irabu. Mathalani;

79. a) Kijakazi alitufagilia nyumba.

b) Mtoto atawakimbilia wageni wafikapo.

Alomofu {le} nayo hutokea katika mazingira ya mzizi wa kitenzi wenye ama irabu 'e' au 'o' kisha ukaisha kwa irabu nyingine, kwa mfano;

80. a) Mama huyu alinilelea mwanangu nilipokuwa ziarani.

3.3.1.2.Kauli ya kutendewa

Vitenzi katika kauli ya kutendewa hutokana na vile vya kauli ya kutendea. Vitenzi katika kauli hii huwa na maana kuwa tendo linafanywa kwa manufaa au hasara za yule (au kile) anayetendewa. Aidha huonyesha kuwa tendo limefanywa kwa niaba ya anayefanyiwa, limefanyiwa mahali fulani au kuelekezwa mahali au kwa mtu fulani. Alomofu zinazowakilisha kauli hii ni {iw, ew, liw na lew}. Mofu {iw} hudhihirishwa katika vitenzi vyenye irabu moja mwishoni huku irabu ya mzizi ikiwa mojawapo ya irabu kaze: 'a', 'i' au 'u'. Kwa upande mwingine, mofu {ew} hubainika katika vitenzi vyenye kiishio irabu lakini ambacho mzizi wake huwa na irabu 'e' au 'o'. Kwa mfano;

81. a) Mwanafunzi ali**chezewa** zawadi.

b) Mimi nili**somewa** riwaya.

c) Rudisha ali**pigiwa** kengele.

d) Mnunuzi ali**pimiwa** nafaka kwa mizani.

Kama tulivyodokeza hapo juu, kiambishi cha kauli ya kutendea huwa –liw- endapo mziz una moja kati ya irabu kaze na inaaisha kwa shadda la irabu. Hali huwa tofauti endapo kitenzi kinaisha kwa shadda la irabu lakini mzizi wake uwe ama na irabu 'e' au 'o'. Alomofu ya kauli katika mazingira hayo huwa {lew}. Tathmini mifano ifuatayo'

82. a) Nita**tiliwa** sukari katika kinywaji changu.

b) Kariuki alipo**telewa** fahamu jana.

Jambo linalobainika katika mifano hii ni kuwa, sentensi ya kauli hii huanza kwa yambwa tendewa. Aidha mtendaji huwa ni kipashio kisichokuwa cha lazima katika sentensi maadamu tendo na yambwa tendewa ndivyo vipashio vinavyotiliwa mkazo.

3.3.1.3.Kauli ya Kutendwa.

Kauli ya ketendwa huwa na maana kuwa tendo linamwathiri mtu (kitu) Fulani. Kauli hii hudokezwa kwa kiyeyusho 'w'ambacho huwa na alomofu {liw} na {lew}. Kama katika kali tendewa, sentensi zizinazoakisi kutendwa hutanguliwa kwa yambwa tendwa na kwa hivyo, mkazo hutiwa kwa mwathiriwa na kitendo chenyewe. Alomofu {liw} na {lew} hudhihirika

katika mazingira ambamo vitenzi vinaisha kwa shadda la irabu na mizizi iwe na irabu kaze na zisizo kaze mtawalia. Tathmini mifano:

83. a) Hadimu amepig**wa** kalamu.

b) Ajuza atafagi**liwa** chumba na mjukuu wake.

3.3.1.4.Kauli ya Kutendana.

Kauli ya kutendana huwa na maana kuwa kuna watu au vikndi viwili au zaidi vya watu ambao wanafanya mambo kuathiriana. Yaani kundi moja hulitenda la pili nalo linalotendwa likalitenda hilo jingine. Athari za kitendo basi huwa kwa pande zote husika ambazo ni tendi na tendwa. (Habwe na Karanja (2004:112). Kauli ya kutendana hudokezwa kwa kiambishi –an-. Mathalani;

84. a) Majirani hawa wanapend**ana**.

b) Mabondia hawa wanapenda kupig**ana** masumbwi.

Japo tunakubaliana na kauli kuwa kauli ya kutendandana huonyesha kuwa watu wanatendana wakati uo huo, kuna uwezo wa watu kutendana mambo katika nyakati tafauti. Kwa mfano, katika sentensi;

85. Fahali hawa hupig**ana** kila mmoja aumiapo.

kuna uwezekano kuwa, mbali na kutenda wakati mmoja, walitenda vitendo vya kulipiza kisasi katika vipindi viwili yofauti. Kwa mfano, fahali wa kwanza humpiga alipoumia naye wa pili humpiga Yule wa kwanza wakati anapoumia.

3.3.1.5.Kauli ya kutendeana

Kauli hii husetiri maana kuwa tendo hufanywa na makundi mawili au zaidi kwa manufaa yao, ambapo kila kundi hulifanyia jingine lililomo katika ushirika fulani. Kama inavyobainika katika maelezo haya, kauli hii huhusisha taratibu mbili: kutendea na kutendana ambapo kutendea hutangulia kutendana. Kwa sababu hii, kauli hii huwa na mofu mbili; ya kutendea na ya kutendana. Kama tulivyoona hapo awali, mofu ya kauli ya kutendea huwa na alomofu tofauti kutegemea mazingira ya udhihirikaji ya kifonolojia. Zingatia mifano

86. a) Marafiki wema hupig**iana** simu.

b) Watoto wanasom**eana** Kuran katika madrassa.

3.3.1.6.Kauli ya Kutendesha

Kauli ya kutendesha hutumiwa kuonyesha kwamba kuna vikundi viwili ambapo kimoja husababisha kingine kutenda jambo fulani. Hii ina maana kwamba kundi linalosababisha jingine kutenda huwa na uwezo wa aina fulani juu ya lile litendalo. Mgullu (1999:206-7) anabainisha alomofu nne zinazodhihirisha kauli hii ya kutendesha. Alomofu hizi ni {lish}, {esh}, {z} na {lish} na kila moja huwa na mazingira yake maalum ya matumizi. Huku tukikubaliana na alomofu hizi, tunaongeza kuwa kuna alomofu zaidi za kauli ya kutendesha. Alomofu hizo ni pamoja na {iz}, {ez},[s},{fy} na {vy}. Tutafafanua kwa kutoa mifano ya matumizi ya alomofu hizo hapa chini;

i) Alomofu {ish} hutumiwa katika vitenzi vyenye mizizi iliyo na mojawapo ya irabu 'i', 'a' au 'u' na inayoisha kwa konsonanti kama vile; pata,shika, fika, piga, ruka, imba n.k. Mathalan:

87. a) Njia hii huwapit**isha** wema na waovu.

b) Askari jela aliwakat**isha** wafungwa nyasi.

c) Si vyema kumruk**isha** mtoto punde baada ya kula.

ii) Alomofu {esh} hutumiwa katika mazingira ya mzizi wa kitenzi wenye irabu 'o' au 'e' na unaoisha kwa konsonanti. Baadhi ya vitenzi vya sifa hii ni; soma, sema,cheza, enda n.k. Kwa mfano;

88. a) Mimi husom**esha** Kiswahili.

b) Churchil anaend**esha** baiskeli.

iii) Alomofu {s} hutokea katika mazingira ya baadhi ya vitenzi ila vichache sana. Kulingana na Oichoe (2005:118) 'hali hii hutokana na uyeyushaji wa kipasuo /t/ hadi kikwamizwa /s/' katika baadhi ya vitenzi vya Mamebantu. Sisi tunakubaliana

na maelezo haya kwa kiasi fulani. Hata hivyo tunasadiki kuwa huku ni kuchoofika kwa kipasuo wala sio uyeyushaji kama anavyotaja Oichoe. Mathalan

Kitenzi 'takata' huwa 'takasa'. Zingatia sentensi:

89. Maulana huwatakasa waumini wake.

iv) Alomofu {z} hutumika katika vitenzi viishavyo kwa shadda la irabu kama vile lia, toa, jaa. Paa, kataa, nyamaa, pungua, poa, n.k. Mathalan:

90. a) Kifo cha mpenziwe kimempunguza furaha yake.

b) Zakayo aliwatoza watu ushuru.

v) Alomofu {ez) hutumika endapo mzizi wa kitenzi una irabu 'e' au 'o' na unaisha kwa konsonanti (Oichoe 2005:119). Hata hivyo, sisi tunabainisha katika uchunguzi huu kuwa maelezo haya si jumuishi. Hi ni kwa kuwa kuna mizizi mingine ambayo inaisha kwa irabu lakini inayochukua ruwaza hii. Mifano ifuatayo inabainisha hili: penda- pendeza, toka- tokeza,potea- poteza, tembea- tembeza, pokea- pokeza. Tathmini matumizi katika sentensi:

91. a) Waridi alimpendeza Ali.

b) Watoto wa shule ya chekechea hupoteza kalamu kila mara.

vi) Alomofu {iz} hutumiwa katika baadhi ya vitenzi vyenye irabu 'i', 'a' na 'u' katika mizizi yake. Mathalani kimbia- kimbiza, chukia- chukiza, ingia- ingiza, iga- igiza. Tathmini mifano katika sentensi:

92. a) Nchi isiyowajibika huwaumiza watu wake.

b) Wakaazi wa hapa walimkimbiza mwizi.

vii) Alomofu {fy} hutokea katika mazingira ya mizizi iishayo kwa kipasuo /p/ kama katika maneno ogopa- ogofya, ongopa- ongofya, bopa- bofya na papa- pafya. Kwa mujibu wa Ireri (1985: 159) mofu {y} ni miongoni mwa alomofu za kauli ya kutendesha katika Mamebantu. Endapo mzizi una kipasuo /p/, kiambishi cha kutendesha kinapotiwa kati ya kipasuo hicho na kiishio, kipasuo hicho hudhoofika na kuwa kikwamizwa /f/. Tathmini mifano katika sentensi:

93. a) Vita vya baada ya uchaguzi wa mwaka wa 2007 viliwaogo**fya** wengi.

b) Mlio wa risasi huweza kumpa**fya** moyo mtu mwoga.

viii) Alomofu {vy} hudhihiri katika vitenzi vya mizizi inayoisha kwa kiyeyusho cha midomo /w/ ambapo kiyeyusho hicho hudondoshwa na nafasi yake kuchukuliwa na kikwamizwa cha midomo na meno /v/ kikifuatiwa na 'y' ya kutendesha. Mathalani lewa- levya, nawa- navya, lowa- lovya. Tathmini mifano katika sentensi:

88. c) Kileo hicho kitawale**vy**a wanywaji wake.

d) Yesu aliwana**vy**a wanafunzi wake wote.

ix. Alomofu {lish} na {lesh} hutumiwa katika vitenzi ambavyo mizizi yake huisha kwa shadda la irabu. Alomofu hutokea pale ambapo mzizi una mojawapo ya irabu 'I', 'a' na 'u', ilhali {lesh} hutokea katika vitenzi vya mizizi iliyo na irabu 'e' au 'o'. Zingatia vitenzi;

| Alomofu {lish} | alomofu {lesh} |
|---|---|
| i) kaa- ka**lish**a | komboa- kombo**lesh**a |
| ii) tia- ti**lish**a | zoa- zo**lesh**a |
| iii) tambua - tambu**lish**a. | toboa- tobo**lesh**a |

Kauli hii hudhihirika hivi katika sentensi:

94. a) Ni vyema kujitambu**lish**a usikotambulika.

b) Manispaa ya jiji huwazo**lesh**a wenyeji taka pindi wazitupapo kiholela.

Baada ya uchanganuzi tulioufanya hapo juu, inabainika kwamba kauli ya kutendesha huwa na alomofu nyingi mno, yamkini kuliko kauli nyinginezo katika vitenzi vya Kiswahili sanifu.

Aidha baadhi ya vitenzi huchukua alomofu nyingi kiasi cha kukosa kuwa na mfumo mahususi wa kuchukua kiambishi cha kauli hii. Mathalan'

Kitenzi jua huwa 'juza', 'juvya' na 'ju**lisha**'.

3.3.1.7.Kauli ya Kutendeshwa.

Kauli ya kutendeshwa ina maana kwamba mtu (watu) au kitu (vitu) kimesababishwa kutenda jambo fulani na mwingine au kingine chenye uwezo fulani. Kauli hii hutokana na kauli ya kutendesha na huwa alomofu mbalimbali. Tutatoa mifano michache ya vitenzi katika kauli hii katika sentensi;

95. a) Pondamali aliham**ishw**a nyumbani.
    b) Vyama vingi viliandik**ishw**a kwa mujibu wa sheria mpya ya vyama.
    c) Mwanafunzi alisom**eshw**a Hisabati.

Kama inavyobainika katika mifano tuliyotoa hapo juu, sentensi zilizo na vitenzi vya kauli ya kutendeshwa huanza kwa yambwa tendewa.

3.3.1.8.Kauli ya Kutendeshana

Kauli ya kutendeshana ina maana kwamba makundi mawili au zaidi yanasababishana kutenda jambo au mambo fulani. Kauli hii huhusisha kauli mbili tulizozijadili hapo awali: kauli ya kutendesha na ile ya kutendana. Kwa sababu hiyo, kauli ya kutendesheana huwa na viambishi viwili, kauli ya kutendesha ambayo inafuatiwa na ile ya kutendana. Kauli hii huchukua mofu (au alomofu) za kauli ya kutendesha hapo juu zikifuatiwa na mofu {an} ya kauli ya kutendana. Mathalani

| | | |
|---|---|---|
| i) | a) Lim+ish+an+a | limishana. |
| ii) | b) Som+esh+an+a | someshana. |
| iii) | c) Ingi+z+an+a | ingizana. |
| iv) | d) Tambu+lish+an+a | tambulishana. |

Zingatia mifano ifuatayo katika sentensi:

96. a) Watoto walioaga dunia wali**lishan**a sumu hatari.
    b) Wanasiasa hawa hupenda kuigi**zan**a kwenye jukwaa la kisiasa.

c) Wazee wa Njuri Ncheke husem**eza**na faraghani.

Ijapokuwa utaratibu wa kuunda kauli ya kutendeshana unaonekana kuwa wa moja kwa moja, baadhi ya vitenzi hughairi utaratibu huo. Mifano mahususi ni vitenzi vinavyochukua alomofu {fy} na {vy}. Vitenzi vinavyozalika hivi katika kauli ya kutendeshana havielekei kuwa sahihi na matumizi yake pia ni nadra sana. Tathmini maneno:

*Navyana, ogofyana, pafyana, levyana na lovyana n.k.

3.3.1.9.Kauli ya Kutendua

Vitenzi katika kauli ya kutendua huwasilisha maana kinyume ya kitenzi katika hali yake ya msingi. Viambishi vya kauli hii ni -o- na –u- kutegemea kanuni ya tangamano la irabu (Habwe na Karanja 2004, Ireri 1985 na Oichoe 2005). Endapo mzizi wa kitenzi una mojawapo ya irabu 'e' na 'o' mofu ya kutendua huwa {o} na mzizi huo ukaisha kwa konsonanti. Kwa upande mwingine, alomofu {u} hutumika ikiwa mzizi wa kitenzi una moja kati ya irabu 'a', 'i' na 'u'. Mbali na taratibu hizi, kuna vitenzi ambavyo mizizi yake huwa na irabu na ukaisha kwa irabu 'i' ambayo hudondoshwa na mahali pake kuchukuliwa na mofu {u} ya kutendua.Tathmini maneno;

| Alomofu {o} | | alomofu {u} | |
|---|---|---|---|
| i) Choma | chomoa | panga | pangua |
| ii) Kosa | kosoa | pinda | pindua |
| iii) Shona | shonoa | kunja | kunjua. |
| | | Pakia | pakua |
| | | Fukia | Fukua |

Tuzingatie mifano katika sentensi:

97. a) Mhunzi aliupinda mundu kisha akaupind**ua**.

b) Mwenendo mwema maishani ni kukos**o**a makosa.

c) Usomi wa kina unahusu pia kuwaza na kuwaz**ua**.

d) Utingo ataipakia mizigo kisha aipak**ue** mwishoni mwa safari.

Utafiti huu umebainisha kuwa vitenzi vinavyotumia mofu ya kutendua {o} ni vichache vikilinganishwa na vile vinavyotumia {u}.

3.2.1.10. Kauli ya Kutendata

Kauli hii huonyesha kuwa tendo limetendeka na kuwa katika hali ya mgusano au kushikana. Mofu ya kauli hii ni {at} ambayo pia ina alomofu {t}. Alomofu {at} hutumika katika mazingira ambapo mzizi wa kitenzi huisha kwa konsonanti. Kwa upande mwingine alomofu {t} hutumika katika mizizi inayoisha kwa irabu. Vitenzi hivi ni vichache sana katika Kiswahili (Habwe na Karanja 2004:112). Mifano ya vitenzi hivyo ni;

i) Fumba fumb**at**a
ii) Kama kam**at**a
iii) Paka pak**at**a
iv) Okoa oko**t**a.

Tathmini mifano katika sentensi:

98. a) Nilipoifumb**at**a sarafu yake hakuiona tena.

b) Msamaria mwema alimwoko**t**a mwana na akamtunza vyema.

3.2.1.11. Kauli ya Kutendama

Kauli ya kutendama huonyesha kuwa tendo limefanyika na kuwa katika mkwamo fulani unaodumishwa kwa kipindi fulani cha wakati. Kiambishi kinachodokeza kauli hii ni –m-. Kama, kauli iliyotangulia, kauli hii haidhihiriki katika vitenzi vingi vya Kiswahili sanifu. Mathalani:

i) Tanda tanda**m**a.
ii) Funga funga**m**a
iii) Ganda ganda**m**a
iv) Ficha ficha**m**a
v) Kunja kunja**m**a.

Utafiti huu umebainisha kwamba ni muhali kwa vitenzi katika kauli hii kutumiwa katika sentensi elekezi. Hata hivyo, hili linawezekana endapo vitenzi hivyo vinatumiwa kitamathali. Mathalani;

99. Mwanasiasa asiye na umaarufu amemgandama waziri ili asaidiwe tena.

## 3.3.0. KAULI KATIKA VITENZI VYA MKOPO.

Kama tulivyoeleza hapo awali, lugha ya Kiswahili imeweza kukopa maneno mengi, vikiwemo vitenzi kutoka lugha ambazo imetagusana nazo. Mengi ya maneno ya mkopo katika lugha hii yana asili ya Kiarabu. Vitenzi vingi vya asili ya mkopo katika Kiswahili huisha kwa irabu 'i', 'e' na 'u'. Irabu hizo huwa sehemu ya mizizi ya vitenzi husika. Katika kuambishwa mofu za kauli, vitenzi hivi kwa jumla hufuata ruwaza tofauti kidogo na vile vya asili ya Kibantu (Mgullu 1999:210). Katika sehemu hii tutaonyesha namna ya kuambisha mofu za kauli katika vitenzi hivyo. Maadamu tumekwishatoa maelezo kuhusu maana zinazosetiriwa katika kauli hizo, tutapania kutojirudia ila panapobidi kufanya ufafanuzi maalum.

### 3.3.1. Kauli ya kutendea.

Mofu ya kauli katika vitenzi vya asili ya mkopo huelekezwa pakubwa na irabu ya mwisho ya kitenzi husika. Endapo irabu hiyo ni 'i' au 'e' basi kiishio 'a' huongezwa kwa mzizi huo. Kwa upande mwingine, endapo irabu ya mwisho ni 'u', irabu hiyo hudondoshwa na mahali pake kuchukuliwa na mofu {i} ikifuatiwa na kiishio 'a'. Kulingana na Ireri (1785:167) udondoshaji huu huchochewa na utaratibu wa muundo pendwa wa silabi katika lugha ya Kiswahili. Hii ina maana kuwa, endapo irabu 'u' haikudondoshwa, basi kitenzi kitaisha kwa shadda la irabu tatu, muundo usiopendwa katika lugha hii. Yaani husudi- *husuduia, sifu – *sifuia, dhulumu- *dhulumuia n.k. Mathalani;

| Vitenzi vya 'i' | | | Vitenzi vya 'e' | | Vitenzi vya 'u' | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| i) | Sali - | salia | samehe - | samehea | husudu - | husudia |
| ii) | Buni - | bunia | balehe - | balehea | dhulumu - | dhulumia |
| iii) | Rudi - | rudia | starehe - | starehea | shutumu - | shutumia. |

Japo kisarufi vitenzi vingi vinachukua utaratibu huu, yaelekea kwamba sio vitenzi vyote katika kauli ya kutendea vina mantiki. Mathalani maana ya balehea, na husudia haielekei kuwa dhahiri. Tathmini matumizi katika sentensi;

100. a) Shehe Kijuba aliwasalia waumini.

b) *Mwalimu alimsamehea mzazi mwanawe.

c) Askari waliwaharibia majambazi mipango yao ya kuiba benkini.

Hata hivyo, katika vitenzi vinavyoisha kwa shadda la irabu, mofu ya kauli ya kutendea huwa {li}. Zingatia;

101. d) Rais almsahaulia mwanawe safarini.

e) Watu hawa hupenda kunidharaulia kila kilicho changu.

3.3.2. Kauli ya Kutendewa na Kutendwa

Tunastahabu kufafanua kauli hizi mbili kwa pamoja kwa kuwa viambishi vyake huwa na mwingiliano wa aina fulani unaozua utata endapo maana za vitenzi hazikuzingatiwa katika miktadha ya matumizi. Kauli ya kutendwa na ile ya kutendewa huwakilishwa kwa alomofu {iw} endapo irabu ya mwisho wa kitenzi ni 'i' au 'u' ambapo hiyo irabu 'u' hudondoshwa. Ikiwa irabu ya mwisho ni 'e', alomofu {e} hutumiwa (Mgullu 1999:211). Mathalani;

97. a) Hadhira ilikaririwa shairi na manju yule.

b) Maulana alisifiwa.

c) Aombaye msamaha husamehewa.

Huku tukikubaliana na maelezo kuhusu udondoshaji wa irabu 'u' katika vitenzi vinavyoisha kwa irabu hiyo, tunatofautiana na maelezo kuwa kauli hizi mbili huwakilishwa kwa alomofu {iw} na {ew}. Utafiti huu umebainisha kuwa mofu ya kutendwa na kutendewa ni {w}. Hii ni kwa kuwa irabu 'i' na 'e' zinazotangulia {w} ni sehemu ya mzizi. Kwa hivyo. Vitenzi hivyo hapo juu vinastahili kuwa; ilikaririwa, alisifiwa na husamehewa.

Ni dhahiri pia, kwamba, vitenzi katika miundo hii huwa na maana mbili: ile ya kutendwa na kutendewa. Mathalani katika mfano wa kwanza, manju alikaririri shairi kwa manufaa ya hadhira, na pia alikariri shairi kwa niaba ya hadhira.

### 3.3.3. Kauli ya Kutendana na Kutendeana

Kama kauli zilizotangulia za kutendwa na kutendewa, vitenzi katika kauli hizi mbili huwa na mofu zinazofanana ila maana zake hutofautiana kwa mujibu wa miktadha ya matumizi. Kwa jumla, maana zinazoakisiwa katika mofu za kauli hizi ni kuwa kuna zaidi ya kundi moja la wahusika na kila kundi husika linatenda tendo kwa manufaa ya kundi la pili na pia kwa niaba ya kundi la pili.

Mofu ya kauli ya kutendana na kutendeana ni {an} katika vitenzi viishavyo kwa irabu 'i' na 'e'. Katika vitenzi viishavyo kwa irabu ya nyuma juu /u/, alomofu ya kauli hizi huwa {ian}. Hapa, irabu hiyo hudondoshwa na mahali pake kuchukuliwa na kiambishi –ian- ambacho hatimaye hufuatiwa na irabu 'a'. Licha ya vitenzi hivi vinavyoisha kwa irabu moja, kuna vichache vinavyoisha kwa shadda la irabu. Viambishi vya kauli hizi katika vitenzi kama hivyo ni –lian-. Hapa, kiambishi hiki huambishwa baada ya irabu ya mwisho na hatimaye kufutiwa na kiishio 'a'.Tuzingatie vitenzi;

| Vitenzi vya 'i' | | vitenzi vya 'e' | | vitenzi vya 'u' | |
|---|---|---|---|---|---|
| i) Safari | - safiri**ana** | samehe - | samehe**ana** | Tubu | - tub**iana** |
| ii) Shiriki | - shriki**ana** | starehe - | sterehe**ana** | dhulumu - | dhulum**iana** |
| iii) Sali | - sali**ana** | | | sifu | - sifiana. |

Vitenzi vya shadda la irabu

i) Dharau dharau**liana**
ii) Sahau sahau**liana**.

Tathmini matumizi katika sentensi;

98. a) Mahasidi hao hudhulum**iana** familia zao.

b) Vijana wa sasa wanastahili kuhubiri**ana** injili.

c) Wakenya wanatakiwa kusemehe**ana** makosa yao.

d) Watu wanaodharau**lian**a tajriba zao huwa hawana ushirikiano mzuri kazini.

Tunapenda kukumbusha hapa kuwa, japo vitenzi hivi vinachukua viambishi vya kauli na kuwa sahihi kisarufi, baadhi ya vitenzi hivyo havina mantiki. Kwa mfano haiyamkiniki 'kumstarehea' au 'kumbalehea' mtu.

### 3.3.4. Kauli ya Kutendesha

Kauli ya kutendesha huwakilishwa kwa viambishi –sh- na –lish- katika mazingira mawili tofauti ya kifonolojia. Kiambishi –sh- hutumiwa katika vitenzi vilivyo na irabu 'i' na 'e' mwishoni.Mathalani'

i) Safari - safiri**sh**a
ii) Starehe - starehe**sh**a

Katika sentensi elekezi vitenzi hivi hudhihirika ifuatavyo;

99. a) Abiria hawa husafiri**sh**a mizigo ya kila nui.

b) Vijana wa sasa wanapenda kustarehe**sh**a rafiki zao vilabuni.

Kwa upande mwingine vitenzi vinavyoisha kwa shadda la irabu huchukua kiambishi –lish- katika kauli hii ya kutendesha. Mathalani;

viii) Askari fisadi atajisahau**lish**a kesi ili asifike mahakamani kutoa ushahidi.

### 3.3.5. Kauli ya Kutendeshwa

Kauli ya kutendeshwa huwakilishwa kwa mofu {shw} katika vitenzi viishavyo ama kwa irabu 'e' au 'i'. Katika vitenzi vinavyoisha kwa irabu 'u', irabu hiyo hudondoshwa na mahali pake kuchuliwa na mofu {ishw}. Kwa upande mwingine, vitenzi vinavyoisha kwa shadda la irabu kiambishi –lishw- huambishwa kwa mzizi. Baada ya kuambisha viambishi vya kauli, kiishio 'a' hutiwa katika miundo hii yote ya vitenzi. Kwa mfano;

i) Starehe - starehe**shw**a
ii) Dhulumu – dhulum**ishw**a
iii) Sahau - sahau**lishw**a .

Tathmini matumizi ya vitenzi hivi katika sentensi:

100. a) Mwaibale alifilisi**shw**a mali yake yote.

b) Kurgat atasahau**lishw**a matatizo yake na kazi nyingi itakayomkabili.

3.3.6. Kauli kutendeshana

Kauli hii hudokezwa kwa kiambishi –shan- ambacho hufuatiwa na kiishio ‘a’. Katika utafiti huu, tumebainisha kuwa kauli hii ina ufinyu wa ubunifu kwa kuwa inaelekea kupendelea vitenzi vinavyoisha kwa irabu ‘i’ katika hali yake ya msingi.Hata hivyo vitenzi vichache viishavyo kwa irabu ‘u’ huhusishwa ambapo irabu hiyo hudondoshwa na mahali pake kuchukuliwa na mofu {ishan}.Mathalani;

i) Shiriki - shiriki+sh an+a shiriki**shana**
ii) Safari safari+sh+an+a safirishana.
iii) Salimu – salim+ish+an+a – mithili**shana**.

Tuzingatie mifano katika sentensi elekezi;

101. a) Madereva hawa husafiri**shana** nyumbani giza liingiapo.

b) Majambazi hao walisalimi**shana** uhai wao walipojua wangeuana.

3.3.7. Kauli ya Kutendesheana

Kauli ya kutendesheana hudhihirishwa kwa kiambishi –shian- ambacho huwa na alomofu {sheana} katika vitenzi vinavyomalizika kwa irabu ‘e’. Kama kauli ya kutendeshana, kauli hii haina ubunifu mkubwa na huhusisha zaidi vitenzi viishavyo kwa irabu ‘i’. Hata hivyo, vitenzi vichache viishavyo kwa irabu ‘e’ hujumuishwa. Zingatia mifano;

i) Safari – safari+sh+ian+a – safiri**shiana**
ii) Wasili – wasili+sh+ian+a - wasili**shiana**
iii) Starehe – sterehe+sh+ean+a – starehe**sheana**.

Katika mifano hii, ni bayana kwamba kanuni ya tangamano la irabu inazingatiwa ambapo ierabu ya mzizi ‘e’ inachochea ‘e’ ya kiambishi cha kauli. Tathmini namna kauli hii inavyodhihirika katika sentensi elekezi;

102. a) Wachuuzi husafiri**shiana** mizigo yao baada ya kazi.

b) Waafrika wana mazoea ya kustarehes**heana** wageni.

3.4.0. HITIMISHO

Katika sura hii, tumeweza kuangalia dhana ya vitenzi. Tumeainisha na kufafanua aina mbalimbali za vitenzi. Tumeonyesha kuwa hapana uainishaji ambao ni wa moja kwa moja

kwa kuwa watafiti wa awali wameviainisha vitenzi kwa mikabala tofautitofauti na kwa hivyo wakajitokeza na makundi tofautitotauti kutegemea madhumuni na nyanja zao za utafiti. Uainishaji wetu umezingatia sio tu, miundo ya vitenzi hivyo bali pia sintaksia na etimolojia yavyo na kwa hivyo kujitokeza na makundi mengi kuliko watafiti waliotutangulia. Tumefanya hivyo makusudi kwa kuwa uainishaji wetu umetuwezesha kuonyesha taratibu mbalimbali za uambishaji mofu za kauli.

Maelezo yetu kuhusu kauli za vitenzi yamejikita katika sentensi elekezi ya Kiswahili sanifu. Tumeonyesha kuwa, uambishaji katika vitenzi vya Kiswahili sanifu huongozwa na kanuni ya tangamano la irabu. Tumebainisha pia kwamba ruwaza za uambishaji mofu za kauli zinatofautiana kwa kiasi fulani katika vitenzi vya asili ya Kibantu na vile vya asili ya mkopo. Tunatambua kwamba kuna kauli nyingi tu lakini tumestahabu kujikita katika mipaka na upeo wa utafiti wetu. Utafiti huu umebainisha pia, kwamba japo vitenzi vya asili ya mkopo huweza kuchukua aina fulani za viambishi vya kauli na kuonekana sahihi kisarufi, baadhi ya vitenzi hivyo hupoteza mantiki, na kwa hivyo, haviwi sahihi.

## 3.5.0. TANBIHI

1. Kulingana na Iribemwangi (2008) lugha zinapokurubiana na kutagusana katika matumizi, huwa zinaathiriana kifonolojia na hata kukopana msamiati na arki nyinginezo za kiisimu.
2. Neno 'oa' katika Kiswahili lina maana ya kitendo cha mwanamme kufanya muungano na mwanamke na kuishi pamoja naye kama mume na mke (TUKI 1990). Tendo la kuoa hufanywa na wanaume katika jamii za waafrika na kwa hivyo hapana hoja ya kutaja X amemwoa mke.

## 4.0. SURA YA NNE: UCHANGANUZI WA KAULI

### 4.1. UTANGULIZI

Katika sura hii tutafafanua na kuchanganua kauli za vitenzi katika Kiswahili sanifu katika muktadha wa sentensi elekezi. Kama tulivyoeleza katika sura iliyotangulia, uambishaji wa mofu za kauli huweza kubadilisha sio tu muundo wa kitenzi, bali pia sentensi yote. Uchanganuzi huu utajikita katika msingi wa nadharia ya Ubanifu. Tutatumia vielelezo vya mistari ili kuonyesha namna nadharia hii inavyotekelezwa katika lugha ya Kiswahili.

Uundaji tungo katika lugha chini ya nadharia ya Ubanifu huongozwa na Kanuni mbalimbali za iktisadi. Kipengele muhimu katika kanuni hizo ni usogezi. Usogezi huo huhusisha vipashio vilivyo na sifa za kimofosintaksia na vya kileksika kabla ya kufikia hatua mbili za Mjumuiko. Hatua hizo ni UF na UM na hufanywa ili kufanikisha ukaguzi sifa.Umuhimu wa utaratibu huu ni kuhakikisha kwamba tungo zalika ni sahihi kifonetiki na kisemantiki mtawalia. Aidha, usogezi huo huchochewa na haja kwani nadharia hii haikubali nafasi tupu. Hili lina maana kuwa vipashio ambavyo havijaidhinishwa na habari hizo za kimofosintaksia na za kileksika huwa havisogezwi kwani hapana haja ya ukaguzi sifa (Radford 1997:174 na Haegeman 1994:591).

Kwa mujibu wa Kaviti (2004:263), Kanuni ya Mvurumisho ya Chomsky inaeleza kuwa vipashio vyote vinavyosogezwa huwacha athari ambayo kimsingi ni kategoria tupu ya kipashio husika. Athari hiyo husalia kama ushahidi katika nafasi ya msingi ya kipashio husika. Aidha athari hiyo hufanya kazi kwa niaba ya kipashio kilichosogezwa kwa kuzingatia mahusiano mabalimbali ya kisarufi kwa kuwa inazingatiwa kama kijalizo cha kipashio kilichosogezwa. Hii ndiyo maana mtaalam huyo anahitimisha kuwa:

> 'Kipashio kilichosogezwa pamoja na athari yake huchukuliwa kuwa vinaunda 'mnyororo' ambapo 'mnyororo' hapa unadhaniwa kuwa aina ya rekodi inayoakisi historia ya usogezi ndani ya muundo husika. Kwa hivyo, athari hudokeza msingi wa 'mnyororo' na kipashio kilichosogezwa huwa kichwa' (TY).

Katika nadharia hii ya Ubanifu, kama tulivyotaja, nomino husogezwa chini ya spesifaya zake mahususi ambapo ukaguzi sifa za uhusika wa kiima na yambwa hutokea. Kwa upande mwingine, vitenzi husogezwa chini ya vichwa vyake mbalimbali kama vile NJ, HAL na UPK ili kuhakikisha kuwa sifa za upatanisho wa njeo, hali na kiima zinakaguliwa. Usogezi na ukaguzi huo kuhakikisha kuwa tungo zalika ni sahihi. Kitenzi, kwa mfano, hubeba mofu za upatanisho na njeo na sifa hizi hukaguliwa katika KUPK.

Usogezi wa nomino huongozwa pia na nadharia ya Uhusika, nadharia ambayo ina misingi yake katika Sarufi zalishi ya Chomsky ambayo ilipendekeza dhana za muundo ndani na muundo nje katika lugha. Ni kutokana na nadharia hiyo ya Sarufi Zalishi ambapo, baadaye, mwanaisimu Charles Fillmore (1968) alitumia dhana ya muundo ndani kuasisi sarufi ya Uhusika (Habwe na Karanja 2004).

Sarufi ya Uhusika ni nadharia ya kisarufi inayozingatia kuwa dhana ya uhusika ina umuhimu maalum katika uchambuzi wa tungo (TUKI 1990: 10).

Nadharia hii inaeleza kuwa vitenzi vya mwendo vinahusiana kwa namna fulani na nomino katika sentensi. Kwamba, nomino huwa na uamilifu maalum wa kisemantiki katika sentensi; uamilifu ambao husalia vivyo hivyo hata sentensi ikifanyiwa mageuzi ya kimuundo. Uamilifu huo ni pamoja na mtenda, mtendwa, mwathiriwa, nguvu, chanzo, lengo, wakati, mahali, malighafi na matokeo. Kwa mfano, tathmini sentensi;

i) Sadiq amenunua gari.
ii) Gari lilinunuliwa na Juma.
iii) Kiti kiliundwa kwa chuma.
iv) Chuma kilitumiwa kuunda kiti.

Katika sentensi za kwanza mbili, nomino *Sadiq* ni 'mtenda' kwa kuwa ndiyo inayosababisha kitendo cha kununua ilhali nomino *gari* ni 'kitendwa' kwa kuwa ndiyo inayoathiriwa na kitendo cha kununua. Katika mfano huu'mtenda' Sadiq ndiye kiima sentensi. Majukumu hayo yanasalia hivyo katika miundo yote ya sentensi.

Katika mifano (iii) na (iv) nomino *kiti* ina uamilifu wa 'matokeo' ilhali *chuma* ina uamilfu wa 'malighafi'. Hapa, *chuma* ni kitu kinachutumika katika ubadilishwaji kutoka hali moja hadi bidhaa iliyo tayari kwa matumizi. Matokeo kwa upande wake ni bidhaa itokanayo na malighafi.

Katika uchanganuzi wetu, tutaonyesha majukumu haya ya nomino na kuonyesha namna nomino hizo zinavyosogezwa katika vichwa vya spesifaya zake ili kukaguliwa sifa za uhusika.

Kwa mujibu wa Nadharia Tete ya Kuvunjika Virai, vitenzi hubeba viambishi mbalimbali vyenye majukumu na uamilifu wa kisemantiki na kisintaksia. Kila kiambishi katika kitenzi

huwa kirai ambacho hujisimamia. Kwa hivyo, viambishi hivyo vya njeo, upatanisho, yambwa kauli n.k huwa ni virai, kila kimoja kikijisimamia (Jerono 2003).

Viambishi vya kauli katika vitenzi vya Kiswahili sanifu huchochea taratibu za valensi. Kulingana na Lyons (1977:456) kama anavyonukuliwa na Otiso (2008) na Munyao (2006:7), 'Valensi huhusisha zaidi ya idadi ya kauli ambazo kitenzi kinaweza kuambatanishwa nazo katika sentensi iliyo sahihi' (TY). Hii ni kwa sababu valensi huhusisha tofauti katika kauli (nomino) ambazo huweza kuambatanishwa na kitenzi.

Vitenzi vya Kiswahili vina taratibu mbalimbali za kimofosintaksia zinazosawazisha majukumu ya kisintaksia na ya kisemantikii katika sentensi.

Kwa upande wake, Payne (1994:147) anaeleza dhana ya valensi kwa kuzingatia mikabala miwili; mkabala wa kisintaksia na ule wa kisemantiki. Kisintaksia, valensi ni jumla ya idadi ya agumenti zipatikanazo katika kishazi. Kwa upande mwingine, kisemantiki, valensi ni jumla ya wahusika; wanaoakisiwa katika kitenzi. Hapa, Payne anakiona kitenzi kama tukio katika uigizaji; tukio linalohitaji idadi fulani ya wahusika. Kwa hivyo, idadi jumla ya wahusika ambao kitenzi huambatanishwa nao ni valensi ya kisemantiki ya kitenzi hicho.

Maelezo haya yana maana kuwa, viambishi vya kauli katika vitenzi huwa na uwezo wa kuathiri, au hata kuamua jumla ya nomino zinazoweza kuambatanishwa na kitenzi katika kishazi sahihi cha Kiswahili sanifu. Viambishi hivyo vya kauli, mbali na kuamua idadi ya nomino zitokeazo pamoja na kitenzi katika kishazi sahihi, huweza kusababisha mpangilio mpya wa nomino katika sentensi. Katika lugha ya Kiswahili kuna taratibu za valensi ambazo huongeza idadi ya yambwa katika kishazi na kuna zile zinazopunguza idadi hiyo ya yambwa.

Katika nadharia ya Ubanifu, taratibu zote za valensi huchukuliwa kuwa vichwa. Fauka ya haya, taratibu zozote zinazoongeza agumenti ya ziada katika kishazi huunda uhusiano mpya wa spesifaya- kichwa kwa kichwa kilichoidhinishwa. Utafiti wetu utapania kuonyesha namna kanuni za usogezi na ukaguzi sifa zinavyoshirikiana kuhakikisha kwamba tungo sahihi zinapatikana kwa kuzingatia taratibu nbalimbali za valensi. Tutaonyesha pia kauli zinazoongeza idadi ya yambwa na zile zinazopunguza yambwa katika kishazi cha Kiswahili.

Kwa kuzingatia uelewa huu, tutachanganua data yetu kuhusu kauli tisa za vitenzi kwa kuonyesha mifano ya sentensi zenye aina mbalimbali za vitenzi.


4.2. Kauli ya Kutendea

Kama tulivyoeleza katika sura iliyotangulia, kauli ya kutendea ina maana ya kutenda kwa niaba ya, kwa manufaa ya, kwa kutumia kifaa au ala fulani, kutendea mahali fulani au kuelekea mahali fulani. Kauli hii huwa na taratibu zinazoongeza valensi kiasi kwamba sentensi iliyokuwa na yambwa moja inaweza kuongeza yambwa nyingine. Kauli ya kutendea huwa na viambishi vinavyochochea kuwepo kwa yambwa tendewa kuongezwa kabla ya yambwa tendwa katika sentensi. Kauli hii hudokezwa kwa viambishi –i-, -e-, -li- na –le-. Kila mojawapo ya viambishi hivi hutokea katika mazingira yake mahususi ya kifonolojia na huongozwa na kanuni ya uwiano wa irabu. Kuwepo kwa kiambishi cha kauli ya kutendea huchochea kitenzi husika kuchukua yambwa punde baada ya kitenzi husika. Ni vyema kutaja hapa kuwa, mofu inayotangulia mzizi pia huchochea yambwa baada ya kitenzi. Tutachanganua sentensi ifuatayo yenye yambwa mbili:

103. a) Mama alisoma hadithi.

b) Mama alimsomea mwanawe hadithi.

Kwa mujibu wa nadharia ya uhusika, nomino 'mama' inatekeleza jukumu la 'mtenda' nayo 'hadithi' ina uamilifu wa 'kitendwa' kwa kuwa inapata athari ya kitendo..


KUPK
Spes
Mama
UPK'
UPK
alimsomea
NJ'
NJ
at
KKEA'
Spes
mwanawe
KEA'
KEA
KUPYw
Spes
hadithi
UPYW'
UPYW
at
KT
Spes
ak
T'
T
at
KH
N
ayew
KN
N
ayw

Katika kielelezo hiki, yambwa tendwa 'hadithi' inasogezwa katika Spes ya KUPYW ili kukagua sifa yake ya uhusika wa yambwa na kuacha athari katika T cha T'. Yambwa tendewa 'mwanawe', kwa upande mwingine, inasogezwa katika Spes ya KKEA' ili kukagua sifa za uhusika yambwa. Kiima 'mama' kinasogezwa kutoka Spes ya KT ambako kinawacha athari, hadi katika Spes ya KUPK ili kufanikisha ukaguzi wa sifa zake za uhusika wa nomino ambayo ndiyo 'mtenda'. Kitenzi 'alimsomea' kinasogezwa katika UPYW ya UPYW' kukagua sifa zake za upatanifu kisha katika KEA ya KEA' kukagua kutendea. Hatimaye katika NJ ya NJ' kukagua sifa yake ya upatanifu wa njeo iliyopita, kabla ya kuishia katika UPK ya UPK' ambapo sifa yake ya upatanifu wa kiima hukaguliwa.

Kama inavyobainika katika kielelezo hiki, maadamu kitenzi ndilo neno kuu na lililo na uwezo wa kusetiri viambishi vingi vyenye uamilifu wa kisintaksia na kisemantiki, hakina budi kupitia msururu wa usogezi ili kuhakikisha kuwa sifa zote zinakaguliwa ili tungo zalika iwe sahihi.


## 4.3. Kauli ya Kutendwa

Katika sentensi za kauli ya kutendwa, kiima na yambwa hubadilishana nafasi katika sentensi zalika. Sentensi msingi huwa na kiima ambacho ndicho 'mtendaji'. Katika kauli ya kutendwa, kiima hicho hupoteza hadhi hii na umuhimu wa kimawasiliano ukawekwa katika kitenzi. Kiima katika sentensi zalika hukwezwa hadhi kiasi cha kutawala upatanisho katika hiyo sentensi zalika. Kauli hii ina utaratibu unaopunguza valensi katika sentensi kwa kuwa kiambishi cha kauli hii –w- huzua ufungizi kiasi kuwa yambwa zaidi ya moja haziwezi kukubaliwa na kitenzi Kitenzi katika kauli ya kutendwa huwa na uwezo wa kuchukua yambwa moja tu,' yambwa tendwa kwa sababu ya ufungizi unaosababishwa na mofu {w} ya kauli ya kutendwa. Tathmni mfano;

104.a) Jambazi lilimpiga askari risasi.

b) Askari alipigwa risasi (na jambazi).

Katika mifano hii, askari anakuwa 'mwathiriwa' kwa kuwa athari ya kupiga risasi inampata yeye. Kwa upande mwingine, risasi ni 'nguvu' kwa kuwa ndiyo inayotumiwa kutekeleza tendo linalotajwa katika kitenzi mintaarafu nadharia ya Uhusika;


KUPK
Spes
Askari
UPK'
UPK
alipigwa
NJ'
NJ
at
KUPYW
Spes
risasi
UPYW'
UPYW
at
KT
Spes
ak
T'
T
at
KN
N
ayw
KH
na jambazi

Katika kielelezo hiki cha kauli tendwa, yambwa tendwa 'risasi' inasogezwa kutoka kwa T cha KT hadi katika Spes ya KUPYW kwa ukaguzi wa sifa ya uhusika wa yambwa. Kiima 'askari' kinasogezwa kutoka kwa Spes ya KT ambapo kinawacha athari, hadi kwa Spes ya KUPK kwa ukaguzi wa sifa za uhusika wa nomino. Kitenzi 'alipigwa' nacho kinasogezwa kutoka katika nafasi yake ya msingi hadi kwa UPYW ya UPYW' kabla ya kusogezwa tena katika NJ ya NJ' na hatimaye kuishia kwa UPK ya UPK. Katika hatua hizi zote, sifa mbalimbali kama vile upatanisho wa kiima, njeo iliyopita na kauli ya kutendwa zinakaguliwa ili kuunda tungo sahihi kwa mujibu wa Kanuni ya Ufasiri wa Kina.

Katika kauli hii, kirai kihusishi, ambacho kimeshushwa hadhi na kuwa kiungo mbadala, hakiwezi kusogezwa. Hii ni kwa sababu kiungo hicho hakijaidhinishwa kimofolojia wala hakina sifa za kileksika zinazochochea usogezi wake. Kwa sababu hiyo, hakina sifa yoyote ya kukaguliwa (Munyao 2006:79).


## 4.4. Kauli ya Kutendewa

Kauli ya kutendewa huonyesha kuwa mtu au watu wanapata manufaa ya tendo fulani. Aidha, kauli hii inaonyesha kuwa tendo limetukia mahali fulani au limetekelezwa kwa ala au kifaa fulani. Kama tulivyoeleza hapo juu, kauli hii hudokezwa kwa mofu {ew} ambayo ina alomofu {iw}, {liw} na {lew} ambazo hudhihirika katika mazingira maalum ya kifonolojia.

Kauli ya kutendewa ni geuzwa ya kauli ya kutendea ambapo kiima na yambwa hubadilishana nafasi za kisintaksia. Fauka ya hayo, yambwa katika sentensi zalika hupoteza umuhimu wa awali wa 'mtendaji'na kuwa kiungo mbadala cha sentensi. Kwa upande mwingine, kiima cha sentensi zalika hukwezwa hadhi kiasi cha kutawala upatanisho wa kisarufi katika sentensi hiyo. Kitenzi katika kauli hii kina utaratibu unaopunguza valensi ambapo kina uwezo wa kuchukua yambwa moja tu; yambwa tendwa. Tutachanganua kauli hii kwa kutumia sentensi 105 (b) ambayo inazalika kutokana na sentensi 105 (a) hapa chini:

105.a) Wakenya walimpa Jelimo maua.

b) Jelimo alipewa maua (na Wakenya).





Katika kielelezo hiki, kiima zalika 'Jelimo' kinasogezwa hadi kwa Spes ya KUPK kwa ukaguzi wa sifa yake ya uhusika wa nomino huku yambwa tendwa 'maua' ikisogezwa kwa Spes ya KUPYW ili ukaguzi wa sifa ya uhusika yambwa utekelezwe. Kitenzi 'alipewa' kinasogezwa kwa usanjari ufuatao: kutoka UPYW ya UPYW', KEW ya KEW', NJ ya NJ' na hatimaye katika UPK ya UPK'. Usogezi huu hukusudia kukagua sifa za upatanisho yambwa tendwa na kauli ya kutendewa, upatanisho wa njeo iliyopita na hatimaye upatanisho na kiima mtawalia.

Katika taratibu hizi, kirai kihusishi 'na Wakenya' hakisogezwi kwa kuwa hakijaidhinishwa kimofolojia wala kileksika, na kwa hivyo, kwa mujibu wa kanuni ya usogezi wa nadharia ya Ubanifa, kipashio hicho hakina sifa ya kukaguliwa.

## 4.5. Kauli ya Kutendeana

Kauli ya kutendeana huonyesha dhana ya kutenda kwa manufaa ya washiriki wa zaidi ya upande mmoja. Ni vizuri kutaja tena hapa kuwa kauli hii inaonyesha uambishaji maradufu wa kauli. Katika utaratibu huu, kiambishi cha kauli ya kutendea hukitangulia kile cha kutendana. Hii ni kwa sababu kauli hii inahusisha kutendea na kutendana. Vitenzi katika kauli ya kutendeana vina uwezo wa kuchukua yambwa moja tu; yambwa tendwa. Kwa hivyo, kauli ya kutendeana ina utaratibu wa kupunguza idadi ya valensi katika sentensi. Hali hii inatokana na uhalisi kuwa kiima huchukua majukumu mawili; lile la kutenda na kutendewa. Kwa hivyo, yambwa tendewa haidhihiriki katika UM. Tutaonyesha namna kauli hii inavyjitokeza katika nadharia ya Ubanifu kupitia kwa sentensi:

106.a) Waumini husomeana Biblia.




Katika mfano huu, kitenzi 'husomeana' kinasogezwa kutoka hatua yake ya msingi hadi kwa UPY ya KUPY' kukaguliwa sifa ya upatanisho yambwa, kisha kwa KAN ya KAN' halafu kwa KEA ya KKEA' na hatimaye katika UPK/UPHAL ya UPK'/UPHAL' ambako sifa za kauli, hali na upatanisho wa kiima hukaguliwa mtawalia. Katika kitenzi husika, badala ya njeo kuna hali inayodokezwa kwa mofu {hu}. Mofu hii pia ina jukumu la upatanifu wa kiima katika sentensi husika.

Kwa upande mwingine, kiima 'waumini' kinasogezwa kutoka kwa T cha KT ambako kinawacha athari hadi kwenye Spes ya KUPK ambako sifa za uhusika wa nomino zinakaguliwa. Wakati uo huo, yambwa tendwa 'sala' inasogezwa kwa Spes ya UPYW kwa ukaguzi wa sifa ya uhusika wa yambwa tendwa.

Mbali na mfano wa sentensi yenye kiima dhahiri, sentensi ya Kiswahili yaweza kuwa bila kiima hicho dhahiri. Isitoshe, sentensi hiyo yaweza kuwa katika hali kanushi. Hivyo basi uchanganuzi wake utakuwa kama ifuatavyo hapa chini;

106. b) Hawakuwa wakisomeana tamthilia.


UPK
UPK
Hawakuwa wakisomeana
NJ'
NJ/UKAN
a Ts
HAL'
HAL
at
KEAN'
KEAN
-at
KUPYW
Spes
tamthilia
UPYW'
UPYW
at
KT
T
a Ts
T'
T
aT
KN
N
ayw


Katika mfano huu, hakuna nafasi ya kudhihirika kwa kiima wala spesfaya yake. Kwa hivyo, KT kinagawika kwa T' na KN inayosetiri yambwa tendwa. Yambwa hiyo inasogezwa kutoka kwa KN ya T' hadi kwa Spes ya KUPYW kwa ukaguzi wa sifa ya uhusika. Kitenzi kikuu 'wakisoma' nacho kinasogezwa kwa UPYW ya UPYW' kisha kwa KEAN ya KEAN' ili kukaguliwa sifa ya upatanisho yambwa na kauli ya kutendeana. Kitenzi hicho halafu kinasogezwa kwa HAL ya HAL' ili kukagua sifa ya hali ya utegemezi ilyosetiriwa kwa mofu {ki}. Baada ya hatua hii, kitenzi hicho kinasogezwa tena katika UPK ya UPK' ambapo kinakaguliwa sifa ya upatanisho kiima kwa pamoja na kitenzi kisaidizi.

Katika sentensi ya vitenzi sambamba kama hii, kitenzi kisaidizi huwa na majukumu tofautitofauti. Katika mfano wetu hapo juu, kitenzi Ts 'hawakuwa' kinatekeleza majukumu ya ukanusho, upatanisho wa kiima na njeo iliyopita. Ni sharti hizi sifa zote zikaguliwe ili tungo zalika liwe sahihi. Kwanza, kitenzi hiki kinasogezwa katika NJ/UKAN ya NJ'/UKAN' kwa ukaguzi wa sifa za njeo iliyopita na ukanusho. Baada ya hapa, kinasogezwa katika UPK ya UPK' kwa ukaguzi wa sifa ya upatanisho kiima. Tunakumbusha hapa kuwa mofu {ha} inatekeleza majukumu ya upatanisho na ukanusho wa nafsi ya tatu.

## 4.6.Kauli ya Kutendana

Kauli ya kutendana huonyesha kuwa kuna watu au vikundi viwili au zaidi ambavyo vinatenda matendo kwa manufaa ya kila mhusika kuatika kikoa hicho.Kauli ya kutendana huzua ufungizi ambapo kitenzi huweza kuchukua yambwa tendwa peke yake. Kwa sababu hii, kauli hii ina utaratibu wa kupunguza idadi ya valensi katika tungo sanifu. Kauli hii hudhihirika ifuatavyo katika mfanyiko wake wa kimkokotoo:

107.Mabondia wanapigana masumbwi.





Katika kielelezo hiki, kiima 'mabondia' kinasogezwa kutoka katika T cha KT hadi katika Spes ya KUPK kwa ukaguzi wa sifa ya uhusika wa nomino. Yambwa tendwa 'masumbwi' inasogezwa katika Spes ya KUPYW ambapo ukaguzi wa uhusika yambwa unatekelezwa. Kwingineko kitenzi 'wanapigana' kinasogezwa hadi katika NJ/HAL ya NJ'/HAL' kwa ukaguzi wa njeo ya sasa na hali ya kuendelea. Tunakumbusha hapa kuwa, utafiti huu, kama ulivyobainisha katika sura ya pili, mofu {na} huwa na majukumu mawili katika kitenzi cha Kiswahili sanifu. Jukumu la kwanza ni kuonyesha njeo iliyopo na la pili ni kuonyesha hali ya kuendelea. Hatimaye kitenzi hicho kinasogezwa hadi katika UPK ya UPK' kwa ukaguzi wa upatanisho wa kiima.

### 4.7.Kauli ya Kutendesha

Kauli ya kutendesha huonyesha usababishi, ambapo mtu au kitu hukifanya kingine kutekeleza jambo fulani. Kauli hii, kama tulivyodokeza katika sura ya tatu, ina alomofu nyingi zinazoibainisha.

Tathmini sentensi ifuatayo yenye yambwa moja kwa uchanganuzi wa sentensi ya kauli ya kutendesha:


108.a) Mwalimu amewasomesha wanafunzi.



Katika uchanganuzi huu, kiima 'mwalimu' kinasogezwa kwa Spes ya KUPK kwa ukaguzi wa sifa ya uhusika wa nomino. Wakati uo huo, yambwa tendwa 'wanafunzi' inasogezwa kwa Spes ya KKESH kwa ukaguzi wa sifa ya usababishi. Kitenzi 'amewasomesha' kinasogezwa kwanza katika KSH cha KSH' na pia katika HAL ya HAL' ambapo sifa ya hali inakaguliwa. Hatimaye kitenzi hicho kinasogezwa hadi kwa UPK ya UPK' kwa ukaguzi wa sifa ya upatanisho wa kiima. Kama inavyobainika katika mfano huu, hakuna nafasi ya UPYW. Hili linatokana na uhalisi wa nadharia Ubanifu kuwa nafasi tupu hazikubaliwi katika ujenzi wa tungo, hasa Kanuni ya Ufafanuzi wa Kina ikizingatiwa.

Katika mfano ufuatao, tunachanganua sentensi elekezi yenye yambwa mbili; tendewa na tendwa:

108.b) Mtumishi alimnywesha mtoto maziwa.




Hapa yambwa tendwa 'maziwa' inasogezwa' kwa Spes ya KUPYW kukaguliwa sifa zake za uhusika. Yambwa tendewa 'mtoto' inasogezwa katika Spes ya KKSH' ambapo sifa zake za uhusika wa kutendesha zinakaguliwa. Kwingineko, kiima 'mtumishi' kinasogezwa katika Spes ya KUPK ambako sifa zake za uhusika wa kiima zinakaguliwa. Wakati uo huo, kitenzi 'alimnywesha' kinasogezwa katika UPYW ya UPYW' kukaguliwa sifa za upatanisho, kisha katika KSH ya KSH' ambapo sifa za utendeshaji zinakaguliwa. Baadaye kinasogezwa katika NJ ya NJ' kukaguliwa sifa zake za njeo iliyopita kabla ya kusogezwa tena katika UPK ya UPK' kwa ukaguzi wa sifa za upatanisho wake na kiima cha sentensi. Utaratibu huu una usogezi na ukaguzi mwingi kwa kuwa vipashio vyote amilifu vina sifa nyingi zinazostahili kukaguliwa ili kuunda tungo sahihi kwa mujibu wa KUK.

4.8. Kauli ya Kutendeshea

Kauli ya kutendeshea ina maana kuwa kuna mtu au kitu kinachosababishwa kutekeleza tendo kwa manufaa ya kingine au mwingine. Kauli hii, kwa hivyo, huhusisha kitenzi elekezi kilicho na uwezo wa kuchukua yambwa moja au mbili. Kauli hii inajumuisha kauli mbili: kutendea na kutendesha.

Kauli ya kutendesha inaelekea kuoana na Kanuni ya Kioo inayoelezwa na Baker (1998:13), ambayo inaeleza kwamba,

> 'Ni sharti uambishaji wa kimofolojia uakisi uambishaji wa kisintaksia na ule wa kisintaksia sharti uakisi uambishaji wa kimofolojia'.


Kanuni hii ina maana kwamba mabadiliko ya kimofolojia yanayoshuhudiwa hufanyika sambamba na katika utaratibu uo huo wa yale ya kisintaksia. Kwa mfano, katika sentensi; '*Dereva amwendeshea mwajiri gari'*, viambishi vya kimofolojia vya kauli za kutendea na kutendesha –e- na –sh- mtawalia ni sharti vioane na mpangilio wa kisintaksia wa yambwa mbili 'mwajiri (tendewa) na 'gari' (tendwa).

Tunabainisha katika utafiti huu kuwa, japo hali hii hudhihirika pakubwa miongoni mwa watumizi wa lugha ya Kiswahili, yambwa tendwa yaweza kutangulia yambwa tendewa. Kwa mfano, ni kawaida ya wasemaji wazawa wa Kiswahili kusema;

'*Dereva amwendeshea gari wajiri'*. Hali hii haitatizi mawasiliano kwa vyovyote. Kwa hivyo, lugha ya Kiswahili inaelikea kutoafiki Kanuni ya Kioo ya Baker.

Katika mfano wetu hapo juu, 'Dereva' ni mtenda, gari ni 'kifaa' na 'mwajiri' ni mtendewa kwani anapokea manufaa ya kuendeshewa. Tutachanganua sentensi ya yambwa mbili kudhihirisha utendekazi wa nadharia ya Ubanifu katika mfano ufuatao:

109.a) Dereva amwendeshea mwajiri gari.





Katika kielelezo hiki, kiima 'dereva' kinasogezwa kwa Spes ya KUPK kwa ukaguzi wa sifa yake ya uhusika wa kiima. Yambwa tendwa 'gari' inasogezwa kwa Spes ya UPYW kwa ukaguzi wa sifa zake za uhusika yambwa tendwa ihali yambwa tendewa 'mama' inasogezwa kwa Spes ya KKSHE ambako ukaguzi wa sifa za uhusika wa yambwa tendewaunafanyika. Kwa upande wake, kitenzi husogezwa kwa usanjari ufuatao: katika UPYW ya UPYW', KSHE ya KSHE' na kisha katika UPK/HAL ya UPK'/HAL'. Usogezi huu unakusudia kukagua sifa za upatanifu yambwa, upatanifu wa hali na upatanifu na kiima mtawalia.

Tunapenda kutaja hapa kuwa, kitenzi hiki hakina njeo bali kina hali isiyo maalum inayodokezwa kwa {a}. Mofu hii ina majukumu mawili katika sentensi; inafanikisha upatanisho wa kiima na pia inaleta upatanifu wa hali isiyo dhahiri.

Utafiti huu unabainisha kuwa Kiswahili ni miongoni mwa lugha zisizo na kiima dhahiri. Hili lina maana kwamba sentensi ya Kiswahili inaweza kukamilika kimaana bila kiima almuradi viambishi vya nafsi au vya ngeli huweza kuambatanishwa kwenye mzizi. Viambishi hivi hufanikisha upatanisho wa kiima (Radford 1997:138). Mathalan;

109. b) Tutawasafirishia wageni mizigo.





Katika kielelezo hiki, taratibu zote za usogezi na ukaguzi sifa zinatokea kama katika mfano 109. a) hapo juu. Hata hivyo, maadamu hakuna kiima dhahiri, hakuna kichwa KUPK na hata spesifaya yake. Sehemu ya KT kwa hivyo ina T' peke yake ambayo inagawika kwa T na KN.

Hili lina maana kuwa hakuna ukaguzi wa sifa ya uhusika wa nomino kwa kuwa kama tulivyotaja, nadharia ya Ubanifu haikubalii nafasi tupu.

4.9. Kauli ya Kutendeshana

Kauli hii inajumuisha kutenda na kutendana. Kitenzi kilicho na kiambishi cha kauli hii huwa na utaratibu wa kupunguza valensi kwa kuwa kinaweza kuchukua yambwa moja tu; yambwa tendwa. Tutaichanganua sentensi ifuatayo ili kuonyesha utendakazi wa nadharia hii ya ubanifu:

110.Maarusi watalishana keki kanisani.



Kutokana na kielelezo hiki, inabainika kuwa kiima 'maarusi' kinasogezwa kutoka sehemu yake ya msingi ya Spes ya KT hadi katika Spes ya KUPK ambapo sifa za uhusika wa kiima zinakaguliwa. Kiima hiki kinasalisha athari yake katika Spes ya KT. Yambwa tendwa 'keki' nayo inasogezwa katika Spesfaya ya UPYW' ambapo sifa ya uhusika yambwa inakaguliwa. Kitenzi 'walilishana' kinasogezwa katika UPYW ya UPYW' na baadaye katika KAN ya KAN kwa ukaguzi wa sifa ya kauli ya kutendana kabla ya kuishia katika KSH ya KKSH kwa ukaguzi wa sifa ya kutendesha kwa ukaguzi wa sifa ya upatanisho wa kutendesha. Baada ya hatua hiyo, kitenzi hicho kinasogezwa tena kwa NJ ya NJ' kabla ya kuishia katika UPK ya UPK' kwa ukaguzi wa sifa za njeo iliyopita na upatanisho wa kiima mtawalio.

Ni bayana katika kielelezo hiki kuwa, nafasi ya yambwa tendewa haipo. Hali hii inatokana na uelewa kwamba sentensi ya kauli ya kutendeshana huwa na kiima ambacho pia ndio mtendewa. Kwa hivyo, kauli ya kutendeshana huwa na yambwa moja; yambwa tendwa. Nafasi hiyo ya yambwa tendewa, kwa hivyo, haidhihiriki katika wasilisho la UM. Hali hii inatimiza hitaji la kanuni ya nadharia ya Ubanifu isiyokubalia nafasi tupu (Chomsky 1995:198).

Mbali na hayo, sentensi hii ina kielezi 'kanisani' ambacho hakisogezwi kwa kuwa hakijaidhinishwa kimofolojia wala kileksika. Katika nadharia hii, sifa hizi hupewa vitenzi na nomino tu. Kwa sababu hiyo, hakina hitaji la kukaguliwa sifa (Kaviti 2004).


## 4.10. Kauli ya Kutendeshwa

Kauli ya kutendeshwa inajumuisha kauli mbili: kutendesha na kutendwa. Katika ukaguzi wa sifa, kitenzi husogezwa kwanza katika kauli KW ya KW' kabla ya kusogezwa tena katika KKSH ya KKSH' kwa ukaguzi wa sifa ya upatanisho wa kutendwa na kutendesha kwa usanjari huo.

Kauli hii pia inadhihirisha Kanuni ya iktisadi ya usogezi mfupi sana ambapo kitenzi kinasogezwa katika sehemu ya karibu ya ukaguzi kabla ya kusogea mbali. Kama kauli iliyotangulia, kauli ya kutendeshwa hupunguza valensi kwa sababu huchukua yambwa tendwa tu. Aidha, baada ya geuzwa la kutendeshwa, kirai kihusishi 'na Baya' katika mfano wa sentensi ifuatayo kinapoteza umuhimu wake wa kiima na kwa hivyo kuwa kipashio mbadala katika sentensi hii.

Katika utafiti wetu, tutaichambua kauli hii kwa kuzingatia sentensi

111.Dude alirambishwa asali na Baya.




Katika mfano huu, kiima 'Dude' kinasogezwa kutoka kwa Spes ya KT hadi kwa Spes ya KUPK kwa ukaguzi wa sifa za uhusika wa kiima. Kiima hicho kinawacha athari katika Spes ya KT. Wakati uo huo, yambwa tendwa 'asali' inasogezwa hadi kwa Spes ya KUPYW kwa ukaguzi wa sifa zake za uhusika wa yambwa. Kitenzi 'alirambiswa' nacho kinasogezwa kutoka nafasi yake ya msingi hadi kwa UPYW ya UPYW' ambapo sifa zake za upatanifu wa uhusika zinakaguliwa. Kitenzi hicho, kisha kinasogezwa kwa KW ya KW' na KSH ya KSH' ili kukaguliwa hali yake ya kutendwa na kutendesha kwa usanjari huo kabla ya kusogezwa

tena katika NJ ya NJ' na baadaye kwa UPK ya UPK' ili kukaguliwa sifa zake za njeo iliyopita na upatanifu wa kiima mtawalia. Katika usogezi unaofanyika athari mbalimbali za kitenzi hicho zinawachwa katika kila awamu kinapohamishwa.

Katika tungo hii, kirai kihusishi 'na Baya' hakisogezwi kwa kuwa hakina sifa zistahilizo za kimofolojia na kileksika kusogezwa, na kwa sababu hiyo, hakina sifa zinazostahili kukaguliwa kama vitenzi na nomino kwa mujibu wa nadharia ya Ubanifu.

## 4.11. HITIMISHO

Katika sura hii, tumeeleza kwa kutumia vielelezo namna kauli za vitenzi zinavyojitokeza kwa mujibu wa nadharia ya ubanifu. Tumetambua kuwa kuna taratibu mbili kuu za valensi katika kauli za vitenzi, utaratibu wa kuongezeka kwa agumenti na ule wa kupungua. Kauli ambazo zinachochea kupunguka kwa valensi hasa ni zile zinazozua ufungizi kiasi kwamba kitenzi elekezi huchukua yambwa moja tu. Miongoni mwa kauli hizi ni pamoja na kauli ya kutendwa, kutendeshwa, kutendeshana, kutendeana, kutendana na kutendewa. Kauli zinazozua utaratibu wa kuongezeka kwa agumenti katika lugha hii ya Kiswahili huvifanya vitenzi kuchukua yambwa mbili. Uchunguzi wetu umebainisha kuwa yambwa tendewa huitangulia yambwa tendwa katika sentensi elekezi ya Kiswahili. Kauli za vitenzi ambazo zinachochea ongezeko la agumenti ni pamoja na kauli ya kutendea, kutendesha na kutendeshea.

Tumebainisha pia, kwamba, Kanuni kioo ya Baker (1998) haielekei kuwa na mashiko katika kuamua muundo wa sentensi. Hii ni kwa kuwa katika lugha ya Kiswahili yambwa tendwa inaweza kutangulia au kufuata yambwa tendewa bila kubadilisha maana ya sentensi wala kukwaza mawasiliano. Fauka ya haya, tumeonyesha namna usogezi hutekelezwa ukiwa na madhumuni ya kukagua sifa muhimu za vitenzi na nomino.

## 5.0. SURA YA TANO: HITIMISHO NA MAPENDEKEZO

### 5.1. HITIMISHO

Utafiti huu ulikusudia kuchanganua kauli katika sentensi elekezi ya Kiswahili sanifu kwa kutumia nadharia ya Ubanifu. Tumefanya hilo hasa kwa kujikita katika Kanuni za Iktisadi ambazo huhusisha usogezi, usogezi unaokusudiwa kufanikisha ukaguzi wa sifa mbalimbali ili tungo zalika ziwe sahihi.

Katika sura ya kwanza ya kazi hii, tumetoa utangulizi wa utafiti. Tumefafanua mada ya utafiti, nadharia tete, madhumuni ya utafiti na tukafafanua kwa kina nadharia tuliyoitumia ya Ubanifu. Tumeeleza pia mbinu za utafiti, uhalalishaji wa utafiti, umuhimu wake pamoja na kudurusu yaliyoandikwa kuhusu mada yetu ya utafiti pamoja na nadharia ya Ubanifu.

Katika sura ya pili tumeeleza dhana za Uambishaji na Unyambuaji kama taratibu mbili za kisarufi. Tumefafanua pia tofauti za dhana hizi kwa kuweka vigezo vya kuzitofautisha. Hatimaye tumeeleza viambishi mbalimbali vya vitenzi vya Kiswahili sanifu. Tumeonyesha kuwa viambishi vya kauli ni viambishi tamati vya kitenzi cha Kiswahili sanifu. Fauka ya hayo, tumeeleza kuwa mofu za kauli ni tokeo la uambishaji wala sio la unyambuaji kama ambavyo baadhi ya wataalam waliotutangulia walivyoeleza.

Sura ya tatu imefafanua aina mbalimbali za vitenzi kwa misingi ya asili zake, mofolojia yake na sifa zake za kisintaksia. Katika kufanya hivyo, tumeeleza kuwa hakuna idadi mahususi ya vitenzi kwa sababu kila mtafiti anaviainisha kutegemea madhumuni ya utafiti wake. Aidha sura hii imefafanua aina tofautitofauti za kauli katika vitenzi vya Kiswahili katika muktadha wa sentensi elekezi.

Katika sura ya nne tumezifafanua kauli za vitenzi kwa kutumia nadharia ya Ubanifu. Tumeeleza kuwa Kiswahili kama lugha yenye upatanisho imara, kinaafiki mahitaji ya nadharia hii. Tumetumia vielelezo vya mistari kuonyesha usogezi wa vipashio vya tungo. Tumefafanua pia namna Kanuni za iktisadi zinavyoshirikiana katika nadharia hii kufanikisha usogezi wa vipashio ili kufanikisha ukaguzi mbalimbali wa vipashio vya kisarufi. Tumeonyesha pia kwamba, kila kipashio kinachosogezwa huwacha athari katika nafasi msingi kama rekodi ya usogezi huo na ukaguzi.

Fauka ya hayo tumeonyesha kuwa Kiswahili ni lugha ambayo huweza kuwa bila kiima dhahiri katika sentensi. Hata hivyo tumefafanua umuhimu wa kiima dhahiri na kisicho dhahiri katika kuleta upatanisho wa kisarufi katika sentensi. Tumeeleza pia, kwamba viambishi vya njeo na hali huwa katika mgawanyo wa kiutoana katika sentensi za Kiswahili sanifu. Hata hivyo, kwa kutumia mifano, tumeonyesha kuwa kiambishi cha njeo -na- huweza kutekeleza jukumu la hali pia. Mbali na hayo tumeonyesha kuwa baadhi ya viambishi vya hali kama vile hali isiyo maalum na hali ya mazoea hutekeleza upatanisho wa kisarufi katika sentensi ya Kiswahili.

Utafiti huu uliweza kufikia malengo yake na pia kuthibitisha nadharia tete zilizouongoza. Mosi, tumebainisha kuwa viambishi vya kauli ni viambishi tamati katika kitenzi cha Kiswahili sanifu. Viambishi hivi hutokea katika aina takribani zote za vitenzi elekezi. Vitenzi vishirikishi, visaidizi na visoelekezi havichukui viambishi vya kauli na kwa sababu hiyo havitumiwi kuunda sentensi elekezi.

Katika utafiti huu, ilibainika pia, kuwa, japo vitenzi vyote elekezi huchukua viambishi mbalimbali vya kauli, baadhi ya vitenzi vilivyo na viambishi hivyo hupoteza mantiki. Vitenzi hivyo vingi vilikuwa vya sili ya kigeni kama vile; *sherehekeana, sahauliana, thubutia* miongoni mwa vingine. Ukosefu huo wa mantiki unatokana na uhalisi kuwa mtu hawezi kumtendea mwenzake vitendo vinavyosawiriwa katika vitenzi hivyo.

Uchunguzi huu umebainisha kuwa baadhi ya kauli hukubalia yambwa mbili ilhali nyingine huzua ufungizi ambapo ni yambwa tendwa peke yake inaweza kufuatia kitenzi katika sentensi ya Kiswahili sanifu. Yaani;

a) Kauli ya kutendwa, kutendana kutendua, kutendata, kutendama, kutendeshana na kutendeshwa husababisha kupungua kwa valensi katika sentensi sahihi ya Kiswahili sanifu kwa kuwa zinakubalia yambwa moja; yambwa tendwa.
b) Kauli ya kutendea, kutendewa, kutendeana, kutendesha na kutendeshea husababisha utaratibu wa kuongezeka kwa idadi ya valensi katika sentensi. Hii ina maana kuwa kauli hizi hukubalia yambwa mbili; yambwa tendewa na yambwa tendwa.

Tulibainisha pia kwamba, viambishi vya kauli mbalimbali pamoja na mofu za yambwa katika sentensi elekezi huelekezwa na viambishi vya mtendwa na mtendewa vinavyotokea kabla ya mzizi wa kitenzi.

Tumebainisha pia kwamba, viambishi vya kauli huathiri na kupangua mpangilio wa sentensi lakini haviathiri maana ya sentensi husika. Hali hii pia inaafiki mwongozo wa nadharia ya Uhusika ambayo inaonyesha kuwa nomino huwa na uamilifu maalum katika sentensi na uamilifu huo haubadiliki hata miundo ya sentensi ikibadilishwa.

Utafiti wetu pia umebainisha kuwa mofu za kauli huongozwa pakubwa na kanuni ya Wiano wa Irabu. Tumeonyesha kuwa irabu kaze zinapokuwa katika mzizi wa kitenzi na mzizi huo uishe kwa konsonanti, kauli hudokezwa kwa kiambishi -i-. Ikiwa mzizi una irabu 'e' au 'o' halafu uishe kwa konsonanti, kiambishi cha kauli hudokezwa kwa –e-. Utafiti huu umebainisha kuwa endapo kitenzi kinaisha kwa shadda la irabu, kauli hudokezwa kwa –li- au -le-. Tumeonyesha pia uambishaji wa mofu za kauli hufanana na kutofautiana kwa kiasi fulani katika vitenzi vya asili ya Kibantu na vile vya asili ya mkopo. Kwa mfano, tumebainisha kuwa mofu ya kauli ya kutendwa na kutendewa katika vitenzi vya asili ya mkopo {iw} huwa na mofimu mbili kama inavyodhihirika katika neno 'sifiwa'.

Katika uchunguzi tulioufanya tumeonyesha kuwa Kiswahili ni lugha yenye upatanisho imara. Aidha viambishi vyote vya vitenzi huzingatiwa kama virai vinavyojisimamia. Kwa sababu hiyo, hali hii inaafiki vizuri mahitaji ya nadharia ya Ubanifu hasa kipengele chake cha usogezi wa spesifaya katika kichwa kwa ukaguzi wa sifa mbalimbali. Kwa sababu hii, nadharia hii ya Ubanifu ni mwafaka kwa uchanganuzi wa lugha hii ya nasaba ya Kibantu.

## 5.2. MAPENDEKEZO

Utafiti wetu ulifanywa kuhusu kauli katika sentensi elekezi ya Kiswahili sanifu. Lugha hii ina lahaja nyingi. Kwa sababu hii, tunapendekeza kuwa utafiti zaidi unaweza kufanywa kuhusu lahaja za Kiswahili ili kutathmini endapo kuna mwingiliano au tofauti katika ruwaza za kauli kati ya vitenzi vya Kiswahili sanifu na vitenzi vya lahaja hizo.

Aidha, tunapendekeza kuwa utafiti zaidi unaweza kufanywa kuhusu lugha nyinginezo za Kibantu kwa kutumia nadharia hii ya Ubanifu ili kuona endapo matokeo yake yatakuwa sawa na haya yetu. Utafiti huo unaweza kuwa wa kiulinganishi ili kubainisha mahusiano ya kauli kati ya lugha ya Kiswahili sanifu na lugha zenza za Kibantu.

Katika utafiti huu, tulijikita katika mipaka na upeo wa sentensi sahili ya Kiswahili sanifu. Litakuwa jambo la busara endapo uchunguzi wa kauli unaweza kufanywa katika sentensi ambatano, changamano na ambatano changamano. Utafiti kama huo utatusaidia kuona namna usogezi unafanywa katika muktadha wa vishazi viwili vikuu pamoja na vishazi tegemezi.

Mbali na kauli, kitenzi cha Kiswahili kina viambishi vingine muhimu ambavyo vina uamilifu tofautitofauti wa kisarufi. Itakuwa vyema endapo utafiti utafanywa kuhusu viambishi ambavyo havijawahi kufanyiwa uchunguzi, na hasa kwa kutumia nadharia ya Ubanifu. Viambishi hivyo ni kama vile viambishi vya, urejeshi, ukanusho, yambwa na vile vya dhamira ili kuleta uelewa mzuri wa vipashio mbalimbali vya kisarufi katika kishazi cha Kiswahili sanifu.

## MAREJELEO


Abdulaziz, M. H (1996). *Transitivity in Kiswahili.* Koln: Ruidiger Koeppe Verlag.

Baker, M.C. (2003). *Lexical Categories: Verbs, Nouns and Adjectives.* Cambridge: Cambridge University Press.

Baya, F.M. (1993*). Kitenzi Kisaidizi cha Kiswahili: Mtazamo wa Sarufi Geuza Maumbo Zalishi.* Tasnifu ya M.A ambayo haijachapishwa,: Chuo Kikuu cha Nairobi.

Broomfield, G.W. (1975). *Sarufi ya Kiswahili.* Nairobi: General Printers Limited.

Chomsky, N. (1 957). *Syntactic Structures.* The Hague: Mouton.

---------------- (1965). *Aspects of The Theory of Syntax.* Massachusetts. MIT

--------------- (1993). A Minimalist Program for Linguistic Theory ; in Occasional papers in Hale, K and Keyson, S.J. (eds) in The View from Building 20: Essays in Honour of the Sylvian Brombeger. Massachusetts, Cambridge: MIT.

---------------- (1995) *The Minimalist Program.* Massachusetts: MIT

Comrie, B. (1975). *Aspect.* Cambridge: Cambridge University Press.

Cook, V & M. Newson (1988). *Chomsky's Universal Grammar: An Introduction.* Oxford: Blackwell Publishers Ltd.

Crystal, D. (1990). *A Dictionary of Linguistics and Phonetics.* Oxford: Blackwell Publishers.

Gachono, (2004). *Tense, Aspect and Mood – Morphosyntactic Verb Inflections in Kikuyu.* Unpublished M.A. Thesis, University of Nairobi.

Guthrie, M. (1948). *The Classification of Bantu Languages.* Oxford: Cregg Press.

Habwe, J & P. Karanja (2004). *Misingi ya Sarufi ya Kiswahili.* Nairobi: Phoenix Publishers.

Haegeman, (1994). *Introduction to Government and Binding*. Oxford. Blackwell Publishers.

Horrocks, G. (1987). *Generative Grammar*. London: Longman.

Ilongo, A.P. (1983). *A Functional approach to the Morphology of Verrbal Extensions in Kidawida with Comparative Statements of the same phenomenon made with respect to Kiswahili*. Unpublished M.A. Thesis: University of Nairobi.

Iribehmwangi, P. I. (2008). *A Synchronic Segmental Morphophonology of Standard Kiswahili.* Unpublished PhD Thesis: University of Nairobi.

Jerono, P (2003). *Kishazi Huru Arifu cha Kiswahili: Mtazamo wa X-ba.* Tasnifu ya M.A ambayo haijachapishwa, Chuo Kikuu cha Nairobi.

Kapinga, M.C. (1983). *Sarufi Maumbo ya Kiswahili Sanifu*. Dar-es-Salaam: TUKI.

Karimi, B. (2008). *Njeo na Hali katika Lugha ya Kiswahili Sanifu: Mtazamo wa Uminimalisti.* Tasnifu ya M.A ambayo haijachapishwa: Chuo Kikuu cha Nairobi.

Kaviti, L. (2004). *A Minimalist Perspective of the Principles and Parameters in Kikamba Morpho-syntax*. Unpublished PhD Thesis: University of Nairobi.

Kihore, Y.M. et al (2003). *Sarufi Maumbo ya Kiswahili Sanifu (SAMIKISA): Sekondari na Vyuo.* Dar-es- Salaam: TUKI.

Kulikov, L. et al (2006). *Case, Valency and Transitivity.* Amsterdam. John Benjamins Publishing Company.

Maringah, E. (1987). *A Comparative Analysis of Verbal Extensions in Kimbeere and Kiswahili.* Unpublished M.A Thesis: University of Nairobi.

Massamba, D. et al (1999). *Sarufi Maumbo ya Kiswahili Sanifu*. Dar-es-Salaam. TUKI.

--------------------- (2004). *Kamusi ya Isimu na Falsafa ya Lugha*. Dar-es-Salaam: TUKI.

Mbaabu, I. (1985). *Sarufi ya Kiswahili.* Nairobi: Kenya Publishing and Book Marketing Company Ltd.

Mdee, J.S. (1986). *Kiswahili: Maumbo na Matumizi Yake*. Nairobi: Intercontinental Publishers.

Mgullu, R.S. (1999). *Mtalaa wa Isimu: Fonetiki, Fonolojia na Mofolojia ya Kiswahili.* Nairobi: Longhorn Publishers.

Munyao, M.K. (2006). *The Morpho-syntax of Kikamba Verb Derivations: A Minimalist Approach.* Unpublished M.A Thesis, University of Nairobi.

Mwalili, N. (2008). *Mofosintaksia ya Kishazi Nomino cha Kiswahili: Mtazamo wa Uminimalisti,* Tasnifu ya M.A, Chuo Kikuu cha Nairobi, ambayo haijachapishwa.

Oichoe, M.P. (2005). *Ulinganishi wa Kirai Tenzi cha Kiswahili na Ekegusii Kimofosintaksia: Mtazamo wa Uminimalisti.* Tasnifu ya Shahada ya Uzamili ya Chuo Kikuu cha Nairobi, ambayo haijachapishwa.

Ouhalla, J. (1991). *Functional Categories and Parametric Variation.* London: Routledge.

Polome, E. (1967). *Swahili Language Handbook.* Washington D.C: Center for Applied Linguistics.

Radford, A. (1992). *Transformational Grammar of the English Language*. London: Longman.

.................... (1997). *Syntactic Theory and the Structure of English: A Minimalisti Approach.* Cambridge: Cambridge University Press.

Schroeder, H. (2002). *Word Order in Toposa: An Aspect of Multi-feature Checking.* Unpublished PhD Thesis, University of Nairobi.

------------------ (2005) *Hand-out on Minimalist Program* as presented in a seminar on 12th April, 2006 at the University of Nairobi.

Singleton (2000). *Language and the Lexicon: An Introduction.* Great Britain: Arnold.